**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais. |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |

| | |
|---|---|
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |

| | |
|---|---|
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Disemba, 2013**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na virusi vya UKIMWI na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na virusi vya UKIMWI na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 28**

**Kuchukuliwa Mashamba ya Mikarafuu**

**Mhe. Omar Ali Shehe (Kny: Mhe. Hija Hassan Hija)-** Aliuliza:-

Mara tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964, serikali iliamua kuwapa wananchi mashamba ya mikarafuu na kuyaendeleza ambapo wananchi hao. Wamefanya kazi hiyo kwa muda mrefu bila ya kuingiliwa kati na serikali au

taasisi yoyote. Kwa bahati mbaya hivi karibuni wamejitokeza baadhi ya maafisa wa serikali kupita na kuyachukua ama kuyakodisha mashamba hayo.

(a) Je, maamuzi ya Mzee Karume yamefutwa na kutolewa maamuzi mapya.

(b) Tangu kuanza kwa zoezi hilo ni mashamba mangapi yamechukuliwa na kupewa watu wengine.

(c) Kwa yale yaliyoidhinishwa ama kuuzwa ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana na zimeingia mfuko upi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 28 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Maamuzi ya Mzee Karume hayajafutwa na bado tunaendelea kuyaheshimu na kuyaendeleza na kuyaenzi na ndio maana mashamba yote yenye mikataba halali yamerikodiwa tu na wala hayakukodishwa.

   Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba hakuna mtu mwenye warka halali ambaye shamba lake limekodishwa na serikali. Hata hivyo, wamiliki wengi wao wamevunja makubaliano hayo kwa kuyatelekeza mashamba kwa jamaa zao, ndugu zao na hata wengine kudiriki kuyarejesha kwa jamaa ambao waliokuwa nayo kabla ya Mapinduzi kinyume na mkataba huo uliopo.

b) Mhe. Naibu Spika, tangu kazi ya uhakiki ilipoanza hakuna shamba lolote lililochukuliwa na kupewa mtu mwengine. Hata hivyo, kazi ya uhakiki itakapomalizika hatua ya kuwapatia wananchi mashamba ambayo hayana wamiliki halali zitachukuliwa. Hali hii ni pamoja na watu ambao wameomba au watakaoomba, ambapo kipaumbele pia kitakuwa kwa wale waliokuwa wakiendeleza na kuyashughulikia bila ya kuwa na umiliki halali.

c) Jumla ya mashamba yaliyokodishwa hadi sasa 453 na jumla ya shilingi 215,507,500/= zimepatikana na kuingizwa katika serikali kama ni mapato ya serikali.

**Utaratibu**

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Naibu Spika, mimi niko kwenye utaratibu na sio kwenye swali hasa. Maana yake kifungu cha 37(1) natumia hicho, wakati alipokuwa anajibu Mhe. Naibu Waziri, hapa swali (c) lilikuwa linaelezea mashamba ambayo yameuzwa, lakini yeye amejibu kwamba mashamba yaliyokodishwa, wakati swali la msingi linasema yaliyouzwa ni mangapi na sio yaliyokodishwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri, mashamba yaliyouzwa kama yapo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Naibu Spika, hakuna shamba hata moja ambalo limeuzwa katika mashamba ambayo yaliyochukuliwa na Wizara ya Kilimo, isipokuwa ni mashamba ya mikarafuu yaliyokodishwa tu.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna mashamba ambayo hayana wamiliki halali na kuwa watu mashamba hayo wanayashughulikia. Je, Wizara ya Kilimo na Maliasili itawasaidia vipi watu hawa ambao wenye mashamba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Naibu Spika, kwanza mashamba haya wamepewa nafasi kubwa hao ambao wanayo kuyakodisha na ikiwa mashamba haya yamekodishwa na mtu mwengine, basi hurejeshewa zile gharama walizotumia katika usafishaji wa mashamba hayo.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mashamba haya yalitambulika katika shehia, hivi shehia zenyewe ni ngapi na zipi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Naibu Spika, shehia zote ambazo zilizotambuliwa mashamba haya ni shehia 39. Kwa mfano Mkoani zimegundulikana shehia 15, Chake Chake shehia 8, Wete shehia 10 na Micheweni shehia 6

**Nam. 24**

**Kuhamishwa Kitengo cha Macho na Kukosekana Huduma Muhimu ya *CT Scan* katika Hospitali ya Mnazimmoja**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub –** Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 24 naomba kutoa maelezo yafuatayo. Napenda kuinasihi sana Wizara ya Afya kwamba kuna wanafunzi walioandikishwa Chuo cha Afya Mbweni wamefukuzwa sababu haijajulikana na wengine wamechukuliwa fedha zao mpaka hivi sasa ni mwezi wa 4 au 5 na wala hawajarudishwa kwa ajili ya kuendelea na masomo.

Kwa hivyo, ninaomba kama chuo hakitaki wanafunzi wale kuendelea na masomo basi ni vyema wanafunzi wale warejeshewe haki yao, kwa sababu wale watoto ni wa kinyonge na wengine wanajua namna gani walivyopata fedha.

Baada ya Maelezo hayo, naomba swali langu Nam. 24 lipate jawabu.

Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja inategemea kuwa Hospitali ya Rufaa nchini, maana yake ni kuwa kesi zote za maradhi zitakazoshindikana vituo vyengine vya afya zitafikishwa Mnazi Mmoja kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi zaidi. Na kwa kuwa hivi karibuni kitengo cha matibabu ya macho cha Hospitali hiyo kimehamishiwa Hospitali ya KMKM iliyopo Kibweni. Kwa kuwa huduma muhimu ya *C-T Scan*, haifanyikazi hospitalini hapo.

(a) Serikali haioni kuwa wananchi wanaotoka maeneo ya mbali mfano Kusini Unguja au Kisiwani Pemba watasumbuka kufuata huduma za matibabu ya macho Kibweni.

(b) Wizara inajuwa kuwa huduma ya *C-T Scan* haifanyikazi na wananchi wanasumbuka kupata huduma hiyo muhimu.

(c) Kutokana na changamoto hizo serikali haioni kwamba haijajipanga sawa sawa kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri wa Afya, majibu pamoja na maelezo uliyopewa yachukuwe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Nataka nisikubaliane na hoja aliyoijenga Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wanaotoka Kusini ya Unguja na Pemba watasumbuka kufuata huduma za utibabu wa macho Kibweni, kwa sababu kuna usafiri wa uhakika kutoka Kusini na wakifika Mjini wanaunganisha na daladala za Fuoni zinazoelekea Bububu au wanaotoka Pemba halikadhalika wakishuka Forodhani wanaelekea kwa Bakhresa ili kupanda daladala za Bububu kwenda Kibweni kufuata huduma za macho ndio anaona ni usumbufu. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo Mhe. Mwakilishi, anapendekeza turudishe huduma za macho Mnazi Mmoja kwa sababu ndio hospitali ya rufaa wakaangukiwe na jengo.

Wizara ya Afya kama taasisi ya kukinga na kutibu, ushauri huo hatuwezi kuukubali na kusema la haki hili ndilo lalamiko la kwanza tuloanza kulipata, kwani wagonjwa wakifika Hospitali ya Mnazi Mmoja wanafahamishwa na wanakwenda bila ya malalamiko.

Wizara tunachokumbuka wakati wa bajeti kati yao Waheshimiwa Wawakilishi hawa hawa walilalamikia jengo hilo hilo kuwa ni bovu, ilibidi huduma za macho zikahamishiwa Kibweni, kwani ndipo tulipopata nafasi ya kutosha kufanya matibabu ya nje na ya kulaza wagonjwa kwa wakati huo.

Baada ya kufanya hivyo, ndipo tulipoanza kujiangalia katika wizara yetu wapi tengeweza kuihamishia huduma hiyo na hatimae tukafikia uamuzi wa kupeleka huduma za wagonjwa kwa wagonjwa wa nje hapo kwenye kituo cha Kwamtipura na kopi ya barua ya uhamisho huo kapelekewa mpaka Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na kwa wagonjwa wa kulazwa kwa upasuaji watakuwa wanatumia wodi ya masikio, pua na koo kwa kupokezana kila wiki. Wiki moja macho na wiki inayofuata masikio, pua na koo. Wagonjwa wa dharura wanalazwa pamoja na wagonjwa wengine katika wodi za upasuaji. *(Makofi)*

(b) Hata kama tukijipanga kiasi gani changamoto ndio sehemu ya maendeleo, vitu na majengo vitachakaa na vitahitaji ukarabati na kufanyiwa matengenezo madogo au kusafishwa, yaani *service* muda

wake ukifika.*CT Scan* inatoa huduma kwa idadi ya wagonjwa iliyopangiwa na baadae ifanyiwe *service*. Sasa hiyo haina maana kwamba imeharibika bali husimamishwa shughuli zake kwa muda ili *service* ifanyike. Bahati mbaya mafundi wa kazi hiyo hawapatikani hapa Zanzibar. Kwa hiyo, huwa tunawaita na tunasubiri zamu yetu ikifika wanakuja na hii inategemea wanakazi kiasi gani huko waliko nasi tunaunganisha foleni.

(c) Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ndiyo hospitali ya rufaa kwa Zanzibar ina matawi matatu Mnazi Mmoja yenyewe, Muembeladu na Kidogochekundu. Pia, inaweza kuwa na matawi ya ziada popote pale pindipo yatahitajika. Kwa vile huduma zinazotaka kutolewa katika hospitali hiyo zinaongezeka, ndio maana wamepewa kiwanja sehemu nyengine Binguni Wilaya ya Kati mbali kuliko hata Kibweni ili kutanua huduma kama Tawi.

Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa rufaa haizuiwi na hilo la umbali wa tawi lake jengine kwa maana tafsiri halisi ya rufaa ni aina ya huduma zinazo patikana hospitalini hapo au kwenye Tawi lake na ambazo hazipatikani katika hospitali nyengine. Kwa mantiki hiyo serikali inachokifanya ni kuendelea mbele na kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa na si vingenevyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya kama Wizara ya Afya yenyewe ilivyo. Naomba alifahamishe Baraza hili, anasema ameweka usafiri wa uhakika, hivi Wizara ya Afya imeweka usafiri wa uhakika kutoka kwa Bakharesa kuelekea Kibweni.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya baadhi wa wafanyakazi wa hospitali hiyo na mimi mwenyewe nikiwemo leo Kanuni zetu za Baraza zinakataza kusema uongo. Mimi nimekwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo hivi sasa ni wiki ya tatu *CT Scan* haifanyikazi na hata hivi asubuhi kabla ya kuja kuuliza swali hili *CT Scan* haifanyikazi, wakati Kanuni zetu zinatukataza kusema uongo. Kwa hivyo, naomba kwanza Mhe. Naibu Waziri, kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aombe radhi kabla ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, kabla ya kuomba radhi Mhe. Naibu Waziri, ni kwamba nilivyofahamu mimi amejibu kwamba *CT Scan* inapoharibika wataalamu hawapo hapa wanaagizwa kutoka nje na wakipata nafasi wanakuja kuitengeneza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, wakati alipojibu swali la msingi Mhe. Naibu Waziri wa Afya alisema kwamba *CT Scan* inafanyakazi, lakini kwa huduma ndogo au watu kidogo, wakati haifanyikazi hata kidogo na rikodi zipo na *hansard* naweza kwenda kuchukua Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri, majibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, sikusema hivyo.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, na mimi nimesikia vyengine na nimemwambia hapa. Kwa hivyo, tunaendelea.

**Utaratibu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, nilichomwambia Mhe. Naibu Waziri wa Afya narudia tena ni kwamba hichi chombo ni cha wananchi *CT Scan* hakifanyikazi, mimi asubuhi nimekwenda kumpeleka mgonjwa kuhakikisha kwamba *CT Scan* haifanyikazi, leo ni wiki ya tatu, sasa yeye anatuambia kwamba inafanyakazi kwa huduma ndogo ndogo ambapo kitu hicho si kweli.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Naibu Waziri wa Afya kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aombe radhi na wala si aibu kusema kwamba ninaomba radhi na kama anataka twende na watu na kamati ipo tukathibitishe hicho kitu na itakuwa siku zote watu hatuwafanyii kazi wananchi Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, kaa kitako. Mhe. Naibu Waziri wa Afya unayo maelezo ya ziada.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, narudia kusema tena hivyo anavyosema sivyo nilivyosema.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri wa Afya, rejea ulivyozungumza.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, hivyo anavyosema yeye sivyo nilivyosema, isipokuwa nilivyosema ni hivi … *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tusikilize.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, nimeanza hivi sentensi hata kama tukijipanga kiasi gani changamoto ni sehemu ya maendeleo, vitu na majengo vitachakaa na vitahitaji ukarabati na kufanyiwa matengenezo

madogo madogo au kusafishwa (*service*) muda wake ukifika na hivyo ndivyo nilivyoanza.

Baadaye nikasema hivi *CT Scan* inatoa huduma kwa idadi ya wagonjwa iliyopangiwa na baadaye ifanyiwe *service*, sasa hiyo haina maana kwamba imeharibika bali husimamishwa shughuli zake kwa muda ili *service* ifanyike. Kwa bahati mbaya mafundi wa kazi hiyo hawapatikani hapa Zanzibar. Kwa hiyo, tunawaita na tunasubiri zamu yetu ikifika wanakuja na hii inategemea wana kazi kiasi gani huko waliko na sisi tunaunganisha foleni. Haya, hayo madogo madogo nimesema saa ngapi. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nadhani jawabu limetolewa kwamba *CT Scan* inafanyiwa *service* na inasimamishwa kwa muda na baadaye inaendelea kufanya kazi na hivi sasa inafanyiwa *service* haifanyikazi. *(Makofi)*

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, sawa anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa hivyo hivyo twendeni nitauliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Kiasi gani cha fedha zilitumika kwa ajili ya kukarabati jengo lile la Macho mwaka na leo hii tunaambiwa jengo lile halifai na kuhamishwa kitengo kile cha Macho kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na kupelekwa Hospitlai ya KMKM Kibweni.

b) Vifaa vya uchunguzi ikiwemo *CT Scan* pamoja na vifaa vyengine vya *ICU*, mafundi wake hapa hawapatikani kwa nini na wakati mafundi wapo hapa, kwa nini hawawezeshi mpaka tusubiri na mtegemea cha ngudu hufa masikini Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli mafundi wapo kwenye kitengo, lakini kwa nini hawawapi elimu ya kutosha, mimi ninachofahamu ni kwamba mpaka hivi sasa *CT Scan* haifanyikazi na wananchi wanateketea.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, sijafahamu swali.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, Mhe. Naibu Waziri wa Afya anasema swali hajalifahamu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, uliza taratibu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika.

a) Ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kwa ajili ya kukarabati Jengo la Macho na leo hii tunaambiwa huduma zimesitishwa kutokana na uchakavu wa jengo wakati matengenezo yalifanyika mwaka jana. Kwa hivyo, nini kilichotengezwa na serikali na kiasi gani cha fedha zimetumika.

b) Vifaa vya uchunguzi ikiwemo *CT Scan* pamoja na vifaa vyengine vya *ICU,* mafundi lazima wanatoka nje, kuna faida gani ya kuwa na Kitengo cha Mafundi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri, umeyafahamu maswali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, jibu la mwanzo hilo lilizungumzwa kwa uwazi wakati wa bajeti kuhusu fedha zilizotumika, kiasi gani na kama hakuwepo mimi hilo silirudii.

Vile vile, kuhusu *CT Scan* mafundi waliopo hawana ujuzi wa hilo ndio maana tunaagiza mafundi kutoka nje. *(Makofi)*

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi sitaki kujua kiasi cha fedha isipokuwa swali langu ni dogo. Lengo la serikali yetu ilikuwa ni kuboresha Kitengo cha Huduma za Macho ili iweze kufanyakazi kwa ufanisi na ndio maana serikali ikatoa gharama za kufanya marekebisho kitengo kile.

Kwa hivyo, ninachotaka kujua baada ya kufanyiwa hayo matengenezo, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kuondosha huduma ya macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kupeleka Hospitali ya KMKM Kibweni baada ya kutumia fedha nyingi za wananchi kwa ajili ya matengenezo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, fedha zilitumika kwa ajili ya kutengeneza sehemu ya paa ya jengo hilo. Lakini jengo lile ni la kizamani na limejengwa kwa kutiwa dari ya udongo, baadaye likafungwa kupitia kwenye dari ikawekwa *hardboard*, ili kukinga ile hali na ikawa ile sehemu ya udongo na dari ya zamani haionekani. Sasa katika kufanya hivyo ndipo tatizo lilipotokea na huko ndiko kunakotokea matatizo ya hilo jengo.

Kwa ujumla jengo lenyewe ni jengo zima, isipokuwa kwenye paa ndio kunakotatizo, kwa sababu ile ni nyumba ya kizamani na imejengwa kwa utaratibu mwengine na ukarabati uliofanywa kwa utaratibu wa kileo. Kwa hivyo, hivyo vitu hivyo viwili havikukubaliana na limeachana *hardboard* kule juu na matatizo ndio yametokea na hicho ndicho kilichotokea.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Kwa hivyo, hiyo ndio sababu ya msingi kuondoshwa wagonjwa pale na kupelekwa Hospitali ya KMKM Kibweni.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, wao walilalamika na walikuja Waheshimiwa Wawakilishi na kamati hiyo hiyo na wakasema kwamba jengo bovu tuwahamishe watu na tukakubaliana tukawahamisha na hiyo ndio sababu ya msingi. Lakini hivi sasa ninavyokwamba kuna askari polisi pale wanakaa humo humo.

**Nam. 59**

**Serikali Kuzipatia Skuli Huduma ya Maji Bila ya Malipo**

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa –** Aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inatoza huduma ya maji hata katika skuli na kwa kuwa skuli zetu hazina uwezo wa kulipia huduma hii jambo ambalo hupelekea kukatwa kwa huduma hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kulipia huduma hiyo katika skuli zake badala ya kuziachia skuli hizi kulipa wenyewe.

(b) Je, Serikali haioni kuwa imefika wakati kuruhusu skuli kupatiwa huduma hii bila ya malipo, ili kulinda afya za walimu na wanafunzi.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 59 lenye sehemu (a) na (b), kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Waziri wakati anajibu, baadaye mnakuja kuuliza maswali wakati tayari yameshajibiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya swali hayo, napenda kueleza yafuatayo. Skuli zangu zote za Unguja na Pemba zimeruhusiwa kukusanya mapato kupitia kwenye Kamati zao za Skuli na kutumia fedha hizo wenyewe bila ya kuingiliwa na serikali katika masuala ya kulipia maji, umeme na kadhalika.

Hadi hivi sasa ninavyozungumza sijapata kusikia kwamba kuna skuli imekatiwa maji kwa sababu haijalipa maji na kama ipo skuli ya aina hiyo, basi naahidi kwamba tukimaliza Baraza hili tunayo ziara ya kutembelea skuli zote za Unguja na Pemba kwa ajili ya kutizama tatizo hilo kama lipo, kama lipo basi tutawalazimisha Walimu Wakuu watupe hesabu ya fedha wanazopokea kwa wananchi, wanazifanya nini.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 59 kama hivi ifuatavyo:-

a) Kwa hivi sasa hakuna skuli hata moja ninayoijua ambayo imekatiwa maji kwa sababu imeshindwa kulipa. Lakini kama skuli hiyo ipo basi nitachukua juhudi mimi mwenyewe kuzipitia skuli zangu na kuhakikisha kwamba tatizo hilo kama lipo au halipo na kama lipo, basi nitauliza kwa nini lipo na Walimu Wakuu wanipe hesabu ya fedha wanazokusanya na jinsi gani wanavyotumia mpaka wakashindwa kulipa maji.

b) Kilio cha serikali kuzilipia skuli hizi gharama za maji, Waziri anayehusika amezisikia. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba skuli hizi ni nyingi na fedha za serikali zinazotiwa kwenye bajeti hii ni kidogo. Kwa hivyo, serikali haiwezi kulipia gharama za maji za skuli hizi. Kwa kweli nitashukuru sana kama tukizungumza na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na akilikubali suala hilo la kulipia skuli gharama za huduma za maji, basi nitashukuru sana.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Wakati alipokuwa akijibu swali mama Mhe. Waziri amesema kwamba wameziruhusu skuli zote za Unguja na Pemba kutumia fedha zinazokusanywa kwa ajili ya Kamati za Maendeleo.

Kwa hivyo, napenda kumuulia Mhe. Waziri kwa sababu skuli zote za Unguja na Pemba hazina miradi ya maendeleo ya aina yoyote ile na kuwaruhusu kwamba watumie fedha hizo na wakati hawana miradi ya maendeleo.

a) Je, haoni kama inasababisha skuli kuwachangisha sana vijana wetukutoa michango mingi kwa ajili ya kulipia huduma zao na wakati hawana miradi ya kupatia fedha za maendeleo.

b) Je, kwa kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza mwaka 1964 kwamba elimu bure, lakini hivi sasa

tunachangia tu kidogo. Hivyo, hakuna haja ya serikali kusaidia malipo mengine ya skuli kwa ajili ya kupunguza michango kuwa mingi zaidi.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, ameuliza Mhe. Mwakilishi kwamba hatuoni haja ya kuisaidia miradi ya maendeleo ya skuli hizi kwa sababu fedha wanazokusanya hawa ni kidogo sana.

Kwanza nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba miradi ya maendeleo ya skuli ipo mingi sana. Kwa mfano ukarabati wa majengo, kuta, sakafu na kadhalika ni sehemu ya maendeleo ya skuli. Kwa hivyo, hivi vyote tumeahidi na tunatekeleza ahadi zetu ili kuzisaidia hizi skuli kwa sababu gharama zake ni kubwa sana.

**Nam. 20**

**Mkakati wa Kupata Walimu wa Michezo Kutoka Nje**

**Mhe. Saleh Nassor Juma –** Aliuliza:-

Katika kuinua kiwango cha soka kwa upande wa Tanzanzia Bara, Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, aliajiri kocha wa mpira wa miguu kutoka Brazi l- Marcio Maximo hapo zamani na hivi sasa ameajiriwa Kim Poulsen kutoka Denmark, kuna taarifa kuwa yumo mbioni kuajiri kocha wa mpira wa kikapu toka Marekani kwa ajili ya kuendeleza mchezo huo.

Je, ni lini serikali yetu itaajiri makocha toka ughaibuni, ili kuendeleza tasnia ya michezo kama ilivyofanya siku za nyuma pale ilipomuajiri Tambwe Lea kutoka nje ya nchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 20 kama hivi ifuatavyo:-

Katika kuinua kiwango cha soka, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilimuajiri kocha wa kigeni Marcio Maximo, kwa ajili ya kufundisha mpira wa miguu. Kwa azma kama hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijawahi kuajiri kocha kutoka nchi za Kiarabu, lakini imekuwa ikipokea makocha wa soka kutoka Misri wanaokuja kwa njia ya msaada. Makocha hawa wanaokuja kwa ajili ya kufundisha timu za vijana kwa kusaidia Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu umetuletea mafanikio makubwa ya soka, kwani tumekuwa na makocha wetu wengi wazalendo wa kuendeleza kazi zao.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Naibu Spika, mafanikio ya jambo lolote ni pale tija ya jambo hilo inapopatikana. Na kwa kuwa Timu yetu ya Taifa kila siku inaendelea kufanya vyema ikiwemo hata katika mashindano ya *CECAFA* yaliyomalizika jusi, leo nasema imepata mafanikio.

(a) Je, Mhe. Naibu Spika, anaonaje Mhe. Naibu Waziri, akafuata taratibu za wenzetu, timu yetu ya taifa kuweza kufanya ziara katika nchi za ughaibuni kama vile Brazil, kama walivyofanya Timu ya Simba katika miaka ya 1980 walipokwenda kule na wakafanya ziara pale, wakachukua ile *style ya Canivosamba* na kufika hapa wakachukua ubingwa zaidi ya mara nne. Haoni sasa timu yetu ya taifa kuna haja ya kuipangia ziara hiyo katika nchi za ughaibuni kama Brazil, Uingereza na kadhalika ili kuwafanya vijana wetu kuwa makini katika kulisakata kabumbu.

(b) Kwa kuwa mwenzetu Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kaajiri makocha mara mbili tena alikuwa analipa fedha yeyé mwenyewe makocha hao kwa mujibu wa taarifa nilizonazo. Je, ni lini serikali yetu kupitia Rais wetu tunayempenda sana Mhe. Ali Mohamed Shein ataajiri makocha wa nje ili na timu yetu iweze kufanya vizuri na vijana waweze kufarijika katika tasnia ya kabumbu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, nakubaliana sana na yeye, lakini nataka nimwambie kitu, kama ni kuzisafirisha timu zetu basi kwa kweli tutazisafirisha, lakini pia namuomba Mhe. Mwakilishi watuongezee bajeti yetu iwe kubwa ili tuweze kuzisafirisha timu zetu hizo kwenda nje.

Vile vile, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba, timu yetu kama juzi alivyoeleza Mhe. Waziri wangu kuwahakikishia Wajumbe kuwa timu yetu haikukwama, nataka niseme mgeni anayekwenda katika nchi yoyote kucheza mpira lazima atashindwa. Kwa sababu anapoingia kiwanjani anaingia kwa muono wake. Hilo nataka Waheshimiwa mlijue.

Jengine Mhe. Mwakilishi namuomba sana tushirikiane pamoja ili tuweze kuendeleza soka ya Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, baada ya uteuzi wa kocha wetu wa Timu ya Taifa ya Zanzibar, Ndugu yetu Bausi wakati wa kutafuta wachezaji wa Timu ya Taifa kulitokea mgogoro namna ya kuwapata wachezaji wa kutuwakilisha taifa hili la Zanzibar, mgogoro ambao ulianza tangu mwaka jana kutokana na malipo yaliyopatikana baada ya kushinda nafasi ya tatu Zanzibar.

Matokeo yake Mhe. Naibu Spika, uteuzi ule haukuwaridhisha Wazanzibari wote baada ya kuachwa kwa baadhi ya wachezaji wakiwemo kina Aggrey Moriss, Cannavaro, Mwadini na wengineo hatimae kocha yule alipeleka wachezaji ambao hawana uzoefu na kuifikisha timu hii katika kutolewa hatua ya awali.

Je, alikuwa akifahamu mgogoro uliojitokeza kati ya kocha na wachezaji wa Timu ya Taifa. Kama alikuwa anaufahamu kama wizara imechukua hatua gani kuhakikisha tatizo lile haliwezi kuendelea ili kudhoofisha michezo katika nchi yetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, sisi kama wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa na *ZFA* suala hili tunalijua na kwa kweli Mhe. Mwakilishi hata kama ni wewe una timu yako utawaambia wachezaji waje kwa siku maalum, ukawapigia simu hasa kuwaambia njooni kwa ajili ya safari au kuandaa kambi wakadharau na wewe hukubali. Sasa kwa hilo kocha wetu tusimtie kwenye matatizo, hatuwezi tukampembejea mtu kwa kitu alichokuwa hakitaki.

Mhe. Mwakilishi nataka nikwambie wizara inajua na Baraza la Taifa linajua pamoja na *ZFA*, lazima tulione hilo na tuangalie jamani tusimpembejee mtu kwa kitu alichokuwa hakitaki.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali imekuwa ikichukua kila jitihada kuleta makocha kutoka nje ikiwemo kutoka Misri kusaidiana na makocha wazalendo, lakini kinachoonekana chanzo cha soka kushuka ni *ZFA.*

Je, ni lini wataivunja *ZFA* kuunda *ZFA* ya kileo ili soka ipate sura nzuri.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa umahiri wake wa kujibu maswali ya Wawakilishi na namshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa swali lake zuri.

Ni kweli kwamba kwa muda mrefu matatizo ya mpira wetu wa Zanzibar ulikuwa unasababishwa na migogoro ndani ya Chama cha Mpira wa Miguu (*ZFA*). Sasa hio hasa ndio siri ya kutokuwa na mafanikio mazuri, lakini nashukuru kwamba uchaguzi uliofanywa miezi mitatu, minne tayari umeweka safu nzuri sana ya *ZFA* makini na naamini kwamba kwa *ZFA* ile iliyopo tukipata mashirikiano ya wadau wa soka ndani, basi tutapata mapinduzi makubwa katika medani ya mpira wa miguu Zanzibar.

Ninachowaomba wapenzi wa mpira wa miguu wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watoe ushirikiano mzuri kwa timu ile makini ya *ZFA* iliyochaguliwa ili kuwezesha kuleta mafanikio makubwa katika mchezo wa mpira wa miguu Zanzibar, imeanza vizuri naamini ikipata mashirikiano hayo basi yale ya nyuma kwa kweli tutaweza kuyasahau.

**Nam. 14**

**Faida Iliyopatikana Baada ya Matengenezo ya Meli ya *L.C.T* Jitihada**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Meli ya Jitihada inayomilikiwa na Shirika la Bandari imetumia gharama kubwa sana kufanyiwa matengenezo.

Je, ni faida kiasi gani imepatikana tokea meli hiyo kumaliza matengenezo na kuanza shughuli zake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano**- Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Meli ya *LCT* Jitihada, ilianza shughuli za kibiashara kwa majaribio mnamo mwezi wa Mei, 2011 baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa na Shirika la Bandari kwa kufanya safari katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Aidha, baada ya kukatiwa Bima meli hiyo ilianza rasmi shughuli za kibiashara mnamo mwezi wa Machi, 2012 na kuanza safari za nje ya Zanzibar kwa bandari za hapa pamoja na Tanzania Bara. Kwa vile muda wa meli hiyo kufanya biashara ni mdogo tangu ilipoanza kazi hiyo, bado haijaweza kurudisha gharama zilizotumika kuifanyia matengenezo.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa meli hiyo inajiendesha kwa faida kulingana na matumizi kama yale ambayo yamekusudiwa. Ni matarajio yetu chombo hiki kiendelee kuwa kizima na kufanya kazi zake vizuri, hatuwezi kutegemea faida kubwa katika kipindi hiki kidogo ambacho chombo hiki ndio kimeanza kazi ya kibiashara.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kanuni za biashara zinasisitiza umuhimu wa faida na gharama za uendeshaji pamoja na kutokulipishwa kodi za ada ya bandari imekuwa ni mzigo wa Shirika la Bandari.

Je, mnafikiria vipi meli hio kuikodisha au kuiuza ili kuipunguzia mzigo, kwa sababu hata wenyewe watu wa bandari hivi sasa wana hofu kuja kuula mtaji wa bandari, ukitizama kwamba meli ile imetengenezwa kwa gharama kubwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, anachokisema Mhe. Mwakilishi kwamba meli hii imekuwa ni mzigo na kwamba tunaliathiri Shirika la Bandari. Mimi niseme kwamba sina hakika, lakini sikubaliani na kauli hiyo kwa sababu naamini wizara yetu ndio sehemu ya kuisemea Shirika la Bandari. Kama Shirika la Bandari wangekuwa na tatizo hili wangekuja wakatuona tukafanya mazungumzo nao wakatueleza.

Lakini jambo la msingi ambalo nataka kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kama tulivyoeleza katika majibu mama kuwa meli hii imemaliza matengenezo na kuanza biashara mwezi Mei, 2012. Katika kipindi hiki hatuwezi kutarajia kwamba irejeshe gharama zote na ilete faida kama hivyo ambavyo tungetarajia. Malengo yetu kwamba tuipe muda meli hii ifanye kazi bila shaka kwa mujibu wa utaratibu unaokwenda faida itaonekana, hakuna mwenza ambaye anapata mapato chini ya shilingi milioni 20, 25 mpaka 30.

Kwa hivyo, matarajio yetu kwamba ikipata muda, kazi zikienda vizuri, ikiendelea kuwa nzima meli hii itazalisha na itakuwa na tija, kama kutakuwa kuna haja ya meli hii kuondoa Shirika la Bandari watatueleza na sisi kama serikali tutalizingatia hatutoona ulazima wa kuibakisha hapo ilipo.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Katika siku za karibuni pale Bandari ya Mkoani *crane* imeharibika kwa sababu hiyo watu hawawezi tena sasa kupakia magari yao katika meli yetu ya Serengeti na Maendeleo, wanategemea Meli ya *Sea link* ya Said Salim Bakhresa ambayo gharama za uchukuzi ni kubwa mno kiasi ambacho watu wengi wamevunjika moyo.

Je, kwa sababu Shirika la Bandari ni shirika la serikali, Meli ya Jitihada kwa nini haifanyi *route* za kawaida kwenda Pemba kwa sababu haihitaji *crane* ili iweze kuwasaidia wananchi wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, meli hii inafanya biashara kati ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam na kama wananchi hao watakuwa na mizigo utaratibu uko wazi, ni kufuata wahusika pale watapakia mizigo yao itakwenda Pemba na hakuna kikwazo kinachowakwaza kwamba meli hii kwa nini isiende Pemba. Msingi ni kwamba waende mapema kwa sababu pengine wanakuwa na tenda za watu wengi.

Kwa hivyo, waende mapema wakutane na uongozi watapangiwa siku watapakia mzigo wao utakwenda Pemba kama inavyokwenda mizigo mingine katika maeneo mengine, ikiwemo Pemba, Tanga pamoja na Dar es Salaam.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi kwanza nitoe shukurani kwa Shirika la Bandari kwa kufanya jitihada kubwa sana ya kuifanyia matengenezo Meli ya Jitihada kutoka hali mbovu iliyokuwa mpaka ikawa inafanya kazi.

(a) Nilitaka kujua hasa shirika lilitumia kiasi gani cha fedha katika matengenezo ya meli ile mpaka ikaweza kufanya kazi kama inavyofanya hivi sasa.

(b) Kutokana na uchakavu wa meli ilivyo na muda mrefu wa kuishi ningeliomba kujua kwa kila safari inayofanya meli hii kwa gharama zake zote pamoja na malipo ya wafanyakazi na faida inayopatikana hii meli inafanya kazi kwa faida au kwa hasara.

(c) Wizara ili isije ikatumia fedha nyingi sana za matengenezo kwa vile hiki ni chombo kinatumika, imefanya tathmini kuwa hii meli inaweza ikaishi kwa muda mrefu zaidi au kutokana na hali ilivyo ishafika wakati kuwa itafutiwe yeyote anayeiweza ainunue kwa kukimbia hasara inayofuatia huko mbele.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:**

(a) Mhe. Naibu Spika, Meli hii tunayoizungumza hapa ya *LCT* Jitihada ilikuwa ni meli ambayo inamilikiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mwaka 2007 meli hii ikaanza kutengenezwa na Shirika la Bandari kwa gharama zao hadi mwaka 2011. Gharama ambayo kwa ujumla kutoka mwaka 2007 mpaka 2011 imetumia takriban shilingi

2.6 bilioni kukamilika matengenezo yake, na matengenezo haya yamekamilisha mashine, jenereta, *plate* pamoja na *overhaul* yote ya meli nzima, kwa maana kwamba meli hii sasa inaonekana kama imekuwa mpya kulingana na hali iliyokuwa na matengenezo ambayo yamefanyika.

(b) Kama tulivyoeleza katika majibu mama kwamba, ukichukua muda ambao imefanya kazi meli hii sisi tunasema inakwenda kifaida, hatutarajii kwamba gharama zilizotumika zirejee kwa muda mfupi katika kipindi ambacho hakizidi miezi 12, hatuwezi kurejesha gharama kubwa iliyotumika. Lakini matarajio yetu ikiendelea kuwa nzima meli hii, ikiendelea kufanya biashara kama inavyokwenda, gharama hizo zitarudi na itaendelea kuwa inazalisha faida.

(c) Kutokana na matengenezo hayo yaliyofanyika, sisi tunaamini kwamba meli hii itaishi muda mrefu vyenginevyo yatokee mambo mengine ambayo yako kinyume au yako nje ya utaratibu wa mwanadamu katika kuizuia. Lakini kiufundi tunaamini kwamba meli hii imetengenezwa na iko vizuri na itaweza kuishi muda mrefu.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mswada wa Sheria ya Amri ya Barabara (Marekebisho) ya 2013**

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe jana tumemaliziana na Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kuchangia, sasa hivi tunamwita Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kufanya majumuisho. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa mtulie kusikiliza majibu ya Mheshimiwa ili na *quorum* yetu iwe nzuri tuweze kupitisha mswada huu halafu tuendelee na masuala mengine.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho kuhusu Mswada wetu wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Barabara au kwanza ilikuwa ikiitwa Amri ya Barabara. Kwanza napenda nitoe taarifa kwamba Mswada huu utasomwa pamoja na orodha ya marekebisho iliyoletwa. Kwa hivyo, mswada unakwenda sambamba pamoja na orodha ya marekebisho ambayo yameletwa kwenye hadhira hii.

Kwanza napenda nimshukuru Allah (*S.W*) kwa kutupa uhai, uzima na *taufiq* ya kukutana hapa. Pili, napenda nirudie yale maelezo yaliyotolewa mwanzo wakati wa kuwasilisha mswada huu kwamba, sasa hivi tuko zaidi ya miaka 50 tokea mwaka 1964, lakini tuko miaka karibu ya 70 tokea mwaka 1958 ambapo sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya mwisho. Kutokana na ongezeko kubwa la hali ya usafiri, vyombo vya usafiri na mahitaji ya usafiri sheria ile ni dhahiri kwamba ilikuwa haikidhi tena haja ya matumizi. Kwa hivyo, ili kwenda sambamba na hali halisi ya matumizi ya barabara na usafiri kwa ujumla, wizara ilikuwa ni lazima ifanye marekebisho ya sheria ile iliyokuwepo ili kwenda sambamba na hali halisi ya mahitaji yaliopo katika karne hii.

Mhe. Naibu Spika, maeneo muhimu makubwa ambayo yalipitiwa katika kufanyiwa marekebisho ni majina ya utawala, wakati ule mwaka 1958 ilikuwa Zanzibar iko chini ya koloni. Kwa hivyo, wale ambao walikuwa wanapaswa kutekeleza majina yao yalitajwa kwa njia hiyo, lakini sasa hivi kutokana na aina ya utawala iliyopo majina yale hayapo tena, hivyo wale wanaopaswa kutekeleza ile sheria na kuisimamia sio majina yaliyokuwepo. Sasa ilibidi ifanyiwe marekebisho ya kwanza kuondoa majina ya kiutawala.

Lakini pia, kubwa ni upana wa barabara ukimaanisha pamoja na hifadhi yake. Katika kipindi kile tunajua sote idadi ya gari zilizokuwepo na hata huo upana wa gari zenyewe uliokuwepo. Kwa sababu tukitizama gari hizo zilizokuwepo kwa wakati huo zilikuwa na upana mdogo zaidi kuliko zilizopo sasa hivi. Kwa hivyo, hata kama gari mbili zinataka kupishana kwa wakati mmoja mwaka 1958 sasa hivi inapita gari moja tu, wakati mwaka huo gari mbili zilikuwa zikipishana.

Mhe. Naibu Spika, kwa utangulzi huo wa umuhimu wa kurekebisha hayo pamoja na yale ambayo yametajwa hapa na baadhi ya Wajumbe kutokana na adhabu zilizokuwepo thamani ya fedha iliyotajwa kutoka mwaka 1958 hadi hii leo ilikuwa ni ndogo mno ukilinganisha na hali halisi. Kwa hivyo, maeneo matatu hayo makubwa na mengineyo ndio yaliyolazimisha kufanya marekebisho haya ili sheria tuliyonayo iende sambamba na wakati tulionao.

Baada ya hayo naomba sasa niwashukuru sana Wajumbe wote waliochangia tukianza na Mhe. Panya Ali Abdalla, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Yeye alizungumza kwa niaba ya kamati na sitaki niwapongeze kwa kutoa maelezo hapa tu, lakini nataka niipongeze kamati kwa dhati kabisa kwa kazi nzito tulioifanya pamoja nao wakati wa kupitia mswada huu mpaka leo tukaweza kuhudhurisha hapa.

Kwa kweli maelezo mengi ambayo yameelezwa na baadhi ya Wajumbe hususan kwenye misamiati na mambo mengineyo yalisaidiwa sana na michango ya wana kamati ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa. Wizara imeridhika sana na michango yao na ndipo ikapatikana pamoja na ule mswada orodha ya marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, wengine ambao walichangia na napenda nitoe shukurani ni kama hawa wafuatao:-

1. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
2. Mhe. Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Asha Bakari Makame
6. Mhe. Mussa Ali Hassan
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
8. Mhe. Hija Hassan Hija
9. Mhe. Hamza Hassan Juma
10. Mhe. Subeit Khamis Faki
11. Mhe. Salma Mohamed Ali

Mwisho napenda nimshukuru na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kusaidia michango mbali mbali iliyotolewa kutoa baadhi ya ufafanuzi.

Kwa kweli michango ya Wajumbe ilikuwa ni mizuri, safi na inayopelekea mwelekeo. Kuna baadhi ya mambo napenda niyatolee ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, michango yake mingi ilikuwa kwenye misamiati, mfano kutumia neno ‘amri’ kama ilivyotajwa inatumiwa neno ‘sheria’; neno ‘kusababisha’ tayari limeshafanyiwa marekebisho lilionekana; tunabakisha na neno moja ‘hifadhi’ badala ya kutumia ‘hakiba na hifadhi’.

Kutokana na maelezo ya faini limetumika neno lililokuwa haligeuki laki badala ya mia elfu. Kwa sababu hata Mhe. Subeit Khamis Faki, alibabaika kidogo kuona mia elfu, lakini katika sheria hiyo linatumika neno ;laki’ kama ambavyo lilipata ushauri.

Kifungu cha 30(a) marekebisho yenyewe yamefutwa kwa hivyo ndio maana ikawa hicho kifungu hakipo. Kwa hivyo, yale marekebisho yenyewe ya 25 yamefutwa hayapo ndio maana kifungu nambari 33 ikawa hakikutokeza.

Tukija kwenye mchango wake aliosema ama ni uzembe au ni dharau au vipi. Lakini nasema kwamba sheria ya nyuma moja ilisababisha hiyo, kwamba njia zilizotajwa ni nyembamba mno, kama zilivyotajwa futi 23 pamoja na *reserve* yake, kutoka katikati ya barabara mpaka ncha ya barabara. Sasa tuna mita 15 ndio njia kuu na hii mita 15 kama nikimjibu kabisa Mhe. Subeit Khamis Faki, ni kutoka katikati ya barabara mpaka pale inapomalizia hifadhi ya barabara ndio upana huo.

Pia, suala hili kama sio dharau peke yake, lakini ni suala linalowachukua watu wengi wakiwemo mipangomiji, watu wa ardhi, watu wa halmashauri. Kwa hivyo, inategemea na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya wajenzi wa barabara na taasisi nyengine.

Tukija kwenye michango aliyoitoa Mhe. Saleh Nassor Juma, tunampongeza kwa michango yake na sisi tunapokea, masuala yake yalikuwa ni barabara za Vikunguni, Ng'ambwa na Uwandani. Siku tu haijafika, lakini ikifika tayari suala hili litashughulikiwa, namuomba aende kuanzia Ole ajezake kupitia Vitongoji tayari ataziona pegi zimeshawekwa za ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja. Sasa masuala ya muda kufikiwa, lakini barabara hizi hazikudharauliwa, zimo katika mpango lakini kutokana na bajeti ndogo tunakwenda kwa mujibu wa hali inavyokwenda.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe.Waziri, hebu kidogo nitoe taarifa samahani.

Waheshimiwa Wajumbe tumepata wageni leo kutoka Kituo cha Kulelea Watoto Yatima Mazizini. Jumla yao 16 na ni wageni wa Mhe. Mgeni Hassan Juma. Kwa hivyo, wageni wake wasimame tuwaone (*Makofi*).

Ahsanteni sana kaeni kitako.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Kuhusiana na uchimbaji wa kifusi, suala hili naliunganisha pamoja na mchango wa Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Naibu Spika, uchimbaji wa kifusi unafanywa katika maeneo wazi ambayo hayana miti wala majumba. Ila wale watakaonekana wana vipando vidogo vidogo vya muda mdogo vya kama mahindi na mengineyo hulipwa fidia yao, lakini lile ni eneo la wazi ambalo ni mali ya serikali.

Kwa hivyo, hakuna ulipwaji wa fidia kwa kuchukua eneo lile kwa sababu maeneo yale ni ya Makaani na ni ya wazi na yanakuwa hayana miti iliyokuwa imepandwa na watu, isipokuwa ikionekana kuna vipando basi wale wenye vipando hupewa fidia yao kabla ya kuondoshwa.

Suala la uwekaji wa matuta lililoulizwa na Mhe. Hija Hassan Hija na Wajumbe wengi walioulizia. Mhe. Naibu Spika, barabara hujengwa ili wale wanaoutumia barabara wafike yale maeneo wanayokwenda kwa njia nyepesi na kwa muda wanaotaka. Sasa ikiwa kila pahali tutaweka tuta, nadhani itakuwa hakuna anayefika safari yake kwa muda alioupangia.

Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo wizara inatafakari hivi sasa namna gani barabara zetu tutaziweka matuta pale inapohitajika kwa aina zote, lakini matuta haya yanasaidiwa vile vile na utekelezaji wa sheria ya usalama barabarani, vyombo wanaoendesha mbio. Karibuni hivi tulipata taarifa kwamba tuta hilo hilo ndio lililosababisha ajali na gari ikapinduka.

Kwa hivyo, tuta si suluhisho la kuzuia ajali na tuta linaleta tafsiri mbaya ya ile barabara, kwa sababu ikiwa mtu anapanga safari yake kama sisi tuna wasafiri mbali mbali wakiwemo watalii wameshapanga ndege yao saa fulani wanatoka katika hoteli na mgonjwa anawahishwa hospitali, sasa ikiwa njia yetu itajaa matuta kwa kweli itakuwa ni hali ngumu.

Kwa hivyo, sote Waheshimiwa Wajumbe tulifikirieni kwa pamoja hili suala. Je, uwekaji wa matuta ndio suluhisho la kuzuia ajali ili na wananchi wetu waweze kulifahamu badala ya kusema kila pahali tuweke tuta, kwa sababu barabara inapojengwa inamaanisha kurahisisha usafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Lakini pamoja na ujenzi wa barabara unaoweka usafiri uwe mgumu zaidi kuliko kutoka sehemu moja kwenda nyengine inakuwa ni kazi ngumu. Sasa utiaji wa matuta barabarani kwa kweli ni suala la kuzingatia, ni suala la kupewa muda ili wataalamu wetu nao wakaweza kufanya kazi.

Zipo njia tofauti ambazo sasa wizara inazipitia na kuona kwamba baadae ili kuweza kuzitumia. Wenzetu nje wanatumia njia hizo mbali ya kuweka alama lakini kuna vitu vinawekwa barabarani ambavyo vinaweza kuzuia mwenendo wa mbio wa gari bila ya kuipunguzia kasi yake kubwa.

Kuhusu suala la Mhe. Hija Hassan Hija, vile vile aliuliza suala la hifadhi ya barabara. Ndio zipo barabara hizo za mita kumi na tano hivi sasa zenye urefu wa barabara hiyo, na barabara yenyewe ni Tunguu/Makunduchi, Tunguu/Kinyasini, Dunga/Chwaka, Pongwe/Matemwe.

Hizi zote zimefuata ule utaratibu ambao umetajwa katika kifungu Na. 1 cha ugawaji wa nini, sasa na huko tunakokwenda ndio barabara zote ambazo zipo kiwango hicho kilichotajwa katika *category one* zitafanywa hivyo. Hapa nalijibu suala jengine la Mwakilishi mmoja au wawili walioulizia, je yale zile

sehemu zilizokuwa zimeshajengwa zitaingia kwenye mswada huu au sheria hii itakapopitishwa. Ninasema ndio zitaingia.

Hapa itakayotengwa ni Mji Mkongwe tu kwa sababu ni hifadhi maalum lakini maeneo mengine yote yataingia isipokuwa kama nilivyosema kwamba utaratibu utafuatwa wananchi watajuilishwa mapema iwezekanavyo kama hapa itapita barabara, alama zitawekwa na baada ya hapo hakuna mtu atavunjiwa nyumba yake bila ya kulipwa fidia kabla ya barabara kupita. Hilo ndio tunalihakikishia hivyo.

Lakini kila eneo ambalo ule utaratibu wa ugawaji wa barabara upo basi katika ujengaji wa barabara unaokuja utazingatia utaratibu ule ili miji yetu iweze kutanuka na kuweza kupata hali ya usafiri kwa urahisi na wepesi. Kwa sababu barabara inapita gari, inatarajiwa iwe na njia yake, wanapita wenye vyombo vidogo vidogo ikiwemo baiskeli wanatarajiwa kupata nafasi yao lakini pia na watembeaji wa mguu wanatarajiwa wapewe nafasi yao.

Sasa tusiifikirie barabara ni ile gari tu. Sasa kila ikija gari wewe upishe uingie msingini itakuwa taabu sana hiyo. Lazima na wale waendaji wa miguu wawekewe yao, ndio maana barabara zikawekwa kwa njia hizo, zile njia zilizokuwa zina nini. Tatizo kubwa ukosefu wa ardhi na ule utaratibu wa ujenzi uliopita.

Je, sheria hii inazingatia *Zanzibar Transport Master Plan*, ndio. Ujenzi wa barabara unazingatia na ndio maana sasa hivi barabara yoyote inayojengwa inazingatiwa kutokana na *Zanzibar Transport Master Plan*. Tuna ujenzi wa gati unazingatia *Zanzibar Transport Master Plan* na mengineyo.

Hapa Mhe. Hija Hassan Hija, alichangia vile vile kwamba ulipwaji wa fidia, tukimaliza Mhe. Hija tunakuja sasa michango aliyoitoa Mhe. Hamza Hassan Juma. Yeye alitaka kujua kuhusu lile suala la umiliki wa barabara. Sheria za Tawala za Mikoa imezipa Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa kusimamia baadhi ya barabara za mijini na vijijini.

Hata hivyo kutokana na ukosefu na uwezo wa kuzifanyia matengenezo stahiki, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikizifanyia matengenezo pale panapohitajika, lakini mmiliki halisi wa maeneo yale kwa barabara zile ni Manispaa na Halmashauri.

Mfuko wa barabara haukusanyi *road toll* unakusanya hivi sasa ni shilingi mia moja ya *petroleum levy* ipo katika chini ya Wizara ya Fedha, na hii wizara yetu inahusika vipi na Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara upo chini ya Wizara ya Fedha. Mara baada ya kufika kipindi, wizara yetu inakutana na

Mfuko wa Barabara uongozi wake na bodi yake na kukubaliana juu ya utekelezaji wa miradi iliyokubalika.

Kwa hivyo, kunakuwa na mkataba maalum wa utekelezaji ujenzi na matengenezo ya barabara zilizokubalika. Kwa hivyo, ni sawa kwamba Mfuko wa Barabara ni watoaji fedha, Miundombinu na Mawasiliano ni watekelezaji wa kazi za mradi huo. Sisi hatuna fedha za moja kwa moja zinazotolewa na Mfuko wa Barabara bila ya kazi maalum. Kunakuwa na kazi maalum iliyokwishapangwa iliyokwishatiwa thamani, halafu ndio tunasaini mkataba na Mfuko wa Barabara ili kuweza kuitekeleza kazi ile.

Na Mfuko wa Barabara wana bodi yao, wana mkaguzi wao, wana *engineer* wao. Kwa hivyo kazi zilizokwishafanywa zinapitiwa sio tu na wizara yetu lakini wanazipitia wao wenyewe na baadae tunamaliziana. Ikimaliza pale barabara ile ile iliyojengwa ikiwa imejengwa na kampuni kwa upande mmoja au imejengwa kupitia Mfuko wa Barabara, dhamana ya barabara ile sasa ndio chini ya Wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya Idara ya UUB.

Ushauri uliotolewa kuhusu kuweka alama za barabarani. Sisi tumeupokea ushauri huo na bahati nzuri nilipokwenda mimi kwenye matibabu, kabla ya tarehe 4 na 5, nilihudhuria *workshop* ambayo ilizungumza kuhusu *road safety* pale India, yaani usalama wa barabarani.

Wenzetu wana alama tofauti. Unaweza barabarani ukatia rangi, unaweza ukatia *sellotape* ambayo inaganda kwa muda mrefu sana. Kwa hivyo, utaalamu ule, wataalamu wetu wameuchukua na kuona kwamba sasa badala ya kutumia pengine rangi tu na mambo mengine, zipo njia chungu nzima za kutumia *sellotape* na vitu vyengine ambavyo si rahisi sana kuondoka pale barabarani. Kwa hivyo, utaalamu ule tumeuchukua na tunautizama uwezekano wake wa kuutekeleza hapa kwa mujibu wa fedha ambazo tutapata.

Lakini karibuni hivi yameonekana maeneo matano ya kuwekwa taa za barabarani zile za kuongozea gari, yaani *stop light*, ni moja katika alama muhimu sana za barabara za kuweka gari kuongozwa. Kwa hivyo, kupitia Mfuko wa Barabara na wizara yetu mambo haya yanatekelezwa.Wizara inathamini sana kuwepo kwa alama za barabarani kwa sababu ndio vitu muhimu vya kuwaongozea, lakini tujue kwamba baadhi ya alama zinachomolewa na watu wetu. Kwa hivyo, sisi kama ni Wawakilishi tunapaswa kuwaelimisha wizara yetu pamoja na nyinyi, kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuzibakisha alama za barabarani.

Mwananchi ajue kwamba akiitoa alama ya barabarani, eneo lile likipata ajali kwa sababu ya kutolewa alama ile, anapewa adhabu ya Mwenyezi Mungu kuanzia siku aliyoitoa mpaka atakapofufuliwa na huko mbele ya safari. Kwa hivyo, alama ya barabarani ni kitu ambacho kinamzuia dereva kufanya vile anavyotaka yeye na kufuata ule utaratibu. Kuna alama za kuwa kuna kona, kuna alama za kuwa kuna njia zinapishana.

Sasa wananchi wajue kwamba wakichomoa alama hizo basi wanajitafutia mashaka ya hapa duniani na kesho akhera. Kwa sababu kila *accident* itakayotokea kwa ajili ya kuichomoa alama ile na yeye anaingizwa, anaandikiwa lake, kapu anajaziwa tu. Sasa atajiona anafanya mazuri lakini kumbe ile alama imeshamuingia pabaya.

Suala la fidia kweli kuna kipindi kulikuwa hakuna uwazi, lakini ninawahakikishia Mhe. Naibu Spika, wewe mwenyewe na Baraza lako tukufu na Mhe. Mwakilishi Hamza Hassan Juma, kwamba sasa hivi wizara imetengeneza *invoice* maalum zenye kopi tatu ambazo mwenye kutaka kupewa fidia kwa ajili ya kuondoshewa nyumba yake au miti yake anajazishwa, anapewa mwenyewe kiwango cha thamani yake mpaka siku ya kulipwa, ndio analipwa fedha zake.

Na hata sasa tunadiriki kupiga mpaka picha mbele ya nyumba yake ili asije akaseme nyumba yake ilikuwa ni ya ghorofa wakati ilikuwa ni ya chini. Kwa hivyo, hatua zote hizo tunachukua ili kupata ule uwazi. Tatizo kubwa liliopo katika ulipaji wa fidia ni gharama za ulipaji wa fidia. Kwa hivyo, tunaomba sana kwamba bajeti yetu ambayo huwa munakataa kuipitisha, lakini muna watu wanazingoja fedha zile za kulipwa fidia. Kwa hivyo, zitakapokuja bajeti zetu muzipitishe kiwepesi ili wale wananchi wakalipwe fidia.

Kama nilivyosema katika suala la Mhe. Hija Hassan Hija, kwa sababu barabara zenye ukubwa ule uliotajwa zipo na zinafanya kazi na zinaendelea vizuri, hakuna haja basi ya kupunguza ukubwa wa uhifadhi wa barabara kwa sababu tayari ishaonekana na yale maeneo ambayo hayakuwahiwa, kila tukienda mbele serikali ikiwa na uwezo itawalipa fidia wanaohusika na barabara zitakuwa nzuri kwa sababu kitu cha mwanzo kinachozungumzwa hapa ni hali ya usafiri na urahisi wa utoaji wa gari katika maeneo. Wenzetu wanajenga *fly over* wanajenga *under ground*. Sasa sisi itakuwa ni suala gumu la kuzitanua tu barabara za kuweza kupitisha magari yetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, yeye alitaka kujua juu ya usimamizi wa sheria hii. Kama nilivyosema mwanzo usimamizi wa sheria ni muhimu kweli, lakini ni suala mtambuka, kila mmoja analo. Tukiwa sote tutashirikiana katika

kuona kwamba sheria hii inatekelezwa bila ya vipingamizi basi tutaweza kwenda.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alitaka kujua kuna jengo na nyumba. Ilivyotafsiriwa katika sheria hii ni jengo na sio nyumba. Kwa hivyo, *foundation* ni jengo, *foundation* ya ukuta ni jengo, ukuta wenyewe ni jengo na kadha wa kadha. Kwa hivyo, kilichotafsiriwa ni jengo na sio nyumba. Kwa hivyo, nilikuwa ninamtanabahisha tu basi.

Umiliki wa maeneo yaliyochimbwa kifusi, nilikwishakulijibu hili kwamba umiliki ni wa serikali, kwa sababu ni maeneo ya wazi ila wale ambao walikuwa na vipando vyao wangestahiki kulipwa fidia kabla ya kuondoshwa.

Mhe. Asha Bakari Makame, tunamshukuru kwa mchango wake, ni sahihi kwamba lazima sote tuwe na *vision* tujue tunakoelekea, hilo ni suala muhimu sana, isiwe tunakwenda tu, tuwe na *vision*. Na kwa sababu hiyo, ndio maana wizara ikaona sheria ya mwaka 1958 haiwezi ikatufikisha pahali.

Suala la raia kujiwekea matuta kiholela. Limetajwa katika sheria hii na adhabu yake. Kwa hivyo, sasa hivi ni utekelezaji tu, kwa sababu wapo binadamu wengine ndio kama nilivyosema huamka usiku wakatia zege katika barabara bila ya kujua athari yake. Wananchi wanapaswa kuelimishwa kuhusu taathira hiyo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad, kwanza ninapenda vile kama alivyosema, niombe radhi kwamba kweli tulikuwa na kasoro kidogo katika kuhudhurisha ile bango kitita ya sheria iliyopita na hii. Kwa hivyo, kwa mara hii tuchukulie upungufu huo kutokana na mambo kadha wa kadha ikiwemo muda na mambo mengine ambayo yalihusiana na marekebisho.

Kwa sababu sheria si ya wizara tu, ikifika katika kiwango hiki ina vyombo vitatu; sisi wizara, tuna kamati na kuna Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa lazima huwezi kutoa *document* ambapo hajakwenda katika ngazi hizo. Kwa hivyo, kutokana na muda uliokuwepo tunaomba radhi sana kweli, lakini nadhani tutakubaliwa radhi yetu. Ni binadamu ni hali ilivyo.

Suala la uharibifu wa mazingira kwa binadamu njia za Konde, Gando zinaeleweka, ni kweli watu wanaathirika sana, na serikali kupitia wizara hii kwa kweli inakwenda kasi mno kulishughulikia suala la njia za Wete/Konde na Wete/Gando. Lakini hali sijui imekuwa vipi.

Mimi binafsi siridhiki na hali halisi lakini ndivyo hali ilivyo, mpaka juzi kuamkia jana nilipita njia ya Konde nikaiona hali ilivyo, tunarudi nyuma

lakini wizara itachukua kila juhudi ili kuona mapema iwezekanavyo, ile njia imefikia pahali karibu pa kutiwa lami tu lakini kuna mambo chungu nzima kwa sababu...

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa munaotoka tunataka tupitishe vifungu sasa hivi. (*Makofi*).

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, kuna wajenzi na kuna watoaji fedha. Hii njia ina watoaji fedha watatu. Kuna *BADEA, Saud Fund* na serikali. Sasa wote hawa wanatarajia kila mara waweze kulingana katika mambo yao; mmoja tu akichelewa yule mwengine mradi wote unachelewa.

Kwa hivyo, tunaomba uvumilivu wananchi wote wa Jimbo kuanzia Wete mpaka Konde tunawaomba radhi sana, Wete/Gando tunawaomba radhi sana, lakini wizara inajitahidi sana kuweza kufuatilia ili kufanikisha. Mwakilishi wao yupo hapa Mhe. Suleiman Hemed Khamis, analifuatilia sana hili suala ninajua na ninawaarifu Waheshimiwa huko kwamba Mhe. Mwakilishi pamoja na uwaziri wake, kila baada ya siku mbili ananipigia simu. Kwa hivyo, tukiona vile vile ananikumbusha lakini hali halisi ndio hiyo, hatupendi kuweka hivyo, lakini ndio hali iliyotokezea.

Suala la kuharibu njia nyengine, hili suala huwa linafuatiliwa na wizara na mara nyingi njia zinazoharibiwa hufanywa mazungumzo baina ya wizara na wale wakandarasi kwa kupitia viongozi wao waliopo; na hufanya matengenezo ama hutoa fedha za matengenezo au hufanya matengenezo wao wenyewe katika maeneo waliyoyaharibu.

Sasa huu ukubwa wa magari uliozungumzwa, huu tutaufanyia kazi kuona kwamba, je, gari zetu zilizojengwa haziwezi kuchukua ukubwa wa magari yale, kwa sababu sasa hivi kuna makontena yanapita. Kwa hivyo, sio magari yale tu ya peke yake ya mzigo, lakini kuna makontena yanapita katika njia zetu, yote haya yatafanyiwa kazi ili kujua.

Kuna chombo kimoja ambacho sasa hivi tunapigania kipatikane baina ya wizara tatu, kuna *weighing machine*, kuna mashine zile za kupimia gari kwenye barabara. Sasa hatuwezi sisi kuli-*charge* gari ikiwa hatuna ushahidi kwamba uzito wake ni kiasi fulani.

Sasa naomba sana tutashirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Biashara na Masoko ili chombo hiki kiweze kupatikana, kwa sababu sisi tunakihitaji kwa upande mmoja, Wizara ya Biashara wanakihitaji na Wizara ya Fedha wanakihitaji kwa ajili ya *taxation*. Kwa hivyo, ni suala muhimu ili kuweza

kujua hasa uzito wa magari yanayopita tuweze kuwa na *weighing machine* ambayo inawekwa juu ya barabara.

Mhe. Salma Mohamed Ali, mitaro ndio neno sahihi kama nilivyosema kwamba hii kazi ilifanywa na Kamati na yeye ndiye lakini alikimbia siku hiyo. Kwa hivyo, ilifanywa na imeshasahihishwa na hiyo kamati yako ambayo ni kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi. Ilifanya kazi kubwa, hatukunywa chai ya asubuhi wala chakula cha mchana siku ile, tulipiga kazi mpaka kazi ikamaliza.

Vifungu vya adhabu kwa sababu kanuni anatunga Waziri, vifungu vya adhabu katika sheria zote huwa vinawekwa kabisa katika sheria. Kwa sababu kwenye Mahakama inayochukuliwa ni sheria na sio kanuni, Kanuni zinatumika huku ofisini kuweza kutoa adhabu ndogo ndogo.

Ninakubali kwamba sheria hii pamoja na uwekaji matuta zinahitaji elimu. Hii sheria yenyewe inahitaji tutoe elimu ya kutosha, hilo ninalikubali na ushauri huo tumeuchukua na tunavyo vipindi hivyo na vimeshaanza katika redio; kutoa taaluma kuhusu sheria hii na tunaendelea kutoa taaluma. Kama nilivyosema kwamba sote tufahamu nini taathira ya sheria hii ya kutanua barabara ili usafiri wetu uende, tupunguze ajali, twende katika hali ya usalama barabarani na pia tuweze kufika kwa wakati kule tunakokwenda.

Suala la kuruhusu tumeshasema kwamba ukiachia Mji Mkongwe ambao umo katika hifadhi ya ulimwengu; maeneo yote mengine yaliyo katika visiwa vya Unguja na Pemba yataingia katika sheria hii kwa ajili ya utanuzi wa barabara. Ila nasisitiza tena kutoa kwamba wananchi wataarifiwa kabla, taarifa itatolewa, vipimo vitawekwa na kila atakayehusika kwa kuvunjiwa nyumba basi atalipwa kabla ya kupita barabara ile. Katu haitovunjwa nyumba ya mtu tukijaaliwa bila ya kulipwa fidia.

Suala lililozungumzwa sana kuhusu utaratibu wa vituo vipya vya daladala. Wawakilishi watu; Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma na Jaku Hashim Ayoub na walilizungumza kwa hamasa kubwa. Mimi ninakubaliana na hamasa zenu, lakini mungesoma kwanza nani muhusika katika ubadilishaji wa vituo vile, angalau mungeuliza basi. Kwa sababu vituo vile uendeshaji wake upo chini ya Manispaa na sio Idara ya Usafiri na Leseni au Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika daladala:-

1. Kutoa leseni kwa madereva na makondakta,

2. Kutoa ruhusa ya njia (*route)*,

3. Kutoa leseni kwa gari yenyewe baada ya kuipasisha kutokana na uzima wake ile gari.

Hizo ndizo kazi zetu. Kazi za kupanga vituo gari hizi zikae wapi ni kazi ya Manispaa na maeneo mengine ya Mjini/Magharibi itakuwa ni kazi za Halmashauri. Sasa kabla ya kuja kutoa lile dukuduku lako ungeuliza ni nani anayehusika. Ila kwa sababu Manispaa ipo chini ya Wizara na mimi ni Waziri katika Serikali hii hii, mimi ninalichukua kama ni *concern* iliyotoka katika Baraza tutawapelekea wenyewe na ninafikiri kama jana Mhe. Spika nilimfahamu alizungumza akasema kwamba *message sent* au *received*. Kwa hivyo, mliopeleka *message* imefika, lakini wizara yetu sio inayohusika na kupanga utaratibu wa vituo vya kufikia gari za shamba na daladala. Lipelekeni linakohusika na sisi vile vile tutawasaidia kulipeleka, kama ndio wananchi wana- *concern* hiyo, pia na sisi tutalipeleka, kwa sababu sote tuko hapa kuwahudumia wananchi wetu, ama ni shughuli hii au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya mwisho kuna suala moja alilozungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu suala la uwezo wa kuwafidia watu wote waliojenga ndani ya hifadhi ya barabara. Nilisema kwamba haya mambo yatakwenda kwa awamu. Kila barabara iliyotajwa isiyokuwa ya Mji Mkongwe basi imo katika utaratibu huu wa hifadhi, lakini namna ya uondoshaji wa majumba na ujenzi wa hizo barabara utakwenda kwa hatua ambazo serikali ina uwezo wake.

Kwa hivyo, sio kwamba ikishapitishwa sheria hii siku ya pili nyumba zote tena zitavunjwa kwa kuwekwa hifadhi ya barabara, laa, hilo halitatokea. Itakuja kwa awamu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kuwaachia wanyama katika barabara. Kwanza katika neno tafsiri wanyama limetajwa wanaofugwa. Kwa sababu wanatajwa wanaofugwa ni kuingiza wale wanyama wa kawaida wanaofugwa kikawaida na dhamana ni ya yule mtu anayefuga na kuingiza wanyama wengine ambao kikawaida sio wanyama wa kufugwa, lakini mtu mwenyewe kaamua kuwafuga. Kwa hivyo, na yeye pia akimuachia kuingia barabarani na yeye ataingia kwenye hatia.

Mimi nililokuwa sikubaliani nalo na ninamuunga mkono Mhe. Jaku Hashim Ayoub sana kabisa, ni kuwafanyia vibaya au ukatili wale wanyama, kwa sababu mnyama siye aliyekosa. Sasa kama kuna watu wanawafanyia ukatili wanyama baada ya kuwakuta barabarani, hao kwa kweli ni wa kushughulikiwa. Kwa sababu imekatazwa kwamba ng'ombe haruhusiwi

kutembea njiani, halafu wale wanaomkamata wakamfanyia ukatili yule ng'ombe. Ng'ombe siye aliyevuka sheria, aliyevuka sheria ni yule mwenye ng'ombe aliyemuachia na kumfanyia ukatili mtu au mnyama yote hayakubaliki. Kwa hivyo, hapo naungana mkono na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kusema kwamba sote tujue kuwa hata wale watakaowakamata basi wawakamate katika hali ya kiutaratibu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, napenda tena nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, Wajumbe wote waliochangia mswada huu na ninawaomba sana sote kwa pamoja tuupitishe, ili tuweze sasa kuendelea na kazi kama ambavyo zimetukabili. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wote waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

### Mswada wa Sheria ya Amri ya Barabara (Marekebisho) 2013

### Sehemu ya Kwanza

### Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Tarehe ya

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake alioutoa katika masuala mbali mbali. Lakini vile vile, katika ushauri mbali mbali ambao tulioutoa inaonesha kwamba yeye pamoja na watendaji wake mengi wameyazingatia. Isipokuwa kuna suala moja niliuliza katika hii tafsiri. Imeeleza kwamba sheria hii inaweza kuitwa

kama amri ya barabara na marekebisho yake ya mwaka 2013, na itatumika mara tu baada ya Mhe. Rais atakaposaini.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwenye hiki kifungu cha 1(2) ndio nilichokuwa naulizia.

Kifungu cha 1(2):

> "Sheria hii itasomwa pamoja na Amri ya Barabara Sura ya 134 ambayo katika sheria hii itarejewa kama sheria mama"

Sasa hapa mimi nilitaka kujua miswada mingi tunayoletewa hapa inakuwa inarekebisha sheria, labda sheria nambari 8 ya mwaka fulani. Sasa hapa Mhe. Waziri, tulimsikia akisema marekebisho haya tunayafanya kwa sheria ya mwaka 1958, lakini hatujui sheria hii ilikuwa nambari ngapi. Ndio nikauliza au zamani baada ya kuitwa sheria nambari ngapi ndio ilikuwa inaitwa hii sura mfano 134. Kwa hivyo, hapa ndio kidogo nilikuwa nataka maelezo. Labda hii miswada ya zamani ilipokuwa inakwenda inaitwa sura nambari fulani, kwa sababu siku hizi tumebadilisha utaratibu, tunasema sheria nambari 8 au sheria nambari 10 ya mwaka fulani. Kwa hivyo, hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi wa kisheria ili angalau tunapofanya marekebisho haya tujue kuwa hii sura ndio zamani hiyo sheria ilikuwa inaitwa sura au vipi, labda Kiswahili tu kimebadilika. Nilikuwa naomba maelezo.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na lile alilioliona Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba hii sheria ya zamani inaitwa sura, haina namba au namba yake ni hii sura na wakati sasa hivi tunatumia utaratibu wa kukipa namba.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lakini hilo sio kosa ni kwa sababu ya utaratibu ambao ulikuwa ukitumika. Kwa zamani na mpaka sasa hivi, pengine tutakuja kugundua huko mbele hata hizi sheria tunazozipitisha zitakuja kupata jina la sura. Kwa sababu kuna utaratibu wa kwamba wenzetu walitunga sheria kwa mfano mwaka 1921 wakaanza kufanya kitu tunaita *consolidation* au *revised edition*, kufanya mapitio ya zile sheria wakaziweka pamoja na vinapotoka vile vitabu kwa pamoja vinapewa majina ya sura, utaratibu huo ulianza mwaka 1921.

Mwaka 1934 yakafanyika mapitio mengine makubwa ya sheria za Zanzibar na ukaja utaratibu huo huo. Utazikuta sheria zilizokuwa na namba za sura mwaka 1921 halafu mwaka 1934 zikapewa namba nyengine za sura. Lakini marekebisho au mapitio makubwa mengine yalifanyika mwaka 1958 na hapo ndipo hizi sheria zikapata hayo majina ya sura. Kwa bahati mbaya toka

mwaka 1958 mpaka sasa hivi hatujafanya tena mapitio makubwa ya sheria na tukaziweka pamoja.

Hii ni kazi ambayo sasa hivi ofisi yangu inaendelea nayo kutayarisha mapitio makubwa ya sheria. Tulisema katika *budget speech* yetu ili tuje tuwe na mkusanyiko wa sheria za pamoja za Zanzibar na ambazo pia zitakuja kupewa majina ya sura na zile namba zitapotea.

Kwa hivyo, kwa sasa hivi tutaendelea kutumia sura kwa zile sheria za zamani na hizi sheria ambazo zimekuja baadae kuanzia mwaka 1959 zote zinatumia namba mpaka sasa hivi.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mhe. Mwanasheria Mkuu nadhani iko haja sasa ofisi yako utufanyie semina, na utufanyie semina kwanza ya kutufanya sisi Waheshimiwa tusome sana, kama unavyosoma wewe. Kwa sababu unavyonukuu hizi sheria za mwaka fulani na mwaka fulani, sasa angalau maana yake ili vinapokuja vitu kama hivi visituchanganye sana. Kwa sababu unajua Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kutunga sheria sio kazi ambayo tumeianza sisi. Kazi hii waliianza wenzetu mababu zetu na mababu zetu na sisi tumerithi.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa hii tu kwa faida ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Hii ilikuwa ni pongezi zake maalum kwamba ni mtu ambaye muda mrefu anayapitia haya makabrasha na anapitia sheria na ndio maana ananukuu sheria za miaka mingi iliyopita, kama anavyofanya mzee wetu Mhe. Ali Mzee Ali. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 1 | Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake. |

**Sehemu ya Pili**

**Marekebisho ya Vifungu Mbali Mbali**

| | |
|---|---|
| Kifungu 2 | Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 3 | Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 4 | Kufuta Kifungu cha 4 |

| | |
|---|---|
| Kifungu 5 | Kufuta Kifungu cha 5 |
| Kifungu 6 | Marekebisho ya Kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 7 | Marekebisho ya Kifungu cha 7 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 8 | Marekebisho ya Kifungu cha 8 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 9 | Kuongeza Kifungu kipya |

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia jana nilisema barabara sasa hivi zimekuwa na msongamano mkubwa na kuhatarisha usalama, na hii barabara nafikiri iko dhamana chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Sijui Mhe. Waziri, anatueleza nini msongamano umekuwa mkubwa kuhusu utumiaji wa barabara hasa eneo la Kisiwandui na usalama umekuwa mdogo wa eneo lile.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sehemu gani.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kifungu 9 barabara za mjini (c)

**Mhe. Mwenyekiti:** Msongamano sehemu gani.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kutoka barabara ya Mkunazini kuelekea mpaka *round about* Michenzani. Msongamano umekuwa mkubwa wa barabara ile.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mwakilishi. Nimezungumza mambo matatu mimi ambayo yote yatapunguza msongamano; kwanza ni kupitishwa kwa hii sheria kwa sababu hii sheria inaweka uhalali wa kupanua hizo barabara ambazo ziliopo sasa hivi. Hilo la mwanzo.

Lakini la pili, nilisema katika kushughulikia wizara wenyewe tayari kwa kupitia mfuko wa barabara imeshaweka maeneo matano ya eneo hili la kuweka taa za barabarani yaani *stop light*. Sasa pale panakuwa na msongamano kwa sababu sasa hivi hapana *stop light* ambayo ingeongoza zile gari kuweza kwenda na nyengine zikasimama.

Kwa hivyo, kama hakuna *stop light* ina maana kila mmoja anakwenda anarudi na kupinda pale. Kama nalifahamu eneo la Mkunazini ndio hilo lenye msongamano, kwa sababu kuna njia nne. Kuna njia inayotoka Haile Selassie kuelekea sokoni, inayotoka Michenzani kuelekea Mkunazini. Sasa hapo palikuwa na *stop light*, lakini sasa hivi hapana. Tayari Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeshatoa zabuni ya kuwekwa hizo taa za *stop light*, moja katika maeneo ni hapo. Kwa hivyo, yeye kasema wizara yetu, sasa wizara yetu ndio inajitihada hiyo. Ahsante.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nafikiri Mhe. Waziri, hakunielewa. Nasema katika Ofisi ya Chama cha Mapinduzi Kisiwandui, chama kikubwa katika vyama vyote Tanzania. Msongamano umekuwa mkubwa pale katika ofisi na viongozi wetu wanapata shida kuingia ndani mpaka *round about.*

**Mhe. Mwenyekiti:** Unajua Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri, alieleza labda mmekosana kidogo. Alikuambia Manispaa ndio inayohusika na walioweka vituo vile, wao kazi yao ni kutengeneza njia na kwa kuondosha msongamano, wakaona wakiweka *stop light* utaondoka ule msongamano. Lakini sasa Manispaa wao kama pale pana msongamano hata kwenye vituo vyengine waweke, kwa sababu vituo vyote sasa hivi ni vurugu.

Kwa hivyo, ni Manispaa na wamesena watalichukua na watawaeleza watu wa Manispaa ili waweze kufanya utaratibu ule msongamano uondoke, pale wamefanya kituo ndio ukasababisha msongamano. Kuanzia CCM mpaka jumba la mwanzo la Michenzani ni watu wa Manispaa wahusika na wameshasema watazungumza nao.

Suala la njia kajibu vizuri tu, ataweka *stop light* ili watu waweze kwenda na kurudi. Una hoja nyengine.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, katika hoja ambayo niliizungumza juzi, nilizungumzia kwenye kifungu cha 9(8)(a) aina za barabara. Mimi nilijaribu kumuuliza Mhe. Waziri, katika hizi *category* tano alizoweka za barabara. Kuna barabara kuu, barabara za vijijini, barabara za mjini, barabara za kulishiza na barabara nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilipongeza sana kwamba serikali yetu kwa kupitia Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano imeanza kuona ni namna gani huko tunakokwenda barabara zigaiwe katika *category* fulani. Hoja yangu ilikuwa kwamba mara nyingi tunapokuwa tunauliza maswali hapa, kuhusu suala la huduma za barabara hasa hizi barabara ndogo ndogo ambazo maarufu

tunaita *feeder roads*. Mhe. Waziri, mara nyingi anatuambia kwamba barabara hizi zinatakiwa zishughulikiwe na Halmashauri au Manispaa, lakini tunavyojua katika nchi za wenzetu kwamba zile serikali za majimbo zina nguvu sana na zimepewa mamlaka kubwa na mpaka bajeti zinatengewa kwa ajili ya kushughulikia miundombinu iliyokuwa katika maeneo yao.

Kwa mfano wenzetu Tanzania Bara, utaratibu wao katika halmashauri ni kwamba kila mwaka kuna fungu linalokwenda kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara na mambo mengine. Lakini hapa kwetu Mhe. Mwenyekiti, halmashauri na manispaa zinajitegemea wao wenyewe moja kwa moja kwa kupitia vianzio vyao.

Lakini hata hivyo vianzio katika halmashauri mfano, katika maeneo ya Mkoa wa Kusini au Mkoa wa Kaskazini, kuna mahoteli mengi ya kitalii, lakini fedha zile zinakusanywa na serikali kuu. Kwa hivyo, zile halmashauri zinakuwa hazina *fund* za kuweza kufanya ule ukarabati. Kwa kuwa fedha hizi zinakwenda katika mfuko mkuu wa serikali, vile vile serikali kwa kupitia hii *road fund*, fedha hizi zinakwenda katika mfuko wa barabara.

Kwa hivyo, halmashauri hawana nafasi yoyote ya kuweza kuomba fedha katika mfuko wa barabara, isipokuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, wao ndio wanaomba fedha kutoka katika mfuko wa barabara kwa ajili ya ukarabati.

Sasa ndio nilikuwa nauliza katika *category* hizi. Je, bado kuna barabara ambazo zitakuwa zinaendelea kushughulikiwa na halmashauri na manispaa. Na kama zitakuwepo *fund* za kufanya matengenezo madogo madogo ya barabara hizi, wao watakuwa na uwezo gani wa kuweza kuzipata fedha hizi. Nilikuwa kidogo nataka ufafanuzi katika hizi *category* za hizi barabara 5. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nimesikia mawazo ya Mhe. Mjumbe, lakini naomba nimpe maelezo yafuatayo. Kile kifungu kwanza nimetaja kuhusu aina tu za barabara, kwamba barabara zenye ukubwa ule zitakuwa ni zile zilizotajwa pale kwenye vifungu vitano. Nani anayepaswa kutengeneza, ni sheria mbali mbali zilizopo zinazowapa uwezo wa kutengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu nililomjibu nilisema hasa sheria ya tawala za mikoa imezipa Halmashauri za Wilaya na mabaraza ya miji kusimamia baadhi ya barabara za miji na vijijini. Kwa hivyo, baadhi ya barabara zilizomo zinasimamiwa hivyo, hilo liko wazi, sheria ndio iliyosimamia.

Lakini maelezo yanaendelea, kutokana na ukosefu wa uwezo ambao yeye ndiyo anayozungumza sasa hivi, wa kufanyia matengenezo stahiki Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikizifanyia matengenezo pale panapohitajika. Ni wakati ule Mhe. Hamza Hassan Juma ulipoondoka, na ulipokuja ninajibu suala jengine.

Kwa hivyo, suala hili nililijibu, na ndio maana mfuko wa barabara hauko chini yetu, sisi tunapokwenda tunakwenda na *plan of action*. Hii ndio *plan of action* yetu na haya ndio makisio. Kwa hivyo, mfuko wa barabara tunaingia nao mkataba, na mfuko wa barabara unaweza ukatoa msaada kwa taasisi yoyote katika ujenzi wa barabara, isipokuwa hapa kutokana na udogo wa pahala tunaingia napo mkataba wa ujenzi wa barabara zile zinazohusika.

Sasa kama halmashauri inahitaji barabara zake, moja kwa moja iende kunakohusika, sisi tutakabidhiwa ile kazi tu, hata kama sisi hatukupeleka programu ya barabara ile, wakishakubali mfuko wa barabara watatukabidhi ile kazi tuifanye. Tunachokabidhiwa sisi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutoka mfuko wa barabara ni kazi ya kuifanya kwa pesa zile. Wao wana *auditor* wao, wana *inspector* wao na wana *engineer* wao, sisi tunaifanya wanakuja kuitizama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ushahidi kamili kuna zilizotengenezwa za mjini, vijijini na za mashamba. Juzi tulikwenda kuzindua daraja lililounganisha Msitu wa Ngezi na kijiji kilichokuwa huko mbali hata huwaoni ukipita huko nje, wamegharamia mfuko wa barabara. Kwa hivyo, sio kwamba hizi shughuli hazifanywi, zinafanywa, lakini pengine hiyo tu haijafanywa. Nawaambia utaratibu hata wao wanaweza kuzungumza na mfuko wa barabara watatukabidhi sisi kazi tu. Tunachoingia mkataba na mfuko wa barabara ni kufanya kazi, sisi kama ni *Government Company* inayoingia mkataba na mfuko wa barabara, hilo ndio jibu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri na hapa hoja yangu nataka vile vile na sisi tumsaidie kazi ili kila siku tusimuulize maswali ambayo anasema yako nje ya wizara yangu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mfuko wa barabara. Kwanza tunawashukuru sana fedha zetu wanazikusanya vizuri na wanazihifadhi vizuri. Hivi karibuni tulipofanya vikao na mfuko wa barabara wakasema wanazo fedha nyingi, lakini tatizo hii idara ya utunzaji na ujenzi wa barabara wamekuwa na uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi.

Sasa kwa kuwa amesema Mhe. Waziri, kwamba halmashauri zina uwezo wa moja kwa moja kwenda kuomba fedha kutoka katika mfuko wa barabara, na

sasa hivi tunashukuru hata Wizara yenyewe ya Miundombinu na Mawasiliano, wamejaribu kuanza kutoa kazi kwa kampuni nyengine ukiacha hao Idara ya Utunzaji na Ujenzi wa Barabara.

Je, halmashauri kama mfano wanaona kuna barabara zao za ndani wanataka kuzitengeneza na vile vile wao halmashauri baada ya kwenda mfuko wa barabara, watakuwa na uwezo wao wenyewe halmashauri kutoa *tender* kwa ajili ya kutafuta *private company* kwa ajili ya kutengeneza barabara zile au lazima itabidi zirudi miundombinu, halafu wao Idara ya Utunzaji na Ujenzi wa Barabara ndio watoe *tender* kwa kampuni nyengine, kwa ajili ya kukarabati hizo barabara za ndani, hilo lilikuwa ni suali la ziada.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu. Lakini alipokuwa hakunipata ni pale aliposema kwamba sisi tunapewa kazi tu na mfuko wa barabara. Kwa hivyo, hayo maelezo yote aende kule mfuko wa barabara wao ndio wanaotoa *tender*. Sisi hata *tender* hatutoi, sisi tunapewa ile kazi tu. Kwa hivyo, kama tunaifanya sisi ile kazi basi ile *tender* ndio tunaichukua sisi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Kwa hivyo, ukienda mfuko wa barabara utaelezwa yote na masharti yao ili kupata *fund* ni mfuko wa barabara, suala la kufanyiwa kazi kwa sasa ni sisi. Suala hili nilitaka aweze kupambanua. Kwa sababu wao Waheshimiwa Wawakilishi walipewa semina na mfuko wa barabara ina maana waliitwa, mtu akikukaribisha njoo nyumbani kwangu ule chakula cha mchana, ina maana anakukaribisha kwa mambo mengineyo kama ukiwa na shida uende.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri umefahamika. Mhe. Hamza Hassan Juma, tumalizie hii, nadhani umemuelewa Mhe. Waziri, kwamba mambo yote yako kwenye mfuko wa barabara. Kama una makisio yako, una barabara yako, kama halmashauri, kama manispaa.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemuelewa sana Mhe. Waziri. Unajua sisi kazi yetu Wawakilishi haya masuali tunayouliza, haya ni masuali ambayo tunapewa na wananchi wetu na haya masuali vile vile yatawasaidia makatibu wa halmashauri na wakurugenzi wa mabaraza ya miji, kwamba sasa hivi wao moja kwa moja wanapokuwa na zile barabara za ndani wasihangaike waende mfuko wa barabara, wapeleke maombi yao. Kwa hivyo, mfuko wa barabara watashirikiana nao kwa ajili ya kutoa *tender* kwa ajili ya kutengeneza barabara za ndani. Sasa hilo suali nimeliuliza mimi, lakini najua faida watapata watu wengi katika utekelezaji. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

| | |
|---|---|
| Kifungu 9 | Kuongeza Kifungu kipya cha 8A |
| Kifungu 10 | Kufutwa kwa Kifungu cha 9 |
| Kifungu 11 | Marekebisho ya Kifungu cha 10 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 12 | Marekebisho ya Kifungu cha 11 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 13 | Kuongeza Kifungu kipya cha 11A pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 14 | Marekebisho ya Kifungu cha 15 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 15 | Marekebisho ya Kifungu cha 19 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 16 | Kufuta Kifungu cha 20 na Kukiandika upya pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 17 | Marekebisho ya Kifungu cha 21 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 18 | Kuongeza |

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, naendelea tena kukushukuru kwa kunipa nafasi nikaweza kupata ufafanuzi wa ziada.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kifungu cha 18 kifungu kipya cha 23A (2) kinachozungumzia kwamba

Kifungu cha 23A (2):

> "Isipokuwa pale ambapo mali binafsi imehifadhiwa kwa matumizi ya Idara, masafa ya hifadhi ya barabara kutoka katika barabara kwa ajili ya kila aina ya barabara kwa pande zote mbili za barabara yatakuwa, yaani masafa walivyokusudia hapa kwamba mita 15 kwa barabara kuu, mita 12 kwa barabara zinazoungana na barabara kuu, mita 10 kwa barabara za wilaya na kwa barabara nyengine kama itakavyowekwa na Idara"

Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, niliuliza maswali, lakini kidogo Mhe. Waziri pengine alipoyatolea ufafanuzi sikusikia vizuri, hivyo nikipata maelezo ya ziada nitaweza kuridhika. Kuna hizi barabara ambazo zinaendea vijijini, zinatoka nje ya mji barabara kuu. Zile kwa sasa hivi tunaamini hizi mita 15 zitapatikana hazina matatizo, na hata hizi barabara zinazoungana na barabara kuu mita 12 zinaweza zikapatikana.

Lakini nakusudia hizi barabara za zamani hasa zilizokuwepo katika miji. Sheria hii tukiipitisha serikali imeshakubali kupitia Wizara ya Miundombinu kwamba wananchi wataweza kulipwa fidia kwa thamani ya hali halisi ilivyo hivi sasa. Ndio nikajaribu kuuliza mfano kuna barabara hii ambayo inatoka kwa Bi Ziredi, inakuja mpaka kwendea Fuoni. Barabara hii ukiangalia pembeni mle kuna nyumba au vile viduka duka vimewekwa nambari kwa maandishi mekundu. Nimuulize Mhe. Waziri, je, nambari zile ni kwamba zile nyumba zitabomolewa au vipi.

Chengine ni kitu ambacho bado wizara hii tunaiomba sana kwamba katika hizi barabara hata wakitia zile alama kama hawajaweka zile *bicorn* basi bado tatizo litaendelea kuwa la kwao na hasara itaendelea kupata serikali. Sasa hilo la *bicorn* najua wao wenyewe watajiandaa. Zaidi nilikuwa nataka kujua zile nyumba zilizotiwa maandishi, nyengine utakuta zimeandikwa *MD* mia nne na ngapi, Mhe. Waziri bila shaka anajua. Kwa sababu wale sasa hivi hawajui kama wataendelea kuwepo au ndio hawapo kwamba waondoke kabisa. Na kama wataondoka kwa kuwa sasa hivi sheria ndio tunaipitisha, je, ulipaji wao wa fidia utakuwa vipi. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na namshukuru Mhe. Mwakilishi, inaelekea ni mmoja kati ya waliyofahamu vizuri huu Mswada kutokana na maswali anayouliza. Barabara hizo alizozitaja hivi sasa zinajulikana kwamba njia kuu za kuingilia mjini Zanzibar.

Na tayari utaratibu wa *feasibility study* umeshamaliza, sasa unangojewa huo ujenzi tu, basi. Wizara ipo katika harakati ya kumpata mtu ambaye ataweza kutupatia mikopo ya kujenga hizo barabara pamoja na ulipaji wa fidia. Wote wanaohusika katika ujenzi wa barabara hizo watalipwa fidia.

Ningependa nitafautishe neno moja, ukisema mtu atalipwa kwa mujibu wa soko, sisi tuna malipo ya aina mbili. Si kwa mujibu wa mnada lakini kwa mujibu wa bei ya soko. Utaratibu wa kitaalamu wa kulipwa nyumba inapimwa *square metre* zake. Na kwa mujibu wa ujenzi wa kisasa watu ambao wamesoma fani hiyo wanaitwa *Build of quantity Engineers* wanajua

kwamba *square metres* hizi za nyumba ukitaka kuijenga sasa hivi itagharimu kiasi kadhaa.

Na sio kwamba bei ya soko ikatiwe mnada na ipandishiwe kwa mnada. Isifahamike kabisa hapa na Waheshimiwa Wajumbe, bei ya soko kwa mfano ni kuijenga ile nyumba kwa *square metres* zile zilizopo na ndio inavyochukuliwa na hawa wajenzi. Kila nyumba na kilichomo inapimwa kwa *square metres* zake na thamani yake ni kiasi fulani ndivyo utakavyolipwa.

Kwa upupi njia alizozitaja ya Bububu na Fuoni ni miongoni kati ya hizo njia tatu zitakazoingia katika mpango huo kuwa njia zinazoingia mjini. Kwa hivyo, alama hizo kama zimeshatiwa basi ni sahihi itabidi waondoke baada ya kulipwa hiyo fidia yao kwa wale waliojenga kihalali na wale ambao wamevamia tu tena watajijua namna gani ya kuondoka.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa anisaidie ufafanuzi wa mwisho ili tuendelee. Pale alipozungumzia suala la mtu atalipwa fidia kwa mujibu wa bei ya soko. Tunajua kwamba sasa kuna utaalamu kwamba wenzetu mainjinia wanatumia utaratibu wa kuangalia *square metre* na vitu kama hivyo.

Hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi wa ziada. Kuna baadhi ya maeneo hasa kuendea vijijini, nyumba ambazo zilizojengwa katika maeneo ya vijijini, nyingi zimejengwa katika vifaa ambavyo vyenye gharama ndogo, tofauti na nyumba ambazo zilizojengwa katika maeneo ya mjini.

Ina maana utakapoweka thamani kwa ajili ya vipimo vya mainjinia vya *cubic metre* na *square metre*. Je, thamani ya nyumba itakayokuwa imbebomolewa kijijini ambayo ilijengwa kwa gharama ndogo na thamani ya nyumba ambayo itakayobomolewa mjini, kwa sababu ukitumia hivi vipimo vya *square metre* ina maana haitoangalia nyumba hii ilikuwa ya aina gani. Sasa hapa ilikuwa nataka ufafanuzi.

Kwa sababu ukitaka kutumia vipimo vya *engeneer* ina maana hata ile nyumba iliyojengwa kwa miti na udongo, itakuwa na thamani sawa. Kwa sababu ukubwa wa kiwanja au ukubwa wa eneo itakuwa ni sawa sawa na ile iliyojengwa mjini. Je, hapa hizi thamani zitakuaje? Hatuoni kwamba serikali itakuja kuingia hasara zaidi kuliko kuangalia thamani ya ile nyumba moja kwa moja.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma anataka kuurefusha tu huo Mswada. Lakini nyumba si ya kijijini wala siyo ya mjini, inategemea namna gani ilivyojengwa,

imejengwa kwa tofali, nyumba ya chini, nyumba ya ghorofa vipimo vyao wanavyo hawa.

Kwa sababu ukitaka kujenga nyumba ya ghorofa huwezi ukaanza na nguzo ya boriti ukajengea, wao *engeneer* wanajua kwamba ilivyokuwa hii ni nyumba ya ghorofa basi *materials* zake ilikuwa ni kadhaa na *square metre* yake ni kadhaa na ikiwa nyumba ya kukandikwa *square metre* yake ni kadhaa. Kwa hivyo, ikiwa ipo mjini, au shamba inategemea nyumba ilivyojengwa na mle ndani mumewekwa nini.

Kwa mfano hapa mwenzangu kanambia kwamba MCC walivyofanya tathmini kule Pemba hata nyumba iliyotiwa *tiles* ilikuwa wanaitathmini vyengine na ile nyumba ambayo haina *tiles* Kwa hivyo, inaonyesha ile nyumba itakwenda kukaguliwa na kuangaliwa hali ilivyojengwa. Lakini nilisema hapa kwamba tusijetukachukuliwa kwamba ni bei ya mnada.

Kwa sababu sisi hapa tukiuza nyumba hatutizami thamani ya nyumba, tunatizama ile bei ya mnada, inawezekana nyumba ikaibwa kwa mia mbili milioni, mia moja na hamsini milioni, lakini ni tofauti na thamani yake. Kwa hivyo, tusijetukafikiria kwamba ndio serikali itakuja kulipa vile. Serikali itakuwa na wataalamu wake ambao wataitathmini ile nyumba kutokana na *materials* yaliyojengewa na namna nyumba ukubwa wake ilivyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mie hapo hapo alipokuwa Mhe. Hamza Hassan Juma, ukiachia nyumba kuna mtu ana sehemu ya kiwanja chake lakini hakuwahi kujenga kutokana na hali ya uwezo wake. Je, atafidiwa gharama gani yule mtu.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Kiwanja ni ardhi na ardhi ni sehemu ya mali ya serikali.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Tuendelee.

Kifungu cha 18 Kuongeza Kifungu Kipya cha 23(a) Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu cha 19

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, hata ulipouliza nani asiyekubaliana na hoja hii mimi niliinua mkono, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, akacheka. Akaniuliza kwa nini unakataa. Nikamwambia hapa kidogo nitakuwa mkaidi.

Kifungu hiki mfugaji hakikumfanyia haki. Hiki chombo cha wananchi wote, kama barabara wanavutia kwao tu na mfugaji na yeye pia ana haki. Kifungu cha adhabu cha 19(2), hiki mimi kwangu kina utata. Mhe. Waziri *mashallahu*, *Alhamdulillah* kabahatika kuwa mwalimu, kaongoza wanafunzi, keshakuwa Mnadhimu wa Chama cha Wananchi CUF, *Shekhe,* imamu, Alhaji, Mwakilishi karibu vipindi vitatu na leo Waziri.

Leo ni siku ya Ijumaa tusipoteze muda Mhe. Waziri, kwa heshima na taadhima ya hali ya juu, ulitaja mambo chungumzia ya aya hapa kuwa hii si haki kwamba mnyama akabebeshwa mzigo, hiki kifungu kiondoshwe. Nakuomba sana tusipoteze muda, tupo hapa kuja kutetea watu. Hata mabaniani ng'ombe wanamuabudu. Nafikiri nimezungumza kiswahili na kimeeleweka.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, umemfahamu, kama umemfahamu tunaomba maelezo ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kimewekwa kuzuia watu kufunga wanyama karibu na barabara na kusababisha ajali. Au wengine mnyama wake hamshughulikii mpaka akakata ile kamba akawa anatembea barabarani na kusababisha ajali. Kama nilivyosema mwanzo katika tafsiri, kwamba amewekwa mnyama wa kufuga, hatokamatwa mtu, akijaakionekana chui lakini ng'ombe itakuwa kuna mtu anamfuga.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, bado, pazito hapa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Yeye kakupa maelezo kwamba kifungu kinalinda wanyama wasifungwe karibu na barabara anaweza akakata akasababisha ajali watu wakafa na mali zikaharibika. Hoja yako.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, mtu unampa kiganja cha mkono anachukua mkono mzima. Kwa kweli hapa wafugaji hawakufanyiwa haki, adhabu ni kubwa, adhabu iondolewe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Wewe unapendekeza vipi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Iwekwe kanuni kwanza, waelimishwe wananchi, si tutunge sheria tu humu, kuna wengine zinawaathiri hizi. Leo Kwahani kuna mtu ana mbuzi wake kawasomea Halalbadiri, kawakataa wote sasa hivi kuna mbuzi zaidi ya 40 wanacheza barabarani, utawafanya nini wale. Kwa hiyo, hii adhabu ni kubwa, leteni kanuni kwanza, hichi chombo cha wananchi wote Mhe. Mwenyekiti, adhabu ni kubwa.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini Mhe. Waziri kaiona hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sina hakika kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kaiona hoja ya Mhe Waziri. Kwa sababu kinachotaka kuzuiwa hapa ni hatari ambayo inayoweza kutokea kwa kile kitendo cha kufunga mnyama karibu na barabara. Hivi laki tano na maisha ya watu ambayo wanaweza wakapoteza kwa ajali ambayo inaweza kusababishwa na kitendo kile, kipi kikubwa.

Sheria madhumuni yake ni kuzuia, tunaambiwa siku zote "Kinga ni bora kuliko tiba". Sasa hii inayowekwa ni kuzuia kwa sababu maafa ambayo yatatokana na ile ajali hakuna mtu ambaye anaweza akajua ni ya kiasi gani. Lakini akiumia mtu kidole tu kikakatwa kutokana na ajali, akivunjika mtu mguu akakaa kitako hivi kweli utapima kwa kiasi cha pesa.

Mimi nadhani Mhe. Jaku Hashim Ayoub, aone kile kinachotaka kuzuiwa, hapa hakusudiwi kuonewa mtu kwamba labda ng'ombe wako aende akachukuliwe au mnyama wake akachukuliwe, ni kuzuia kwa sababu maafa ambayo yanaweza yakatokana na kitendo kile ambacho kinaweza kikafanywa ni makubwa sana hayawezi kupimika, labda yeye atwambie kwa kila mtu ambaye atapoteza maisha ifanywe kiasi gani, labda inaweza ikatusaidia lakini mimi naomba aone hiyo hoja kwamba tunataka kuzuia jambo kubwa zaidi, baya zaidi, lina gharama kubwa zaidi na haliwezi kupimika thamani yake.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tumalizie hili, nadhani umemuelewa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana tena. Mhe. Mwenyekiti, adhabu bado ni kubwa, ufugaji wetu wa unyonge na anafuga huku ana tai shingoni tofauti na Bara. Bara mtu ana ng'ombe 50, mna kondoo na ana mbuzi ndani. Lakini wafugaji wetu mtu ana ng'ombe wake mmoja ndio roho yake. Kwa hivyo, kweli laki tano ndio tunafanya kweli hivi.

Mimi nafikiri tungefikiria zaidi angalau elfu 50 au 60, lakini hii adhabu ni kubwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tatizo asimfunge barabarani.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Sio tatizo Mhe. Mwenyekiti, ng'ombe unamfuga wale ndama wadogo wadogo wanakimbia kule wanakuja kukaa barabarani. Sasa utazuia vipi, sisi tumewahi kufuga huko tunakotokea na ndio ilikuwa maisha yetu. Kwa hivyo, hii adhabu ni kubwa angalau kidogo ipunguzwe

angalau tuweki laki moja basi. Maana huyo ng'ombe mwenyewe laki tano hafiki. Tuweke laki moja kama zaidi ya hapo Mhe. Waziri, kama hataki kunisikiliza basi tena sina la kumwambia tena.

**Mhe. Mwenyekiti:** Yeye kapendekeza kama hatukuafikiana tupige kura tusongembele.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, adhabu ndio hiyo imeshawekwa. Lakini mimi napenda nimkumbushe Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba angekuwa ng'ombe hula lami basi angestahiki kufungwa karibu na barabara, lakini kwa sababu anakula majani kwa nini afungwe karibu na barabara.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, unajua hapa tunapitisha sheria na kwa kuwa tunapitisha sheria tunatakiwa tupate ufafanuzi wa kina hasa kile ambacho tunakipitisha. Hapa imezungumziwa mnyama kufungwa pembezoni mwa barabara kwa hizo *metres* ambazo zilizosemwa.

Lakini hapa kuna mambo mawili katika wanyama kuingia barabarani, kuna wale waliofungwa karibu na barabara, pili kuna wale ambao hawafungwi kabisa wanatembea mpaka wanafika barabarani hasa katika Mkoa wa Kusini ambapo Mhe. Jaku Hashim Ayoub, jimbo lake lipo, ambapo Mikoa ya sehemu ya pwani pwani mingi wanyama wanakuwa hawafungwi.

Je, adhabu hii itakuwa kwa yule mnyama aliyefungwa akaingia barabarani au hata wale wanyama ambao hawakufungwa wameingia barabarani. Maana yake tusijetukakuta kwamba wafugaji wengi hasa wa maeneo ya Ukanda wa Pwani wako kizimbani baada ya kupitisha sheria hii. Sasa hapa tunataka tupate ufafanuzi wa kina ili tunapopitisha fungu hili tujue yasijeyakatukuta maafa makubwa zaidi, kuliko ile sheria tulivyoikusudia. Hapa tu kidogo nilikuwa nataka nipate ufafanuzi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri naomba utoe ufafanuzi halafu tupige kura tusikilize wajumbe wanasemaje. Kaengeza Mheshimiwa kwamba yule anaefungwa ama na wale wanaochungwa bila ya kamba, ambao wanachunga sana watu wa Kusinini Kaskazini. Mtu ana ng'ombe 40 anawaachia tu, mwenyewe yuko nyuma anachunga kwa gongo. Je, hawa nao wapo katika kifungu hiki.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, maendeleo huja na mabadiliko, hakuna maendeleo ambayo hayana mabadiliko. Sasa tukubali kwamba kupata barabara ni sehemu moja ya maendeleo kwa hivyo ni lazima tuwe na mabadiliko. Aina ya ufugaji

tuliokuwa tukiufanya kabla ya kuwepo barabara tungestahiki kuubadilisha na kufanya ufugaji wa kuwadhibiti wale wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni maendeleo ambayo tunayataka, hatuwezi kufikia maendeleo ikawa na sisi tumejiweka pale pale. Kilichotajwa katika sheria ni mnyama wa kufugwa kwa maana anaye mtu anayemdhibiti. Kwa hivyo, hatoshtakiwa mtu kwa mnyama ambaye sio wa kufugwa. Sasa akiwa yupo Kaskazini au kusini kote huko kunahitaji maendeleo. Maendeleo ya barabara kama alivyotetea Mhe. Hamza Hassan Juma,kwamba hata barabara za kuunganisha zinahitaji nazo kushughulikiwa za Halmashauri ni sawa.

Lakini na wale wanaoekewa miundombinu hiyo na wao waweze kubadilika. Hata tumezungumza hapa utaratibu wa kueka alama, nikawaomba wananchi wazistahi zile alama zinazowekwa, hayo ni mabadiliko. Kwahiyo tunawaomba sana wawakilishi watufahamu hapa hatakiwi mtu kuadhimbiwa kwa sababu ya kuadhibiwa tu lakini kuna maisha ya watu. Jana nasikia Kaskazini kumetokea ajali kwa sababu ya ng'ombe aliyefungwa karibu na barabara na watu wameumia vibaya. Sasa ndio maana ya sheria hii inaweka ili kuzuia na kuwe na matumizi mazuri ya hiyo barabara yenyewe. Nakushukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe hoja imechukua muda mrefu, maelezo yametolewa kwa ng'ombe anayefugwa hana kamba lakini anafugwa ana msimamizi wake. Sasa naomba nilihoji Baraza kwa ujumla wale wanaokubaliana na faini hii wanyooshe mkono, waliokataa. Waliokubali wameshinda. Kifungu kimepita tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu 19 | Marekebisho ya Kifungu cha 24 Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu 20 | Marekebisho ya Kifungu cha 25 Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu 21 | Marekebisho ya Kifungu cha 26 Pamoja na Marekebisho yake |
| Kifungu 22 | Marekebisho ya Kifungu cha 27 Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu 23 | Marekebisho ya Kifungu cha 30 Pamoja na Marekebisho Yake |

Kifungu 24 Marekebisho ya Kifungu cha 32 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 25

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi. Kwanza napenda nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake alionipa juu ya hoja zangu nilizochangia. Lakini kifungu hiki ni kifungu kilichokuwa kimeongezwa kifungu kipya cha 30 (a) kuhifadhi mazingira.

Sasa Mheshimiwa mie sikatai hoja ya Mhe. Waziri, kuwa mfano nilioutoa wa barabara ya Wete\Konde na Wete/Gando, hili ndio limeshapita.

Sasa hoja yangu ni kuwa hii sheria inatwambia nini kwa kipindi cha baadae. Kwa sababu suala la mazingira lina upana mrefu, hapa wanaloliona kuwa ni uhifadhi wa mazingira ya utupaji taka. Mhe. Waziri, hivi kuendelea sisi kuchukua wakandarasi kuja wakatengeneza njia miaka 10 hatimae haizingatiwi utengenezaji wa njia ile kuhusu uharibifu wa mazingira yatakayojitokeza pale.

Mimi nilitaka suala hili nijue sheria inatuambiaje, atakapokuja kufanya tena katika kipindi chengine. Sasa hapa kasema kwamba tustahamili. Ndio lakini hili limeshapita, lakini kuweko na uhifadhi sasa wa hicho kipindi chengine kinachokuja, sheria itwambie kuwa atakayepewa njia kutengeneza ni muda wa miaka fulani au serikali itakapoamua kutengeneza barabara ni kipindi fulani kama hawajawa na uwazo basi wasifanye vile.

Kwa sababu ni uchafuzi wa mazingira. Kifungu hiki naona hakijakamilika. Naomba Mhe. Waziri, anipe maelezo ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kutoa hoja yake hiyo. Mhe. Waziri anayeshughulikia mazingira anamsikia vizuri na ndio maana sisi kama Wizara katika ujenzi wa barabara tukaji-*commit* kwamba na sisi mazingira ni sehemu yetu. Kwa sababu tukizungumza mazingira hapa tunazungumza jambo ambalo mtambuka. Hii hapa imewekwa kama sheria itakavyotumika sheria ya mazingira iliyopo. Kwa hivyo, kuhusu sheria ya mazingira haitofafanuliwa hapa, inafafanuliwa katika sheria ya mazingira iliyopo. Kwa hivyo, sisi tumeji-*commit* kwamba na sisi katika ujenzi huu wa barabara na utunzaji wa barabara tutaji-*commit* katika sheria ya mazingira iliyopo. Sasa ni jukumu la hao watu wa sheria ya kutufatilia sisi. Je, na sisi tunafuata sheria hiyo. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi Mhe. Mwakilishi. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Bikame Yusuf Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, wakati ameshasema asubiri Waziri wa Mazingira ndio washirikiane, mimi nitakuwa sina la kusema tena. Lakini hapa akumbuke kuwa sentensi yao inasema kuwa "Mamlaka ya barabara inayokabidhiwa uendeshaji, uongozi na utengenezaji wa barabara za umma chini ya dhamana yake itafuata miongozo, taratibu au sheria zilizowekwa kuhusiana na uhifadhi wa mazingira na utupaji taka"

Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo tuendelee, lakini Mhe. Waziri, na Waziri mwenzake walitambue. Ahsante sana.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi ni Mwenyekiti ambae Kamati yangu inasimamia masuala ya mazingira. Siku zote kama tunavyosema tunatunga sheria nyingi nzuri lakini tatizo letu linakuja katika utekelezaji. Hii sheria ya mazingira imeeleza wazi wazi kwamba hakuna mradi wowote utakaofanywa bila ya kuanza kufanyiwa tathmini na athari ya mazingira.

Miradi inafanyika hasa hii ya ujenzi wa barabara, ambapo hata kuwasikiliza watu wa Idara ya Mazingira wanakuwa hawataki, matokeo yake barabara zile zinakuwa zinajengwa bila ya ushauri wowote wa mazingira na athari yake inakuwa kubwa sana. Tunakuwa tumeshapata barabara lakini tumepata athari kubwa sana ya mazingira.

Mimi nashukuru angalau sheria hii imetaja moja kwa moja. Hapa kitu nilichokuwa najaribu kumuuliza Mheshimiwa, kwamba katika sheria ya mazingira inasema kwamba asilimia 10 itatengwa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira. Tatizo linakuja na hapa ndio naauliza ile asilimia 10 inapelekwa Wizara ya Miundombinu ili baadae kuja kufidia zile athari za mazingira au ile asilimia 10 inatakiwa iende katika Idara ya Mazingira ili pale utakapotokezea ule uharibifu wa mazingira iweze kufidiwa. Kwa sababu hapa ndio penye tatizo, sasa hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo, ili tupate kuendelea.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, ndio hapa nilipojibu kwamba sisi tulililoiingiza hapa ni kwamba sisi tumekuwa sehemu *concerned*, aliyoisema hiyo sehemu ya mazingira ilikuwa haizingatiwi pengine katika ujenzi wa barabara. Kwa hivyo, kwa sheria hii tumejiingiza, kama kulikuwa na mambo hayo sisi ni sehemu ya hiyo sheria ya mazingira.

Kwa hivyo, yote hayo kama ni asilimia 10 au 15 yote hayo watu kutokana na sheria hii tutashirikiana na wizara inayoshughulikia mazingira, kuona sasa yale mambo ambayo yalikuwa hayafanyiki sasa yanafanyika.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kunabarabara zinazotaka kujengwa na Mhe. Waziri, kama alivyosema katika kuendeleza miundombinu hapa Zanzibar, basi Kamati yangu itafuatilia kwa karibu ili kuona kwamba hizo barabara kabla ya kuanza kupewa hawa wakandarasi tuone kwamba ule ushauri wa mazingira umeweza kupatikana.

Lakini la mwisho Mheshimiwa nilikuwa nataka tu nitoe ushauri kwa Mheshimiwa kwamba kuna kifungu ambacho tulichokipitisha sasa hivi, kifungu hiki hatujakiangalia kwa karibu zaidi lakini kwa kweli kitakuja kuleta *impact* kubwa sana kwa wafugaji. Sasa nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, katika kipindi hiki kabla ya Mhe. Rais hajatia saini, basi ajaribu kufanya makongamano na Wakuu wa Mikoa hasa maeneo ya Kusini na Kaskazini ambao wanyama wengi wanaachiwa tu hawafungwi ili waambiwe kwamba hii sheria tumeshaipitisha na baada ya miezi 3 Rais kuitia saini sheria hii itakuwa inafanya kazi. Ili tusije tukagundua kwamba wananchi wetu wengi wamekwenda Mahkamani kwa jambo ambalo walikuwa hawalijui, hili tu nilikuwa natoa ushauri wa bure kwa Mhe. Waziri.

Na kwa kuwa Mhe. Issa Haji Ussi Naibu Waziri na yeye jimbo lake la Chwaka ni hao watu ambao hawafungi ng'ombe na mbuzi, ninaamini itaweza kusaidia sana wananchi wake wasije wakafungwa halafu akapeleka barua watolewe. Ahsante.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Mwenyekiti mimi nimemsikia sana Mhe. Waziri anavyozungumza katika kifungu hiki cha mazingra. Lakini pamoja na utetezi wake anaojitetea, Mheshimiwa Wizara yake ya Mawasiliano wao kabisa ni waharibifu wakubwa wa mazingira. Lakini pamoja na kifungu hiki wanachokiweka lakini tulitaka na wao kwenye sheria hii waweke kifungu kama yale mazingira wakishayaharibu je watachukua hatua gani.

Kwa sababu katika sheria hii wanasema tundu, shimo, sasa mashimo yanayochimbwa kwetu Micheweni sio matundu yale, tundu ni ndogo, yale ni mashimo. Kwa hivyo, tulitaka kwenye kifungu hiki waweke kifungu kama yanapokuja makampuni watasimamia vipi utunzaji wa mazingira baada ya kuharibu.

Pamoja na kuwa kasema watashirikiana na sheria ile ya mazingira lakini na huku kwenye mambo ya barabara wangeweka sheria yanapokuja makampuni wakajua kwamba kuna sheria fulani inyofuatwa. Sasa tulitaka atupe maelezo zaidi wao watasimamia vipi.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mheshimiwa ninamshukuru sana Mhe. Mwakilishi, lakini kasahau yeye msemo wa

kiswahili, mganga hajigangi. Mimi ninae pale *overstear* wangu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, yeye ndie aliyekabidhiwa mazingira, amwambie yeye mbona mawasiliano hawafuatilii. Lakini akinambia mimi nitamwambia nimeshatengeneza na pengine sijatengeneza.

Kwa hivyo, angojee siku ya Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, aje amwambie. La kwanza hilo, la pili hii sheria yenyewe ambayo tumeitaja leo madhali tumeji-*commit* kwamba na sisi tumo na sisi tushakuwemo humo katika kuyatunza hayo mazingira. Kwa hivyo, tukutane nae atuoneshe hapo pahali ambapo sisi tumeharibu mazingira, tukasawazishe.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Mwenyekiti pamoja na maelezo mazuri ya Waziri aliyoyaeleza, kwanza mashimo kama anataka kuoneshwa hayajifichi yapo wazi Micheweni. Na matatizo yake ni kwamba wakishaharibu hawatengenezi kwa sababu wao walitwambia kwamba makampuni wanakubaliana kama wakeshaharibu wayafukie.

Lakini sasa hayafukiwi, hivyo tulitaka kwenye sheria aji-*commit* mwenyewe kama yeye atashirikiana na Ofisi ya Makamu ya Kwanza wa Raisi inayotunza mazingira ili kile kifungu kitakachoingia cha mazingira kiingizwe kule, sio wapewe wao halafu hawatekelezi.

Pia, kama Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndio wanaohifadhi mazingira kile kifungu cha fedha kinachopatikana kiingizwe kwenye sheria yake kama watapewa wale ili watunze mazingira.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mimi nadhani kakubali Mhe. Waziri, mnakosana lugha tu. Kwa hivyo, suala lako atalichukua na litafanyiwa kazi.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani tusiwe na utata kwa sababu Waziri wa Mazingira yupo na miradi yoyote ya serikali lazima inaingiliana na mazingira hata ya binafsi. Sasa mimi naomba Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwanza mimi niulize Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuna sheria yoyote ambayo inakidhi haja na haya tunayoyazunguza.

Kama kuna sheria haikidhi haja na haya tunayoyazungumza, basi ninaiomba serikali kwa jumla, kitu chochote cha maendeleo ambacho kinafanywa kinaharibu mazingara, ishirikiane na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, wawe karibu ili kuhakikisha hii migongano haipo.

Ninamuomba Mhe. Waziri, asiji-*commit* mambo hajazungumza na mwenziwe si vizuri tukazozana kwa kitu ambacho miongoni mwetu ni chetu. Niseme hivyo tu Mhe. Mwenyekiti ni kwamba Mawaziri mukae pamoja kabla ya mambo yote kutiwa saini na Rais muyarekebishe.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti nimelazimika kunyanyuka kwa kujibu swali la Mhe. Asha Bakari Makame, kuhusiana na suala zima la uwepo wa sheria inayokidhi haja katika masuala haya yanayozungumzwa ya kulinda mazingira, hususan yanayoharibiwa katika shughuli nzima za kuleta maendeleo, kama kujenga barabara.

Kwa kweli sheria iliyokuwepo haikuwa na meno na nimeshazungumza ndani ya Baraza hili kwamba tumo kwenye mchakato na waheshimiwa wajumbe naomba wavumilie sana. Ni muda mrefu inachukuliwa kufanyiwa marekebisho ili iweze kuwa na nguvu za kuweza kukabiliana na masuala haya.

Kwa hivyo, wasiwe na wasiwasi, sisi tunaifanya sheria yetu iweze kuwa na nguvu kuweza kuwajibisha yule ambaye ana jukumu la kurekebisha mazingira baada ya kuweka uekezaji au kuleta maendeleo. Mfano kujenga barabara ili aweze kuwajibika kikamilifu kuyarudisha mazingira yale katika uhalisia wake, au angalau kuleta hali ambayo kidogo ni nzuri kuliko kuwacha mashimo makubwa ambayo ni hatari kubwa ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru.

Kifungu cha 25 Kuongeza kipya cha 30(a)

Kifungu cha 26 Kuongeza kifungu kipya cha 33 pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 27 Kuongeza kifungu kipya cha 34 pamoja na marekebisho yake

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa kamati ya kutunga sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa ninaliomba Baraza lako Tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa wajumbe niwahoji waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

**Mswada wa Sheria ya Amri ya Barabara ya mwaka 2013**

*(Kusomwa kwa mara ya tatu)*

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Amri ya Barabara ya 2013 usomwe kwa mara ya tatu.

Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokuali wameshinda. *(Makofi).*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukuwe nafasi hii kuwashukuru kwa ushirikiano wetu wa tangu asubuhi mpaka hivi sasa na tumeweza kuupitisha mswada wetu katika hali nzuri, majadiliano yalikuwa mazuri, tumekubaliana mswada umepita, na yale ya kufanyiwa kazi Waziri na Waziri mwenzake wakae pamoja waifanyie kazi kabla sheria haijatiwa sahihi.

Kwa kuwa muda wetu uliobakia ni mdogo na tuna mswada mwengine hapa wa kuwasilisha. Ninakiakhirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 05.42 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

**Mswada wa Sheria ya Kukinga na Kusimamia Mambo ya UKIMWI Zanzibar, ya 2013**

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote natanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya na kuweza kuendelea na shughuli za kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kukinga na Kusimamia Mambo ya UKIMWI Zanzibar, 2013. Mhe. Naibu Spika, Mswada huu unawasilishwa pamoja na marekebisho yote yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe, yale yaliyotoka kwa Wajumbe wa Kamati ambayo Ofisi imeyakubali na yale ambayo yameletwa na ofisi yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu lipokee na kujadili mswada huu na hatimaye kuupitisha kuwa sheria kamili. Mswada huu unatokana na Sheria Nam. 3 ya mwaka 2002, ambayo iliunda Tume ya UKIMWI Zanzibar. Sheria hio ilitoa muongozo wa taasisi inayoshughulikia masuala ya UKIMWI pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kiutendaji katika kusimamia suala zima la UKIMWI ili kuona kwamba Zanzibar inaepukana na UKIMWI pamoja na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI.

**Madhumuni na Sababu ya Mswada huu**

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la Mswada huu wa Sheria ni kuweka mfumo wa kisheria wa kuzuia na kuweza kusimamia masuala yote ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI Zanzibar, kwa ajili ya kulinda na kuimarisha haki za binadamu kwa watu wanaoishi au waliyoathirika na virusi vya UKIMWI na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mswada huu unajumuisha sekta chanya, muingiliano wa kuzuia na kusimamia UKIMWI ambayo ni kiashiria cha kimataifa katika hali ya sasa.

Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa mfumo wa sheria ya kuzuwia na kusimamia Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kunaonesha kuwepo kwa tofauti ya mtazamo kati ya serikali na taasisi zisizo za kiserikali, ingawa wanaweza wakawa na lengo moja. Lakini wamekuwa wakifanya kazi bila ya utaratibu mzuri au maelewano na kubwa zaidi bila ya kuwepo kiwango

chochote kinachowabana katika kutekeleza kazi zao. Mhe. Naibu Spika, hili halina shaka kwamba limechangia kwa kiasi fulani kupatikana kwa mafanikio madogo katika juhudi za kusimamia mapambano dhidi ya UKIMWI Zanzibar.

Pamoja na mambo mengine sheria hii itaimarisha uhamasishaji wa wananchi kuhusu chanzo, njia za maambukizi, athari, njia za kujikinga, kudhibiti na kusimamia Virusi vya UKIMWI na UKIMWI na kuimarisha njia nzuri za kushughulikia masuala yanayohusiana na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Hii itapelekea kupanua wigo kwa mtu anayeshukiwa au anayejulikana kuwa ameathirika au aliyeathirika na UKIMWI kwa kupewa ulinzi na uhakika wa haki zake na uhuru wa mtu binafsi.

Vile vile, itaimarisha usalama na tahadhari katika njia zilizo hatari za maambukizi ya UKIMWI. Hatimaye sheria imedhamiria kupambana na kuondosha njia zinazosababisha maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

**Muundo wa Sheria**

Kwa ujumla sheria hii imegawika katika sehemu kuu kumi ikijumuisha kwa pamoja vifungu 46.

Sehemu ya Kwanza, inahusu utangulizi na inazungumzia uhalali wa kuanza kutumika kwa sheria hii na kutoa tafsiri ya maneno muhimu kwa mujibu wa sheria hii na inahusisha kifungu cha kwanza na cha pili.

Sehemu ya Pili, ambayo inahusisha kifungu cha tatu na cha nne ina vifungu vinavyohusiana na majukumu ya jumla pamoja na majukumu ya mtu mmoja mmoja katika kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Sehemu ya Tatu, ina vifungu vinavyohusiana na taarifa, elimu na mawasiliano ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Imeweka vifungu vya taarifa, elimu na mawasiliano katika taasisi za elimu, sehemu za kazi kama huduma ya afya katika vyombo vya habari na jamii ambapo kwa kufanya hivyo kutapelekea muamko kwa jamii katika masuala yanayohusiana na virusi vya UKIMWI. Sehemu hii ya tatu inaanzia kifungu cha 6 na kumalizia katika kifungu cha 10.

Sehemu ya Nne, imeweka hatua mbali mbali na taratibu za kuzuia maambukizi ya UKIMWI chini ya kifungu cha 11 cha sheria hii. Tume ya UKIMWI ya Zanzibar inatakiwa kuchukua hatua mbali mbali kuimarisha utekelezaji na taratibu za kupunguza athari za maambukizo ya UKIMWI zinazoweza kutokea.Sheria hii imeweka vifungu kuhusiana na kupima wakati wa kuchangia viungo vya mwili, kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto na miongozo madhubuti inayohusiana na upasuaji na taratibu nyengine

zinazofanana na hizo. Sehemu hii imeanzia kifungu cha 11 na kumalizia kwenye kifungu cha 14.

Sehemu ya Tano, ina vifungu vinavyolenga kuweka miko na mbinu za kushauri na kupima virusi vya UKIMWI na UKIMWI na inaanzia kifungu cha 15 na kumalizia kwenye kifungu cha 22.

Sehemu ya Sita, imeelezea vipengele kuhusu ulinzi wa watu wanaoishi au walioathiriwa na UKIMWI. Sehemu hii inatambua kwamba, mtu anayeishi au aliyeathiriwa na UKIMWI anafurahia bila ya ubaguzi na anapata haki zake zote za binadamu kwa mujibu wa sheria na kuondoa aina zote za ubaguzi wa bayana au wa kujificha dhini yao, hasa kuondoa ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi au wanaoathiriwa na UKIMWI katika masuala ya kupata mikopo na huduma binafsi katika taasisi na katika masuala yote yanayohusu huduma za afya. Sehemu hii inaanzia kifungu cha 23 na kumalizia kwenye kifungu cha 31.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Saba, imeweka vifungu vya kulinda makundi hatarishi na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi ya UKIMWI. Vifungu maalum vimewekwa kwa kuwalinda watoto wanaoishi au walioathirika na UKIMWI wanawake na wasichana, watu wenye ulemavu na wafungwa, zaidi kifungu cha 34 kimeitaka serikali kwa kushauriana na tume kuandaa na kutekeleza mikakati, sera na mpango wa kuimarisha na kulinda afya ya makundi hatarishi na watu wanaoishi katika hatari zaidi ya kuambukizwa ambao hawajatajwa katika sehemu hii.

Mikakati hii na sera itatumika kwa makundi yote ambayo yako katika hatari ya kuambukizwa kwa kiwango cha juu au yanayoongoza katika maambukizi au yanayoonekana yako juu katika taarifa za UKIMWI za jumla au yapo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya kwa sababu tu ya umasikini, maisha yao, utumiaji wa dawa za kulevya, uasharati, kuvunjika kwa maadili au muingiliano wa kijamii. Sehemu hii inaanzia kifungu cha 32 na kumalizia kifungu cha 35.

Sehemu ya Nane, Mhe. Naibu Spika, imepiga marufuku utafiti katika mambo yote yanayohusiana na tiba ya UKIMWI kwa binadamu, kijamii au utafiti wowote wa mtu mwengine au utafiti wa chembe hai za mwili wa binadamu au utoaji wa damu kwa mtu yeyote isipokuwa kwa wale waliotajwa na sheria hii au sheria nyengine yoyote ile inayotumika. Kwa kuongezea makosa yametajwa katika sehemu husika za sheria hii inayopendekezwa na inahusisha kifungu cha 36 na 37.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Tisa, imeweka makosa yanayotokana na UKIMWI pamoja na adhabu zake. Makosa yanayohusiana na utoaji wa siri, kutoa taarifa za uongo kuhusiana na tiba ya UKIMWI na kizuizi cha utekelezaji wa majukumu. Sehemu hii inahusisha kifungu cha 38 hadi kifungu cha 40.

Sehemu ya Kumi, inajumuisha vifungu vinavyohusiana na mambo mengineyo, vifungu vinaitaka serikali kusaidia jumuiya za watu wanaoishi au walioathirika na UKIMWI pamoja na wale watu wa huduma majumbani. Sheria inayopendekezwa imeazimia kwa nia nzuri zaidi katika mambo yote yanayohusiana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Mwisho mswada huu katika kifungu cha 46 kimetambua kwamba masuala yote yanayohusiana na UKIMWI na virusi vya UKIMWI, iwapo kutakuwa na mgongano wa kisheria basi sheria hii ndio itakayotumika pamoja na kanuni zilizoundwa kwa ajili hiyo. Sehemu hii ya 10 inahusisha kifungu cha 41 hadi kifungu cha 46.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupokee, waujadili na kuuchangia mswada huu ili hatimaye waweze kuupitisha kuwa ni sheria kamili. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza, Mhe. Naibu Spika, sasa kwa heshima naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake, ikiwemo kupitisha miswada mbali mbali ukiwemo mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya Ukimwi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi maoni kuhusu Mswada niliokwisha uainisha hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuwa na sheria madhubuti inayowakomboa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na kupunguza changamoto zinazowakabili kupitia sheria hii.

Vile vile, kamati inapenda kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliokuja kushiriki katika kutoa maoni juu ya mswada huu ambao kwa kweli Kamati imefarajika sana na uwepo wao, kwani imeweza kupata mengi kutoka kwao ambayo yamesaidia uboreshaji wa mswada huu. Wadau hao ni pamoja na *ZAPHA+, ZAFELA, TAMWA, ZYF* na wadau wengine kutoka sehemu na taasisi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya utangulizi huo Kamati yangu inapongeza hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ya kuwasilisha mswada huu muhimu ambao utasaidia sana kupunguza changamoto zinazoikabili jamii juu ya maradhi ya UKIMWI kwa kuweka sheria, taratibu, haki, ulinzi na adhabu ambavyo vyote hivyo vimewekwa kwa madhumuni ya kulinda na kuimarisha haki za binaadamu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokua tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu na hatimae kupitishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu. Naomba sasa kwa ruhsa yako niwataje Wajumbe wa Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Mjumbe
8. Ndg Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg Makame Salim Ali - Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa napenda kutoa maoni ya kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Mswada huu uliopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali lengo kuu la mswada huu ni kuweka sheria madhubuti ya kusimamia masuala ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI Zanzibar ambapo itasaidia kuimarisha upatikanaji wa haki,fursa na kinga dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuweza kuondosha kabisa unyanyapaa uliopo kwa baadhi ya wanajamii ambao ni changamoto kubwa inayoikabili jamii na kupelekea kutokea matukio yasiyotarajiwa ambayo yanaathiri nguvu kazi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umeweka wazi vifungu vinavyoelezea utolewaji wa elimu kuhusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI kupitia jamii, sehemu za kazi, vyombo vya habari, taasisi za elimu, sehemu za ibada na vyuo vya mafunzo ambapo elimu hii itasaidia sana mabadiliko kwa jamii yetu. Kamati kwa upande wake imeona ni hatua nzuri na muhimu kuchukuliwa na kutekelezwa ipasavyo kwani changamoto zinazojitokeza juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI zinasababishwa na jamii yetu kutokua na elimu ya kutosha kuhusu UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, kamati kupitia sheria hii inasisitiza uharakishaji wa kanuni ambazo zitasaidia kutoa ufafanuzi wa sheria mama pamoja na utekelezaji mzuri wa sheria hii, ambazo zitasaidia kufikia azma iliyokusudiwa na kuacha mazoea yaliyopo kwa sheria zetu nyingi kukosa kanuni kwa muda mrefu ambapo huwa ni kikwazo katika ufanisi wa utekelezaji wa sheria husika.

Mhe. Naibu Spika, Kamati kwa upande mwengine kupitia mswada inasisitiza suala la usiri katika maradhi ya UKIMWI ambapo inapendekeza na inasisitiza juu ya suala hili na mkazo zaidi uwekwe katika kumuelimisha mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI juu ya umuhimu wa kuelezea hali yake kwa watu wake iwapo ameambukizwa, kwani kufanya hivyo kutasaidia kupunguza makali ya maradhi haya ijapokuwa katika hili kikwazo ni suala la unyanyapaa, lakini bado kujielezea aliyeambukizwa virusi vya UKIMWI hali yake ni muhimu kwa kuilinda jamii pamoja na watu wake wa karibu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kamati kuupitia mswada huu imeweza kupendekeza baadhi ya vifungu kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka usawa na miongoni mwa vifungu hivyo ni kifungu cha 43 kinachozungumzia adhabu ya jumla. Katika kifungu hichi kamati imependekeza kuwe na uwiano baina ya faini na adhabu kwa ajili ya kuondoa utata unaojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria husika.

Vile vile, baadhi ya maneno kamati imeona ni vyema kutumiwa kama ambavyo inatakikana mfano neno "muathirika" kamati imependekeza kuitwa "mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI". Hata hivyo, kamati imefanyia marekebisho baadhi ya vifungu kama inavyojionesha katika waraka wa marekebisho ya kamati.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako Tukufu juu ya mswada uliopo mbele yetu. Pia, naomba Waheshimiwa Wajumbe wauchambue, waujadili, wauboreshe na hatimae waupitishe kwa madhumuni ya kupata sheria ya kusimamia masuala ya UKIMWI ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa makini, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita mchangiaji mwengine pana tangazo nimepata kutoka kwa Mhe. Waziri kwamba yeyote anayetaka kuangalia afya yake kwa kupima UKIMWI wataalamu wako nje na mtapimwa bure, kuanzia leo, kesho tumepewa nafasi kwenda kupima bure. Kwa hivyo, tunaoa fursa hiyo. Baada ya tangazo hilo sasa nampa nafasi Mhe. Salma Moh'd Ali na baadae afuatie Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

**Mhe. Salma Mohamed Ali:** Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa jioni hii. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii muhimu. Pia, naomba nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kutuletea mswada huu muhimu sana, nampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu katika ukurasa wa 312 kifungu cha 2 chenye *heading* ya tafsiri, kuna tafsiri ya mtu aliyeathirika. Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 2(a) mtu aliyeathirika imeambiwa ni mtu anayehusiana au anayeshirikiana na mtu mwenye virusi vya UKIMWI.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tafsiri hii inahitaji ufafanuzi.Hivyo, kweli mtu kuhusiana na mtu aliye na UKIMWI au na virusi vya UKIMWI na yeye ndio keshakuwa muathirika. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze kuhusiana huku ni kupi, kwa sababu Wazanzibari tuna uhusiano wa koo pana, yaani wengine wanaita *extended family*. Kwa tafsiri hii itakuwa Wazanzibari wote tumeathirika. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atueleze ni uhusiano upi aliyokusudia hapa.

Vile vile, katika kifungu cha 2(b) mtu aliyeathirika ametajwa kuwa ni pamoja na anayeshirikiana na vikundi vya UKIMWI au mfanyakazi katika mazingira hayo. Hapa napo panahitaji ufafanuzi na vipi watu wanaoshirikiana kwa njia moja au nyengine na vikundi vya UKIMWI nao wanaambiwa wameathirika au anayefanya kazi katika mazingira hayo.

Mhe. Naibu Spika, kuna wafanyabiashara wadogo wadogo wengi tu tunaowajua kama wanaishi na virusi vya UKIMWI na wanategemea biashara zao kwa mikopo kwa wafanyabiashara wakubwa.

Sasa Mhe. Waziri, hebu atwambie wale wafanyabiashara wakubwa wanaowakopesha wafanyabiashara wadogo walioathirika na wao watakuwa wameshaathirika na UKIMWI. Pia, kuna watu wengine ni wameathirika ni wafanyabiashara wa mboga mboga, watu hawa wanaishi na virusi vya UKIMWI na wao hawalimi, lakini wanachukua bidhaa zao kutoka kwa wakulima na hupewa kwa mkopo. Kwa hiyo, wale wakulima kuwasaidia wale watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wao tayari wameshaathirika. Hapa Mhe. Waziri, naomba atueleze.

Kwa maoni yangu Mhe. Naibu Spika, ikiwa tafsiri hii itatumika, hii itawafanya watu wasiwe tayari kuwasaidia watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Wazir, atufahamishe vizuri hapa.

Katika kifungu cha 5(2)(b) kimemalizia na kupinga dhana iliyopitwa na wakati ikiwa mwanamme ndiye mtawala. Mhe. Naibu Spika, mimi ni mwanamke na napinga sana udhalilishaji wa wanawake pamoja na udhalilishaji wa watoto wa kike. Lakini Mhe. Naibu Spika, hapa nataka nitoe indhari kidogo, wakati wa kufanya kampeni ya kupinga dhana iliyopitwa na wakati kuwa mwanamme ndiye mtawala tusije tukagusa hisia za kidini.

Kwa sababu watu wengi siku hizi wanasoma elimu ya dini na katika Qurani kuna aya inayosema, *"Alrijalu Kawamuuna Alannisai"*.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, hapa katika kampeni zetu ni lazima tuwe makini sana tukija tukigusa hisia za kidini, basi tuhakikishe tutafeli.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nikumbushie ile kadhia ya Marehemu Sofia Kawawa na usawa wa mirathi, mwanamke na mwanamme jinsi ya hali ilivyokuwa. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, hapa ushauri wangu nadhani kampeni za aina hii zinahitaji kufanywa kwa uangalifu mkubwa na kwa utaratibu unaoiweka nchi katika hali ya utulivu.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya nne ya mswada huu yenye vifungu 11, 12, 13 na 14 ni muhimu sana kufanyiwa kazi. Taarifa za hivi karibuni kwamba takwimu za maambukizo zimeongezeka kutoka asilimia 0.6 hadi asilimia 1 ni za kutisha.

Mhe. Naibu Spika, tafsiri nyepesi ya kupanda kwa takwimu hizi zinatupa somo kwamba Wazanzibari hatuko makini tumejisahau na kila mmoja wetu lazima tuzinduke ili kuona tunafanya kazi kwa pamoja kupunguza ongezeko la watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Hili Mhe. Naibu Spika, si suala la wizara, ni suala letu sote.

Katika kifungu cha 20(2) kinazungumzia hakutatakiwa ridhaa kwa mtu kupima virusi vya UKIMWI isipokuwa pametajwa mambo manne, kwa amri ya Mahakama katika kuchangia viungo kwa watuhumiwa wa makosa ya kujamiiana na kwa wanawake wajawazito. Mimi hapa napenda niongeze kifungu kimoja cha tano, mimi naunga mkono sana, lakini naomba paongezwe na watu wanapotaka kufunga ndoa. Mhe. Naibu Spika, jamii sasa hivi imeshakubali jambo hili.

Kwa hivyo, ni vyema litiwe katika hii sheria na hii ndio fursa nzuri Mhe. Naibu Spika, kuliweka katika sheria rasmi. Kwa sababu hao wanaofunga ndoa wanapokwenda kupima virusi wengine hawataki, wanakwenda kwa sababu ishakuwa kama ni lazima tu, lakini ikiwa itaonekana kwenye sheria haisisitizi hili watu wataanza kuowana bila ya kupima virusi.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia ndoa nyingi kuvunjika kwa mmoja kuwa ni muathirika, ikiwa kutakuwa hakuna kupima virusi hapa basi ninahakikisha idadi ya ongezeko la watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI itaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina mfano ni nyumba ya tano tu kutoka pangu nimealikwa shughuli bado kama wiki mbili na shughuli ile ilivunjika kwa sababu mmoja wao alikuwa na virusi vya UKIMWI. Sasa ikiwa hapa tutaambiwa mambo yaliyokuwa ni lazima kupima UKIMWI ni haya tu, basi yule angelikuwa keshaongeza idadi.

Halafu suala jengine ambalo katika hivi vifungu vilivyotiliwa msisitizo kuwa kupima UKIMWI ni lazima ni katika wajawazito. Mhe. Waziri, namuomba akija anieleze hawa wajawazito kulazimishwa kupima UKIMWI wao kwa sababu huwa wanahofiwa wale madaktari wakati wa kuwazalisha kupata maambukizo au anahofiwa watoto watakapozaliwa kupata maambukizo.

Kwa sababu ikiwa ni hilo Mhe. Naibu Spika, basi na yule baba pengine anaweza akamuambukiza mama na ujauzito wake ule, kwa nini hawaambiwi

huyu mama wakati akiwa mjamzito kwenda kupima virusi afuatane na yule baba.

Kwa sababu mama huyu kupimwa virusi vya UKIMWI pengine ana mimba mwezi wa tatu inawezekana akawa mumewe tayari keshaathirika, lakini yeye hajapata, lakini kwa sababu inaonekana mama tu ndio tatizo yule anaachwa akaja akamuambukiza yule mwanamke pamoja na yule mtoto. Sasa ikiwa tuna nia ya kumhamisha mtoto pamoja na yule mama ,basi huyo mama akiwa mjamzito ende pamoja na mumewe.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie hasa watu waliokuwa ni wazito kuangalia afya zao kwa suala hili ni wanaume, huna vya kuwaambia. Kwa hivyo, hapa naomba pafanyiwe marekebisho yule mama akiwa mjamzito ende na mumewe. (*Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 35 cha mswada huu kinazungumzia kuhusu huduma za waathirika katika vyuo vyetu vya mafunzo. Hili ni jambo zuri, lakini jambo hili linahitaji faragha na siri ya muathirika. Mhe. Naibu Spika, sio siri ujenzi wa miundombinu wa vyuo vyetu vya mafunzo ni ile ile ya jela na inaonekana tumebadilisha jina tu kutoka jela tukaita chuo cha mafunzo, lakini kwa kweli ni ile ile kijelajela. Majengo pamoja na vyoo ni kijelajela tu, hakuna chuo cha mafunzo.

Sasa hapa ushauri wangu serikali inahitaji kubadilisha miundombinu ya sehemu ambazo wahalifu na watuhumiwa wanalala, ikiwa serikali haikufanya hivyo, basi kifungu hiki cha 35 cha mswada huu utekelezaji wake utabakia kwenye maandishi tu.

Mhe. Naibu Spika, sasa kidogo nataka nije kwenye marekebisho. Katika hizi karatasi tulizopewa za marekebisho kuna neno hapa tumeambiwa 'UKIMWI' liliopo katika mswada huu liandikwe kwa herufi kubwa kila tutakapoliona. Lakini vile vile, tumeambiwa pia UKIMWI huo huo kila tutakapoliona neno hili la 'UKIMWI' litakapojitokeza katika mswada lisomwe kwa herufi kubwa.

Sasa namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anifahamishe kusoma kwa herufi kubwa UKIMWI ni kupi, kwa sababu mimi naona nikisoma kwa herufi ndogo ni ile ile UKIMWI nikisoma kwa herufi kubwa ni ile ile UKIMWI, Kiswahili ni kizito.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri, katika majumuisho yake anambie kuandika nimefahamu, lakini kusoma sijafahamu kwa hiyo namuomba sana anifahamishe huko kusoma UKIMWI kwa herufi kubwa. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda wako na naunga mkono mswada. (*Makofi*).

**Mhe. Naibu Spika**: Ahsante sana Mhe. Salma Mohammed Ali, sasa nafasi tunampa Mhe. Abdalla Juma Abdalla na aliyekuwa na nia ya kuchangia alete jina ili tuende uzuri.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ninakushukuru kunipatia nafasi hii adhimu katika kuchangia mswada huu adhimu ambao kwa kweli ni mswada muhimu sana kwa maisha ya Wazanzibari.

Kwanza ninataka nimpongeze Waziri sana kwa kufikiria kuuleta mswada huu muhimu sana. Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka nianze kwenye ukurasa wa 312 na ninataka nianze kwa kifungu cha 2 ambacho ni tafsiri ya maneno. Hapa kuna tafsiri ya mtu aliyeathirika na inasomeka kwamba "Mtu aliyeathirika kuhusiana na virusi vya Ukimwi inajumuisha mtu ambaye anahusiana au anashirikiana na mtu mwenye au anayeaminika kuwa anaishi na virusi vya ukimwi".

Sasa mimi ninadhani huyu Mhe. Naibu Spika, atakuwa hajaathirika huyu labda ni mtu tuseme aliyekuwa katika yale makundi hatarishi. Lakini mimi nilikuwa naona mtu aliyeathirika ni yule aliyepimwa na akangundulikana ama ana virusi vya ukimwi au ana ukimwi, huyo utamwita mtu aliyeathirika, lakini mtu anayehusiana na huo uhusiano hatujajua ni upi, lakini iwe vyovyote itakavyokuwa au anashirikiana na mtu mwenye virusi vya ukimwi, ninadhani huyo ndio tumuweke mtu aliyekuwa ameathirika. Kwa sababu kuna watu wameshirikiana kimwili na watu waliokuwa na virusi vya ukimwi na walipopimwa ni *negative*.

Sasa hiyo kesi inatokea. Kwa hivyo, tusi-*assume* tu kwamba kila aliyeshirikiana na mtu mwenye virusi vya ukimwi na yeye tayari ni muathirika mpaka kwanza tumpime. Na kifungu (b) hapa ukisoma vile vile, kwamba inachukuliwa mtu aliyeathirika anaaminika kuwa ni mwanachama au anashirikiana na kikundi harakati anafanyakazi, anaishi katika mazingira ambayo yanaaminika kuwa yanahusika na dhara yanayoambatana na uenezaji wa ukimwi.

Mimi ninafikiri vifungu viwili hivi havitoi tafsiri halisi ya mtu aliyeathirika. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, hii tafsiri ya mtu aliyeathirika tuiangalie tena upya. Mtu aliyeathirika tuseme tu kama ni yule mtu aliyepimwa akaonekana ana virusi vya ukimwi au ana ukimwi, ndio mtu aliyeathirika.

Kwenye kifungu hicho hicho cha tafsiri , kuna tafsiri ya neno "ulemavu". Ukisoma ukurasa 313 hiyo tafsiri imetolewa mara mbili, sijui ni ipi halisi tafsiri ya ulemavu. Maana yake ulemavu imetafsiriwa mara ya kwanza, halafu neno linalofuata chini vile vile ni ulemavu limetafsiriwa tena kwa lugha nyengine kidogo.

Sasa nilikuwa Mhe. Waziri, aliangalie hilo kidogo na ikiwezekana tupate tafsiri moja ya mtu aliye na ulemavu.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 314. Na hii bado tunaendelea na kifungu kile kile cha 2 cha tafsiri. Kuna tafsiri ya neno "Huduma ya afya". Imeelezwa hapa huduma ya afya maana yake ni "Hospitali inayotolewa kwa mtu, majumuisho lakini haijifungi kwa..."

Sasa niliona kama haya maneno yanazunguka zunguka sana. Mimi ninadhani tungesema tu kwamba huduma ya afya inajumuisha, tena ziendelee zile (a), (b) mpaka mwisho. Lakini haya maneno maana yake ni hospitali inayotolewa ninadhani hayana ulazima haya maneno pamoja na hayo hiyo lugha yenyewe iliyotumika kama kwamba ya kutatanisha kidogo. Sasa nilikuwa naomba haya maneno yafutwe na iandikwe tu "Huduma ya afya" inajumuisha:-

(a) uchunguzi wa mwili au akili kwa mtu huyo, matibabu na mengineyo.

Tukiondoka hapo tuje sehemu ya pili ukurasa wa 317. Hapa nilikuwa ninahisi kifungu cha 3 (d). Pale kuna sentensi imeandikwa, "kuhakikisha kuwa taarifa na huduma zinazohusiana na virusi vya ukimwi na ukosefu wa kinga mwilini", sasa niliona kama ni *repetition*, kwa ule kifupi cha ukimwi na neno ukosefu wa kinga mwilini ni neno hilo hilo.

Kwa hivyo, ninapenda haya maneno "ukosefu wa kinga mwilini" bora yafutwe ibakie hilo neno ukimwi tu, litakuwa linatosheleza au linakamilisha maana iliyokusudiwa.

Nikiondoka hapo nije ukurasa wa 318. Hapa kifungu cha 4 kinasema "Wajibu wa jumla wa watu kila mtu aliyesajiliwa anayefanya kazi au vyenginevyo aliyeopo Zanzibar anawajibika". Neno "anawajibika" Mhe. Naibu Spika, ninafikiri halina tofauti na lazima. Kwa hivyo, mtu huyo mimi naona anawajibika au analazimika ina maana moja. Kwa hivyo, hivi vilivyobakia hapa vyote itakuwa ni lazima kwa huyo kufanya.

Kwanza kuchukua hatua zinazofaa kujua hali ya virusi vya ukimwi. Sasa kama ni tafsiri hiyo niliyoifikiria mimi ndio ilivyo na hii (a) pia nilitaka ibadilishwe kidogo. Maana kuchukua hatua zinazofaa kujua hali ya virusi vya ukimwi, sawa sawa na kusema apimwe ukimwi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba isomeke hivyo, kwamba mtu huyo atakuwa na ulazima (a) kupima ukimwi wa afya yake na mengine yanayofuata huko.

Lakini nikiondoka hapo ninakuja kwenye kifungu cha 5. Sasa kwa mantiki ya kifungu cha 4 kwamba mtu anawajibika au analazimika, lakini ukisoma kifungu cha 5 ana hiyari. Kifungu cha 5 (2) (b). Yaani kifungu hicho kinasema:-

Kifungu cha 5(2) (b) Kampeni za elimu na taarifa zilizoelezwa katika kijifungu cha 1 cha kifungu hiki zitatolewa..., hiyo (a) ninaiacha lakini (b) zitaelekezwa katika kushajihisha upimaji wa hiyari kwa watu. Sasa mimi nilikuwa naomba hilo neno "hiyari" litoke, kwa sababu huku nyuma tayari tumeshasema huyu mtu anawajibika. Sasa kama anawajibika, maana yake analazimika, sasa huo uhiyari una maana gani. Kwa hivyo, maana yake iwe tu kama anatakiwa apime ukimwi tu basi.

Na hiyo (d) ambaye hata Mheshimiwa aliyetangulia aliigusia na mimi nilikuwa nimei-*mark* hapa kwamba Mhe. Naibu Spika, unajua tukipitisha sheria na jamii yetu hii ya Wazanzibari siku hizi, kwa kweli wameelimika. Mimi ninashukuru sana Wazanzibari wameelimika sana, huwezi kuwadanganya kirahisi, halafu ni wadadisi sana wa mambo.

Ninakumbuka mara moja Mhe. Naibu Spika, tuliwahi kupitisha mswada hapa unaohusu mambo ya kuwasili watoto. Ule mswada jamii waliupokea vibaya na sisi Wajumbe pamoja na juhudi zetu tulizofanya kupunguza makali ya ule mswada, lakini haikutusaidia tulipata taabu na maneno makali sana huko katika jamii, kwamba tunakiuka miiko ya dini na haya maneno ni mengi sana, mengine kwa kweli hayakustahili hata kuambiwa, lakini tuliambiwa.

Sasa ndio nikasema ni lazima tuwe makini sana wakati wa kupitisha mswada. Sasa kifungu hichi (b) Mhe. Waziri, aliniambia kwamba kimefanyiwa marekebisho, lakini nimejaribu kuangalia hizi karatasi za marekebisho zote mbili sijaona, ikiwa kimerekebishwa ni sawa, lakini kama hakijarekebishwa nilikuwa naomba sana maneno haya yafutwe kabisa, yaani haya maneno yanayosema "ile kupinga dhana iliyopitwa na wakati kuwa mwanamme ndio mtawala".

Maneno haya nilikuwa naomba yafutwe kwa sababu hata kama yana nia njema, lakini yanaleta msabaha wa kwenda kinyume maelekezo ya dini. Kwa

sababu *Quraani* inasema "*Alrijaali Qawaamuuna ala Nnisai"* na hii aya ni maarufu kweli kweli na kila mtu anaijua.

Sasa kusema kama ni upotofu kwa mwanamme ndio mtawala, watu wanaweza wakaja wakatafsiri kwamba tunakwenda kinyume na ile aya, sasa ikaleta mashaka makubwa sana katika jamii. Kwa hivyo, ili kuepusha hayo, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, akubali dhana hii bora iwemo, tusije tukawapa watu maneno bure ya kusema. Ninasema hivyo kwa nia njema kabisa kwa sababu ni kweli kuna wanaume tunawaonea wanawake sana na tunawadhalilisha sana, lakini hatujafikia pahali pa kuifuta ile aya inasema kwamba wanaume ndio wanaowasimamia wanawake, hii aya itaendelea kuwepo.

Sasa tutafute lugha ya kuja kuchafuana na watu bure. Nilikuwa naomba ikiwa kuna uwezekano na *inshaallah* uwepo basi ni bora tuitoe au tutafute lugha nyengine kidogo iliyokuwa ni rahisi ambayo haileti ugumu wa namna hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 324. Pale kuna kifungu cha 12 kuna kifungu kidogo cha 6. Lakini nilitaka nizungumzie kifungu (3) na (4) kwanza.

Naomba nikisome kifungu cha (3) kinasema;

> "Matokeo ya kupima virusi vya ukimwi kwa mchangiaji wa damu au maji au kiungo cha mwili yatakuwa ni siri na hayatatolewa kwa mtu anayetaka kusaidiwa"

Yaani hapa picha inakuja kwamba kuna mtu anataka kusaidiwa kiungo, sasa akatokezea mtu mwengine kumsaidia huyo mtu kiungo. Masharti ya sheria hii lazima apimwe virusi vya ukimwi. Sasa akishapimwa huyu anayetaka kusaidiwa ambaye ndiye mgonjwa basi asije akaambiwa matokeo. Ndio tafsiri niliyoiona kwenye kifungu hichi cha (3).

Sasa ukisoma kifungu cha (4) kinakwenda kinyume na hicho. Kifungu cha (4) kinasema;

> "Mtu anayetaka kusaidiwa maji au kiungo cha mwili, anahaki ya kuthibitishiwa yeye mwenyewe au muangalizi wake uhakika wa majibu ya vipimo vya virusi vya ukimwi"

Sasa hii kama ni *contradiction* ya hivi vifungu. Kimoja kinasema asiambiwe na kimoja athibitishiwe matokeo. Sasa mimi ninafikiri hiki kifungu cha (3) ni afadhali tungekifuta tukabakisha hichi cha (4) na hichi cha (4) kikawa cha (3)

sasa. Maana yake ni haki yake kuthibitishiwa kwamba hicho kiungo anachotaka kuingizwa mwilini mwake, basi kipo salama hakina virusi vya ukimwi.

Sasa hichi kifungu cha (3) kama nilivyokifahamu ndivyo kitakuwa kinakataa yeye kujuulishwa. Sasa naomba hicho ni afadhali kingefutwa kikabakishwa kifungu cha (4).

Halafu ukisoma kifungu cha (6) kimetoa adhabu kwa mtu anayetaka kinyume na masharti ya vifungu hivi, lakini adhabu iliyotolewa Mhe. Naibu Spika, mimi naona ni ndogo. Ni ndogo kwa sababu kama mtu atafanya kwa makusudi kumuingiza mtu kiungo cha mtu ambacho kimaathirika na virusi vya ukimwi, maana yake huyo mtu amemsababishia mwenzake mauti kama kwamba ni muhalifu. Sasa mhalifu kupewa adhabu ya shilingi milioni mbili au tatu au miaka miwili au mitatu jela, mimi ninadhani hiyo adhabu ni ndogo.Ili kuweka adhabu inayostahiki, mimi ninadhani tungechukua adhabu kubwa zaidi ingawa maisha ya mtu hayalipiki kwa vyovyote, lakini angalau miaka kumi, kwa sababu ni maisha ya mtu ukishamtia kiungo ambacho kimeshaathirika umeshamuuwa yule.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo ninadhani nimalizie kwa kifungu cha 20.

Kifungu cha 20 kipo ukurasa wa 327.

Kifungu cha 20 (1) kinasema;

> "Kwa mujibu wa sheria hii hakuna mtu atakayemlazimisha mtu mwengine kupima virusi vya ukimwi"

Maana yake kupima ni hiyari na huko nyuma tunakotoka kila mtu ana wajibu kupima afya yake. Tushaanza *contradiction.* Lakini nilichokusudia kusema hapa, mimi nilikuwa naomba hiki kifungu kifutwe au kirekebishwe, wala hakuna haja ya kurekebishwa kwa sababu hichi cha huku nyuma tayari kimeshasema ni wajibu wa kila mtu kupima afya yake.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, unapoweka hiyari hii. Hata hapa Mhe. Naibu Spika, tangazo linasema kwamba wapimaji wapo nje, mimi sijamuona hata Mheshimiwa mmoja aliyeinuka pengine wanataka kuchangia, lakini wengine wanakwepakwepa.

Sasa *argument* yangu ni kwamba tunaweka hiyari ya kupima virusi vya ukimwi, hatutofika pahali siku moja tukawa na takwimu halisi. Maana yake takwimu tunazocheza nazo ni wale waliokubali tu kwenda kupima ukimwi

ndio takwimu ambazo tunazofanyia kazi, lakini uhalisia kuna watu wengi hawajapimwa na miongoni mwa hao pengine wengi wameathirika hatuwajui. Kwa hivyo, takwimu zetu hizi za kusema sijui tuna asilimia 0.6 sijui ngapi, mimi naona haijawa halisi kama hatujawapima Wazanzibari wote.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba kifungu hichi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, akubali tukifute na akibakisha kile cha zamani kinachosema ni wajibu wa kila mtu akapime afya yake. Na tusiishie tu basi pia tuseme kama mtu hakupima virusi vya ukimwi atakuwa amefanya kosa la kisheria na ikiwa muda umepita hajapima, basi kuwe na adhabu japo ndogo kuhimizahimiza.

Tukitoka hapo kuna kifungu alikigusia Mhe. Salma Mohammed Ali hapa, hicho kifungu (2) kwamba watu watakaolazimishwa ni wale watakaolazimishwa kwa amri ya Mahakama au wale wanaotaka kuchangia viungo au watuhumiwa wa makosa ya kujamihiana na akinamama waja wazito. Hata mimi nilikuwa ninaungana na Mhe. Mama Salma kwamba ni wale wanaotaka kufunga ndoa bora na wao wawekewe sheria, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hii nayo inawasababisha maambukizi na watu ni wanyambi katika dunia hii, anaweza akajiona ameathirika, halafu akanyamaza kimnya.

Sasa ikiwa anakwenda kumposa mtoto wa watu ambaye hakuathirika, ikiwa hakuna ulazima wa kupima basi huyu mtu anaweza akasababisha maambukizi kwa mtu mwengine, maambukizi ambayo kama angepima yasingekuwa ni ya lazima.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba na mimi nitilie nguvu yale maneno ya Mhe. Salma Mohammed Ali kwamba nao wanataka kufunga ndoa na wao waende wakapime, sheria hii maana yake iwalazimishe wakapime virusi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Chonga, naunga mkono sana mswada huu. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wauchangie kwa nasaha zote na hatimaye tuupitishe tuweze kupunguza maambukizi ya virusi vya ukimwi, lakini pia tuweze kuwatendea haki za binadamu wale ambao wameathirika na virusi vya ukimwi.

Ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Naibu Spika**: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hamza Hassan Juma na wale wenye nia ya kuchangia walete majina.

**Mhe. Hamza Hassan Juma**: Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka nikushukuru kunipa nafasi hii jioni ya leo nikaweza kuchangia mswada huu muhimu sana kwa afya zetu, lakini vile vile na kwa wananchi ambao waliotuleta hapa Barazani. Na mswada huu kama unavyojieleza kwamba ni Mswada wa sheria wa kuweka masharti ya kukinga na kusimamia masuala ya ukimwi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli maradhi ya ukimwi, lakini vile vile na maambukizo ya ukimwi, hili ni tatizo la taifa na kwa kweli ipo haja kuanzia serikali yetu kupitia Tume ya Ukimwi, wizara zote za serikali na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hata na Mahakama kwa kweli tunatakiwa tushirikiane kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba mswada huu wa sheria tuweze kuupitisha, lakini vile vile uweze kutekelezwa vizuri.

Hivyo,watakaoweza kukiuka sheria au watakaoweza kukiuka masharti ya sheria hii, basi Mahakama wenzetu wajitahidi kuchukua hatua zile zinazopaswa ili kuhakikisha kwamba sheria hii inatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, suala la ukimwi kwa kweli ni suala zito na mimi naomba sana mswada huu ni muhimu sana. Kwa hivyo, nitapendelea hasa mimi nikiwa Mwenyekiti katika hili Baraza la Wawakilishi ambalo kamati yangu vile vile inasimamia haya mapambano dhidi ya maradhi sugu ya ukimwi. Basi nitaomba sana Waheshimiwa sote tujaribu kutoa mchango wetu wa mawazo katika mswada tuuboreshe pale ambapo tunapohisi kuna kasoro tuweze kusema na Mhe. Waziri, yupo makini sana, yupo tayari anakusikilizeni.

Sisi kamati katika marekebisho ambayo tuliyoyafanya tumefanya marekebisho ambayo mengi sana na tunamshukuru sana Mhe. Waziri, kwa usikivu wake, kwa kweli amekubaliana na mapendekezo haya pamoja na yale ambayo sisi hatukuyaona vizuri na wao vile vile wamefanya marekebisho. Kamati yako imefanya kazi kubwa sana kuupitia mswada huu. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa na sisi tuuchangie mswada huu ili tuweze kuisaidia jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nilikuwa ninataka nianze huku kwenye tafsiri. Suala la kwenye tafsiri ilivyozungumzwa waathirika wa ukimwi, kuna baadhi ya Waheshimiwa wameanza kuwa na hofu na hii tafsiri.

Mimi ninataka niseme Wazanzibari wote na Watanzania, sisi ni waathirika wa ukimwi, wala tusikatae sote, kwa sababu unajua tunashindwa kutofautisha hizi tafsiri. Mtu aliyepata maambukizi ya virusi vya ukimwi, yule tunamwita mtu aliyepata maambukizi. Lakini yule aliyeathirika hata sisi jamii kwa

sababu mfano wewe katika hayo mambo ambayo ya kijamii tayari tumeshaekewa tahadhari nyingi, hiyo ni moja katika athari.

Vile vile, katika familia zetu ninategemea sijui kama kutakuwa kuna familia, ninavyokusudia familia sio lazima wale munaokaa katika nyumba moja, lakini katika ukoo na katika ukoo sisi tunakutana mazikoni, harusini, lazima katika jamii yetu tutapambana na watu ambao tayari wamepata maambukizi. Sasa ile ni athari kwa sababu leo ukisikia ndugu yako au jamaa yako yeyote amepata haya maambukizi, ile wewe kujisikia unyonge na kumsikia yule mnyonge, ile ni athari.

Kwa hivyo, hii ndio athari ambayo iliyokusudiwa. Sasa mimi ninataka niseme Mhe.Naibu Spika, Wazanzibari sote, sisi ni waathirika na kwa kuwa ni waathirika ina maana tuwajali wale waliopata maambukizi. Kwa nini nikasema hivyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi imekuwa mtu akipata maambukizi ya ukimwi anaona kama ni balaa katika mtaa, anaonekana kama yeye ni mtu wa uasharati mkubwa sana katika jamii, wakati kumbe sivyo. Tumeangalia humu katika makundi wenye maambukizi, kuna wengine mpaka watoto wadogo na wengine walizaliwa na maambukizi, sasa hivi wameshakuwa watu wazima. Je, na wao pia utasema ni waasharati.

Kwa hivyo, mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, hii tafsiri ya waathirika tusiogope. Hii ni tafsiri ambayo lazima tukitaka tusitake, hii lazima na sisi ni sehemu. Sasa kwa nini watu wakawa wanaogopa kuitwa waathirika, kwa sababu bado katika akili zetu tuna *mind set* za unyanyapaa.

Mhe. Naibu Spika, leo humu ndani akitokeza mtu mmoja tu, akisema jamani nimepata maambukizi, basi tayari humu ndani tutaanza kutengana, kama ulikuwa unakunywa maji naye pamoja utajifanya tu upo karibu naye, lakini utaanza kumnyanyapaa.

Sasa mimi naomba sisi tuwe mabalozi wa wananchi wetu, tukae nao hawa ambao walioamua kujitokeza, wao wameshapata ushauri nasaha na ndio maana wameamua kujitokeza, tuwape moyo. Leo Mhe. Naibu Spika, kuna familia, sisi kamati yangu imekaa na wenzetu hawa wa jumuiya mbali mbali, wale ambao wamepata maambukizi, lakini vile vile wale wanaharakati ambao wapo katika harakati za mapambano dhidi ya ukimwi.

Kwa kweli maelezo waliokuwa wanatueleza utatoka machozi. Leo kuna familia wanawatelekeza mpaka jamaa zao. Mtu anapata maambukizi anaumwa wanapigiwa simu *ZAPHA+*, wanaambiwa njooni mchukue

mgonjwa wenu, hii! jamani leo ndugu zetu hawa wa *ZAPHA+* kujitolea kutoa taaluma, lakini vile vile kuondoa hofu katika jamii, leo ina maana tunawatupia mpaka jamaa zetu, itafika pahala nafikiri watapigiwa simu waambiwe njooni mchukue maiti yenu, wakati *ZAPHA+* ile ni jumuiya tu ambao wao wamekaa pale kusaidia haya mapambano.

Wenzetu hawa wanajitahidi wanatoa huduma mpaka kwa wale waliopata maambukizi ambao tayari wameshaanza kupata athari za maradhi, wanakwenda wanawasaidia namna gani ya kutibu. Kuna wagonjwa Mhe. Naibu Spika, jamaa zao wanashindwa kuwashughulikia. Lakini hawa wenzetu wanaharakati wanakwenda wanasaidia tiba, wanawahudumia.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana jamii yetu tuondokane na unyanyapaa na tuone maradhi haya ya Ukimwi ni sawa sawa na maradhi mengine. Mimi niseme kwamba labda watu wakisikia mtu kapata maambukizi, wanaona kwamba huyu kesho au keshokutwa anakufa. Sio kweli.

Mhe. Naibu Spika, ulifanywa mkutano mmoja Afrika ya Kusini tumeangalia. Kuna watu ambao walikwenda kujitangaza kwamba mtu ana maambukizi kwa miaka 25, akipita hapa Mhe. Naibu Spika, shingo lazima itapata tabu. Lakini ana miaka 25 ana maambukizi. Kwa sababu nchi za wenzetu haya masuala ya kushughulikiana sana maana yake unajua labda hizi tabia zetu kwamba tunapenda sana kuandafiana maisha ya mtu, na hii nafikiri ndio inayotufanya hata tukipata maambukizi tunakufa kwa haraka kwa sababu hofu, mtu anaona tabu mtaani, jamii inamtenga, kweli mtu atakufa mapema.

Kwa hivyo, mimi nadhani jamii ikiondoa hofu, nadhani hata maambukizi yatapungua. Mwenzangu alizungumza kwamba maambukizi sasa hivi yamekuwa yakiongozeka. Mhe. Naibu Spika, nataka niwapongeze sana ndugu zetu wa *ZAC;* Tume ya Ukimwi, kwa namna wanavyoweza kutoa elimu, na hii elimu ambayo wameitoa kwa muda mrefu imesaidia sana kudhibiti maambukizi mapya ya maradhi ya ukimwi. Hii elimu ya ushauri nasaha ambayo wanayoitoa. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, imesaidia sana.

Leo ukiangalia hizi takwimu Mhe. Naibu Spika, kila siku zinaambiwa zinaongezeka kwa sababu watu wamepata elimu, wamepata ushauri nasaha wanajitokeza wenyewe kwenda kupima. Hata ukiangalia katika hizo takwimu utakuta kama wamekwenda watu 1,000 wanaonekana labda watu 10 ndio wamepata maambukizi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema tujisifu kwamba maambukizi kwa Zanzibar sio makubwa. Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, kama ingekuwa hakujatolewa

elimu ya kutosha ya maambukizi ya ukimwi, kutokana na *population* ya watu wa Zanzibar ya 1,300,000, sasa hivi hali ingekuwa kubwa sana. Hasa kwa bahati nzuri Zanzibar sisi ni visiwa huwezi ukatoka na gari ukaenda mpaka Morogoro, ukienda Tanga, ukienda Dodoma au kwengineko. Hapa lazima uvuke.

Kwa hivyo, bado watu wengi hawana fursa ile ya kuvuka kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, kuwa suala zima la unyanyapaa tukiweza kuliepuka hili hata haya maambukizi mapya yatapungua.

Mhe. Naibu Spika, kuna haya makundi hatarishi katika jamii yetu kuna hawa ndugu zetu ambao wanatumia dawa za kulevya, bangi na pombe. Maeneo haya ni hatarishi. Rafiki yangu Mhe. Maalim Saleh Nassor Juma, yeye eneo lake kule Vitongoji anasema sasa hivi linaitwa *mortuary*, linaitwa *mortuary* kwa sababu ukifanya masihara huna mchezo wa mbali pale utaingia pahala pabaya.

Kwa hivyo, maeneo kama haya mimi naomba sana ndugu zetu wa *ZAC* mmejitahidi sana kutoa elimu, elimu hii iendelee kutolewa hasa katika makundi haya hatarishi. Elimu kubwa mnatoa, lakini bado tunaomba muendelee na hatua hiyo.

Jengine ambalo nataka kulizungumza Mhe. Naibu Spika, katika mswada huu, limejaribu kuzungumzwa suala zima la kutonyanyapaliwa wakati wa kutafuta ajira. Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa serikali tunashukuru, isipokuwa kuna eneo moja tu na hili bado naomba sana Waziri anayeshughulikia Idara maalum hapa sasa hivi hayupo, lakini najua mawaziri wote wanafanyakazi kwa pamoja.

Bado katika ajira ya idara zetu maalum, suala la upimaji wa virusi vya ukimwi linaangaliwa sana. Sasa hii ni sehemu ya unyanyapaa, kwa sababu mtu sio kwamba akiwa na maambukizi ndio tayari kuwa ni mgonjwa hawezi kufanya kazi, unaanza kumkadiria lini atakufa, huo ina maana ni unyanyapaa.

Kwa hivyo, sasa hivi tunavyotaka baada ya kupitishwa sheria hii, kwa sababu sheria hii inasema fursa sawa kwenye ajira na kwenye huduma zote kwa watu ambao wenye maambukizi. Kwa hivyo, tunaomba sana wasije wakabaguliwa ndugu zetu, vijana wetu au kaka zetu wanapoonekana kuwa wamepata maambukizi, aidha ikawa ndio kigezo cha kusababisha kukosa kazi.

Vile vile, sio katika ajira tu hata katika fursa za masomo, tunajua kuna baadhi ya nchi na kwa kuwa kila nchi zina utaratibu wake, zile hatuwezi kuziepuka.

Kwa mfano China, hata Mhe. Abdalla Juma Abdalla, pamoja na uheshimiwa wake wamekwenda China, lakini ni lazima kwanza uoneshe cheti cha kupima. Kwa hivyo, pamoja na uheshimiwa wako, lakini tunafuata zile sheria za nchi yao, lakini kama wangekuwa hawana masharti hayo basi ungeambiwa tu tiketi yako hiyo hapo nenda zako China.

Kwa hivyo, kwa nchi kama hizi mimi naomba sana serikali yetu, kuna vijana sasa hivi ama wako vyuoni au wamo makazini, wasinyimwe fursa za kwenda kusoma kwa sababu wamepata maambukizi. Kikiweza kufanyika kitu hiki, mimi nasema Mhe. Naibu Spika, suala hili hatutolikubali na Waziri huyo itabidi sasa aje ajieleze vizuri hapa, kwa sababu yeye itakuwa ndio miongoni mwa watu ambao wananyanyapaa. Sasa hili naliomba sana.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa *private sector*. Mhe. Naibu Spika, suala hili bado lina matatizo na kuna miongoni mwa watu ambao walifukuzwa kazi baada ya kupima na kuonekana wana virusi vya ukimwi. Sasa baada ya kupita sheria hii tunakuomba sana Mhe. Waziri, ambapo sheria hii utakuwa wewe ndio unaisimamia, basi yakija malalamiko kama haya tunaomba sana serikali iweze kuchukua hatua, na kwa sababu tunapitisha sheria, kwa hivyo tusiwe tunapitisha sheria lakini bado watu wetu wakawa wanaendelea kunyanyaswa.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta binafsi bado suala la unyanyapaa hasa kwa watu ambao wamepata maambukizi suala hili lipo na tunaomba sana. Kwa upande wa serikalini bado hatujapata taarifa kwamba kuna watu wanapopata maambukizi wanakuwa wananyanyapaliwa, lakini kupatiwa huduma za afya. Waheshimiwa Mawaziri ambao nyinyi ndio mnaoongoza wizara, tunaomba sana.

Kwa sababu mtu akishapima virusi akionekana amepata maambukizi basi aweze kupata haki zote au huduma zote. Sisi nafikiri katika kila wizara kuna fungu tumepitisha maalum kwa ajili ya mapambano dhidi ya ukimwi. Mapambano yale moja ni kutoa elimu, vile vile, na wale waliopata maambukizi waweze kusaidiwa huduma mbali mbali ili waweze kuwa na afya nzuri na kuendelea kulitumikia taifa letu kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika suala zima la upimaji wa hiyari. Katika sheria hii inasema kwamba mtu hatolazimishwa kupima labda kwa dharura maalum kama sheria hii ilivyotaja. Suala hili limefanywa kwa makusudi kwa sababu bado suala la kupima, ingawa Mhe. Abdalla Juma Abdalla pale alisema suala la kupima likiendelea kuwa la hiyari kwa kweli maambukizi yataongezeka. Suala hili la kupima kwa hiyari linakuja pale ambapo elimu ya kutosha inakuwa imetolewa.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tumewaona humu watu mbali mbali ambao afya zao zilikuwa zimedhoofu sana, lakini baada ya kupima na kuonekana wamepata maambukizi, wakapata ushauri nasaha na wanatumia huduma za kidaktari wanaonekana wako vizuri.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, na wale wengine ambao hawajapima basi bado tunaendelea kusema kwamba watu waendelee kupima ili kuweza kujijua afya zao na kwa sababu Mhe. Naibu Spika, inavyotakiwa mtu ukishapima ukionekana umepata maambukizi, basi unatakiwa umueleze mwenza wako. Kwa mfano kama umeoa au umeolewa, na isiwe sababu kumueleza mwenza wako tena ndio ikawa sababu ya ndoa kuvunjika. Kwa sababu haya Mhe. Naibu Spika, pia tulipokaa na wadau tuliyakuta.

Kwa mfano mtu anakwenda kupima amepata maambukizi anakuja nyumbani anamwambia mumewe. Sasa yule mume badala na yeye aende akapime, maana yake hajulikani nani aliyemuambukiza mwenzake, moja kwa moja mume anampa talaka mkewe. Baada ya kuwa mtu ameshapata yale maambukizi, sasa yule anahitaji mapenzi zaidi, anahitaji apate nasaha nyingi ili kumliwaza ule moyo wake mpaka arudi katika ile hali ya kawaida, leo mtu unamuongezea adhabu nyengine, baada ya adhabu ya maradhi unamuongezea adhabu nyengine. Mhe. Naibu Spika, suala hili kwa kweli sio jambo jema hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumza hapa kwamba wake zetu wanapokwenda kujifungua twendeni tukapime pamoja, ndio, kwani tunaogopa kitu gani. Au kwani hutaki mtoto mwengine, sasa unaogopa nini. Sasa mimi nafikiri twendeni tu na kama unaogopa ni sababu gani inayokufanya uogope, hakuna sababu.

Hata hawa wenzetu wa Wizara ya Afya siku zote wanatupa ushauri nasaha na hata kliniki tunaambiwa twende na wake zetu, sasa kutokana na shughuli nyingi ndio muda mwingi tunawaachia wao wenyewe wanakwenda. Kwa sababu yule mtoto anayekuja kuzaliwa ni wenu na atahitaji matunzo ya baba na mama.

Vile vile, kama mama amekwenda kupima pengine akaonekana na maambukizi na wewe ukaenda kupima kama hukuonekana na maambukizi basi mtaweza kuishi tena maisha marefu. Kwa sababu wamo humu watu, utamkuta mama hana virusi na baba ana virusi au unamkuta baba hana virusi na mama ana virusi, kwa sababu utakuta wamepata ushauri nasaha hawanyanyapaliani wao wenyewe na mtoto anayezaliwa anakua anaishi katika afya nzuri kabisa.

Kwa hivyo, na mimi nilikuwa najaribu kutoa ushauri kwa wananchi wetu, na kwa kuanzia sisi wenyewe, tukiondoa huu unyanyapaa basi watu wengi watajitokeza kwa ajili ya kupima, kujua afya zao na vile vile kuweza kupata tiba.

Lakini hapa Mhe. Naibu Spika, imeelezwa katika kifungu cha 38 suala la usiri kwenye kupima. Mhe. Naibu Spika, bado watu wetu wengi wanaogopa kwenda kupima kwa sababu wana hofu ya zile siri zao kuweza kutolewa nje. Sitaki kusema imetokezea hapa.

Lakini Bara kuna kipindi tuliwahi kusikia katika hii miezi ya kuadhimisha siku ya ukimwi. Kuna dada mmoja aliwahi kuzungumza kwamba yeye alisema alikwenda kupima, basi hajatoka hata pale hospitali, alianza kupewa pole. Ina maana hospitali alikuwepo yeye na daktari, anaanza kupewa pole. Hi! Yeye anaanza kujiuliza hii pole ya nini, ina maana yule ambaye alimpima tayari ameshavujisha siri zake.

Lakini hapa katika kifungu hiki cha 38 kimemzuia daktari kutoa siri za mgonjwa na yule mtu akishapimwa hata kama ameonekana na maambukizi, basi bado jukumu la kuieleza aidha jamii inayomzunguka, familia yake na wengine bado ibakie kwa yeye mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana pale unapokwenda kupima, kwanza kuna dakika 10 za yule mama utakayemkuta pale Mnazi Mmoja, tena anakueleza maneno mazuri sana, atakueleza hivi, atakuzungusha hivi na anakupa historia na mambo mengi, halafu anakwambia lete kidogo. Sasa pale unapopewa yale maneno unasahau kwanza kama ulikwenda kupima, ukishaambiwa lete kidogo ndio unakumbuka tena kwamba dah! Kumbe nimekuja kupima.

Kwa hivyo, ule ushauri nasaha anaokupa anakuondoa yale mawazo ya hofu, kwa sababu kuna wengine wanazimia hapo hapo. Mimi nawashukuru Wizara ya Afya wamefanya kazi nzuri sana ya kuwapa elimu wale watoaji wa damu, kwamba mtu anakupa ushauri nasaha pale, yaani mpaka pale unapima unakuwa hofu tena huna.

Kwa hivyo, tunashukuru kuwa kazi wanayofanya ni nzuri, lakini tunaomba kuwa hizi siri za wagonjwa zibakie ni za wagonjwa wenyewe. Sio za maambukizi tu ya ukimwi, ni kwa maradhi yoyote. Daktari anatakiwa kuwa iwe ni siri yake yeye na mgonjwa. Suala hili nilikuwa nawaomba sana madaktari wetu waliangalie na hili ndio litakalowafanya watu waweze kwenda kupima wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, bado watu wetu wana hofu na katika takwimu zinazotolewa, kwa kweli waliopata maambukizi kwa Unguja na Pemba bado ni wengi sana. Sina uhakika kwamba hii takwimu nitakayoitaja kama itakuwa ni sahihi au vipi, lakini hawapungui kwenye 5,000 au zaidi ya 5,000. Lakini wale ambao wanakwenda kupata huduma katika vile vituo, yaani wale waliojiunga kwenye ile Jumuiya ya *ZAPHA+* tunaambiwa ni 2,000 tu.

Kwa hivyo, bado kuna watu wengi ambao wamepata maambukizi, lakini kutokana na unyanyapaa wanaogopa hata kwenda katika zile taasisi kujiunga. Kwa sababu unajua tatizo letu watu wakikuona unaingia katika lile jumba, tayari wanaanza kuoneshana, jamaa tayari yule. Sasa ile ukimwambia mwenzako tu kwamba tayari yule, ina maana huo ndio unyanyapaa.Maana yake ukimwambia mtu tayari yule, tayari nini?

Kwa hivyo, unyanyapaa Mhe. Naibu Spika, huu ndio utakaotumaliza. Mhe. Naibu Spika, mimi nina wasi wasi hata wale ambao wanawaambukiza watu kwa makusudi, pengine na yeye anataka kuwakomoa, kwa sababu kama anasema nyinyi mnamnyooshea vidole basi na nyinyi atataka munyooshewe vidole vile vile, lakini tukiondoa hili suala la unyanyapaa Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani jamii yetu itakuwa iko huru sana na kuweza kwenda kupima wala hawana matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, ukiangalia kifungu cha 14(2), hapa ametakiwa Waziri wa Afya kuhakikisha kwamba huduma za upimaji, lakini vile vile huduma za tiba zinapatikana vya kutosha, tena kwa gharama iliyokuwa nafuu au bure kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nilikuwa nina wazo, unajua sio hospitali zote au vituo vya afya vyote ambavyo vinapima virusi vya ukimwi. Kwa hivyo, kama tunavyofahamu kuwa vituo hivi vingi vipo mjini, lakini vijijini bado vituo hivi vya kupima havipo vingi na hapa katika sheria hii Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri wa Afya ananisikia pale, kifungu hiki kimemtaka Waziri wa Afya kuhakikisha kwamba huduma hizi zinapatikana kwa muda wote.

Lakini katika vituo vya *private* Mhe. Naibu Spika, huduma hizi za upimaji hazipatikani kwa siku zote, yaani katika wiki unaweza kukuta zinapatikana mara mbili. Leo kwanza huyo mtu mwenyewe mpaka akishapata ushauri nasaha akiamua mwenyewe kwa hiyari yake kujitokeza kwenda kupima virusi vya ukimwi, basi hiyo shughuli inakuwa imefanyika kubwa kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mtu leo moyo wake umeshalainika anataka kwenda kupima, basi anaambiwa leo sisi hatutoi huduma ya kupima virusi

vya ukimwi. Wewe utegemee mtu yule siku ya pili atakwenda tena, haendi. Maana kutokana na unyanyapaa, waswahili wana msemo wao, wanakwambia *kisima hakirukwi mara mbili*. Sasa mtu keshaamua kukiruka mara ya kwanza, anakwenda pale anaambiwa huduma hii haipatikani.

Kwa hivyo, nitamuomba sana Mhe Waziri wa Afya atakapokuja kuchangia ili kuuboresha mswada huu, basi atuthibitishie na hivi vituo vya *private*, ambavyo walipewa mpaka hii ruhusa ya kuweza kutoa hii huduma ya damu salama, kuna sababu gani inayofanya kwa nini hawatoi huduma hizi siku saba kwa wiki, isipokuwa zile siku ambazo vituo vile vinafungwa.

Kwa sababu kama huduma hii itakuwa inapatikana kwa baadhi ya vituo tu Mhe. Naibu Spika, basi bado yale mapambano yetu yatakuwa hayajafikia ile asilimia 100, na tunakusudia mapambano haya na kwa kuwa tunakwenda kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kila pahala, ili wananchi waweze kupima afya zao, basi ni lazima kwa vituo vyote vitoe huduma.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, napenda nipate ufafanuzi Mhe. Waziri wa Afya aje anisaidie. Je, hivi vituo vyengine ambavyo havijaruhusiwa kupima virusi vya ukimwi, kuna sababu gani au hizi *reagent* ni chache na wakati katika huu mswada umeshasema katika kifungu cha 14;

Kifungu cha 14:

> "Waziri wa Afya atahakikisha upatikanaji wa vifaa na huduma wakati wowote"

Sasa Mhe. Naibu Spika, sheria hii inasimamiwa na Mawaziri karibu wawili. Kuna Waziri mmoja yeye anasimamia sheria na Waziri mmoja anasimamia utoaji wa huduma, ili hii sheria itekelezeke vizuri. Kwa hivyo, mimi nadhani lazima wawe na mashirikiano makubwa, humu imeshasemwa kwamba daktari yeyote atakayekuja kufanya tiba ya aina yoyote ikasababisha maambukizi, ina maana yeye atakuwa ni mkosa. Lakini ataingia katika makosa labda vile vifaa au huduma pengine hazikuwepo za kutosha katika vituo vile vya afya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati, maoni katika marekebisho ya vifungu kwa maeneo mbali mbali, nimejaribu kuyataja. Lakini kitu ambacho nataka kuendelea kusisitiza ni kwamba tuondokane na unyanyapaa kwa ndugu zetu hawa waliopata maambukizi, tusiwaone labda ni balaa kwetu, hawa ni ndugu zetu na tunatakiwa tuwajali.

Vile vile, katika maskuli Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya maskuli tuliwahi kupata taarifa kwamba kuna kijana mama yake aliamua kujitangaza kwamba

amepata maambukizi, basi wale watoto walifika pahala mpaka nyimbo wakawa wanamuimbia yule mwanafunzi mwenzao. Lakini tunashukuru baada ya kuingiliwa kati suala hili walimu waliweza kulirekebisha.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba sana sheria hii tukiweza kuondoa unyanyapaa, basi mimi naamini itaweza kutekelezeka vizuri. Baada ya hayo machache naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mswada wa kuweka masharti ya kukinga na kusimamia masuala ya Ukimwi kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Muumba kwa kutujaalia leo tukiwa wazima wa afya, lakini nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii. Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mengi ya kusema. Kwanza niipongeze sana wizara kwa kutuletea mswada huu, ambao ulikuwa ukihitajika kwa kipindi kirefu sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba mswada huu sio kinga tu kwa wale ambao tunasema wana virusi vya ukimwi, lakini ni kinga ambayo itasaidia hasa katika kutekeleza yale majukumu ya
wizara na taasisi mbali mbali, lakini vile vile yataweza kusaidia katika kuweka sheria mbali mbali zinazohusiana na masuala ya ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo nimeupitia mswada huu nimeona zimejitokeza kasoro ndogo ndogo ambazo nikitizama katika marekebisho ambayo yameletwa mbele yetu, nimeona kuwa nyingi ya kasoro hizo zimeweza kufanyiwa kazi. Lakini Mhe. Naibu Spika, labda na mimi nimsaidie mwenzangu ambaye amepita Mwenyekiti wa Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu Mhe. Hamza Hassan Juma, kusema neno la tafsiri ambayo wengi wameanza kulitilia shaka.

Waathirika, watu ambao wameathirika. Naweza kusema kwamba kwa upande wetu sisi Wazanzibari sote ni waathirika wa ukimwi. Mhe. Naibu Spika, ninaposema muathirika, kwa hali yoyote jamii ambao wengi wanaopata maambukizi ya ukimwi ni vijana, nguvu kazi ya taifa tunaowategemea katika kuzalisha uchumi wa nchi hii, wakiondoka au wakiathirika kwa maradhi haya, ina maana sisi sote ni waathirika. Naomba sana suala hili tulijue, kwamba tunaathirika kwa sababu wanaoathirika wengi ni vijana, na vijana ndio tegemeo letu katika uchumi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa nataka tu kusema kwamba kwa sababu mimi sio mwanasheria napata tabu sana katika lugha ambayo huwa inatumika

kwenye hii miswada yetu au hizi sheria zetu na ninajua kwa nini ninapata tabu. Napata tabu kwa sababu tafsiri inayotoka moja kwa moja kwenye Kiingereza na Kiswahili inanipa tabu sana. Suala hili limekuwa katika miswada mingi inayokuja hapa. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu ambaye yeye miswada mingi inapitia kwake, kuna baadhi ya maneno linakuwa neno moja.

Kwa mfano Juzi tulipokuwa tunapitia mswada wa Baraza la Vijana, neno "kushajihisha" mimi ninavyofahamu ni kushajihisha sio kushajiisha. Lakini juzi nikaambiwa kwamba hapana, hili neno sio kushajihisha ni kushajiisha. Kwa bahati nzuri hapa naliona katika kifungu cha 2(b) katika ukurasa wa 319, naona limejirudia, lakini huku limerekebishwa na kusema kwamba neno "kushajiisha" lisomeke "kushajihisha". Sasa wakati mwengine tunatafuta *uniformity* ya maneno, neno lile lile moja katika mswada huu linatumika vyengine, neno lile lile katika mswada wa juzi, Mhe. Mwanasheria Mkuu tizama tena utakuta limetumika neno lile lile maana ile ile lakini limeandikwa vyengine.

Kwa hivyo, ningeomba sana wakati wa kufanya hizi tafsiri tuangalie sana, kwa sababu hizi za Kiswahili ndio tunazozisoma sisi pamoja na wananchi. Kwanza kuhakikisha kwamba zinaeleweka vizuri, halafu kunakuwa kuna msongamano wa maneno, hilo ni tatizo jengine. Neno lipo moja kwa moja.

Kwa mfano naweza kusema kwamba kuna sentensi nimeiona ambayo inajizungusha, badala ya kuja moja kwa moja ili kufahamu nini kinazungumzwa. Bahati mbaya sana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najitayarisha vizuri, umenishtua, lakini tutaendelea. Kuna neno ambalo linaonesha kuwa hapa hii sentensi haikukaa sawa.

Kwa mfano, kuna kifungu cha 4(a) kimeandikwa:

"Kuchukua hatua zinazofaa kujua hali yake virusi vya ukimwi"

Kwa Kiswahili hapa kidogo haijaeleweka. Sasa mimi nimeiweka hivi, nimehisi kwa nini tusiseme kuchukua hatua zinazofaa kujua afya yake sio hali yake, na mara nyingi tunapozungumzia suala la Ukimwi tunazungumzia afya, kujua afya yake kwa kupima virusi vya ukimwi. Nafikiria hiyo ingekuwa ni sahihi na ingeeleweka zaidi kuliko namna ambayo imewekwa. Nimeona katika marekebisho vile vile, lakini nahisi hata hapa kwenye marekebisho bado kuna tatizo la kueleweka ile sentensi. Kwa hivyo, nahisi kwenye upande wa lugha kuna matatizo. Kwenye upande wa lugha nimetizama kwa bahati mbaya sikutizama yote, lakini kila nikitizama ile *construction* ya lugha kwa Kiswahili na ambayo itakuwa inaeleweka vizuri bado ina utata mkubwa.

Kwa hiyo, sijui tutafanya nini, lakini kwa kweli nimehisi ipo haja ya kuwa na lugha yetu ya sheria ambayo itakuwa zaidi inaeleweka kuliko kuwa na tafsiri za moja kwa moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nimehisi kuna kipengele kimoja ambacho kinazungumzia suala la kulazimisha, ukurasa wa 313. Kulazimisha humu imetafsiriwa, naomba niisome.

> "kulazimisha" kuhusiana na kitendo chochote chini ya Sheria hii, maana yake ni kitendo cha kumlazimisha mtu bila ya ridhaa yake, kwa njia ya kutumia nguvu, vitisho, kuteza nguvu au njia ya aina yoyote ya kumlazimisha"

Mimi ningeomba sana Mhe. Waziri, tuweke na kutumia nafasi yake au cheo chake. Kwa sababu sasa hivi wengi wanatumia nafasi zao au vyeo vyao kwa kuwadanganya vijana wetu kuwapatia kazi. Lakini kwa bahati mbaya sana badala ya kupata kazi wanapata maambukizi ya ukimwi. Kwa hivyo, ningeomba sana hilo tulitilie maanani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache labda katika kumpongeza Mhe. Waziri, lakini niipongeze sana Tume ya Ukimwi, ambayo kwa kipindi kirefu sana imekuwa ikifanya kazi vizuri. Ningesema kwamba Tume ya Ukimwi tangu ilipoanza kutoa elimu ya ukimwi, haitoi elimu ya ukimwi kwa kundi moja tu, lakini vile vile elimu yao mara nyingi wanaitoa kwa kufanya utafiti wa hali ya juu. Na hii ndio elimu, unapotoa elimu ni lazima ufanye utafiti ni elimu gani ambayo inahitajika kwa makundi gani.

Mhe. Naibu Spika, elimu katika suala la ukimwi ni muhimu sana, kwa sababu elimu ndiyo ambayo itasababisha kupunguza maambukizi ya ukimwi kwa ujumla wake kwa makundi tofauti. Lakini vile vile, elimu itasaidia katika kuondosha unyanyapaa kwa waliopata maambukizi ya ukimwi. Sote mwanzo maambukizi ya ukimwi yalivyoingia katika jamii yetu tulikuwa hatujui, tulikuwa tukikimbiana.

Leo kuna watu wanafunga ndoa na ambao mmoja kapata maambukizi na mwengine hana. Hii inatokana na elimu ambayo imetolewa na Tume ya Ukimwi, mimi nawapongeza sana. Kwa kweli kazi wanayoifanya sio kazi rahisi.

Sisi kama binaadamu tuna itikadi zetu, tuna desturi zetu, tuna mila zetu, tuna ufahamu wetu, kila mtu ana ufahamu wake. Ilikuwa suala la maambukizi ya ukimwi kutokana na ufahamu wa watu tofauti, wengine walikuwa hawafahamu kwa nini elimu ile inatolewa. Lakini kwa kutumia mbinu na

wataalamu tofauti walionao wameweza kufikisha elimu ile katika makundi tofauti.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba wanastahiki sifa na kwa kweli wapewe kila motisha ya kuweza kuendelea na kazi ile. Hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, zimetoka takwimu za kuonesha kwamba Ukimwi unaongezeka.

Lakini mimi niseme kwamba kwa asilimia inayoongezeka na laiti ingelikuwa elimu hii haitolewi ya ukimwi katika makundi na watu mbali mbali, asilimia hii leo tungejikuta kwa upande wa Zanzibar pengine labda asilimia ya walioathirika na virusi vya ukimwi ni wengi mno. Lakini kwa sababu ya elimu inayotolewa ambayo elimu hiyo ni ya kisayansi imesaidia sana katika kupunguza maambukizi ya Ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, suala la unyanyapaa ni changamoto na kuwanyanyapaa wale waliopata maambukizi ya ukimwi. Mimi niseme kadiri tunavyowanyanyapaa wale ambao wamepata maambukizi ya ukimwi kwa sababu wataficha ndio kadiri tunavyochochea maambukizi ya Ukimwi. Mimi ningewasihi sana wananchi wenzangu tujaribu kuishi na wale wote ambao wamepata maambukizi ya ukimwi kuishi nao kama ni watu wa kawaida, tuyachukulie maradhi ya ukimwi ni ya kawaida. Lakini na sheria vile vile ziwalinde ili wapate haki zao za binaadamu kama kawaida.

Hawa ni binaadamu hakuna anayetaka kupata maambukizi ya ukimwi, hakuna. Mimi sijapata kusikia mtu anayefanya kwa lazima ili apate maradhi. Na kwa nini wanyanyapaliwe waliopata maambukizi ya ukimwi, lakini wengine wasinyanyapaliwe ambao wana maradhi chungu nzima. Kwa bahati nzuri sasa hivi ukimwi sio unaoua zaidi kuliko maradhi mengine. Kuna maradhi mengine ambayo yanaua zaidi.

Wagonjwa wa Ukimwi wakifuata utaratibu ambao wanapewa, wakitumia dawa wanaweza kuishi zaidi hata kuliko watu wengine ambao ni wazima, lakini kubwa wanataka *psychological support* kutoka kwetu sisi, tukiwabagua ina maana tunawaua. Hakuna kitu kibaya kama mtu kumtesa kisaikolojia, anapojiona kwamba hapewi haki zake za msingi kama binaadamu kwa sababu ya maradhi bila shaka tutakuwa jamii hiyo basi tunaiteketeza. Mimi nimpongeze sana Waziri, niipongeze sana Tume kwa kazi nzuri ambayo inafanywa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa namuomba sana Waziri na nalisema hili kwa sababu linaanza kunitia khofu. Mheshimiwa tunakubali katika makundi ambayo yapo katika hatari ya kupata maambukizi ya Ukimwi tunayo na yamejitokeza. Kwa bahati nzuri utafiti umeonesha dhahiri kwamba makundi

haya yameathirika sana. Lakini wasi wasi wangu mkubwa katika kuyafikia makundi haya tuhakikishe kwamba mila na desturi zetu tunazifuata. Nasema hivyo kwa maana.

Kuna baadhi ya wafadhili wana utaratibu wao, wana mila zao na sisi tuna mila zetu. Sasa makundi haya yanaweza kuwa yanakubalika katika nchi nyengine. Sisi makundi haya bado hatujayakubali. Inavyotolewa elimu wenzetu wana mbinu za kuingia wakafika. Lakini mimi naomba sana tuchukue tahadhari ili kuhakikisha yale yanayotoka nje yasije yakafika hapa.

Nafikiri Mhe. Waziri, ananifahamu vizuri sana kwa sababu yeye mtu mzima kama mimi. Yale ambayo yapo nje yasije yakafika hapa kwetu, elimu itolewe vizuri sana kwa makundi haya, lakini tuhakikishe sisi ni waumini wa dini; tuna waumini wa Kiislamu, waumini wa Kikristo, lakini tuna mila na desturi zetu. Tukianza kufuata wenzetu wanavyofanya hasa kwa kuyakamata makundi haya tutakuwa tunakwenda pabaya.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri, hilo tulitilie maanani kwa sababu ni kitu ambacho mimi nakifahamu vizuri sana na najua kinaweza kikatokea. Ningeomba sana wakati tunapofanya kazi zetu, sikatai mimi makundi haya lazima tuyaangalie vizuri, nakubali kabisa, lakini tujue mbinu gani tunawafikia. Na tuhakikishe kwamba ile mitandao ambayo itataka kuwafikia kwa njia nyengine tuhakikishe kwamba tuikatae mitandao hiyo.

Mhe. Waziri, baada ya kumaliza hayo na mimi nikupongeze tena wewe binafsi kwa kazi na juhudi yako ambayo kwa kweli tunaiona na inatuletea matunda mazuri. Lakini pia, nikupongeze kama mwanamke mwenzangu kwa sababu tunasema tunaweza sio kwa kuwezeshwa, lakini tunaweza na ina-*prove* hivyo hata hapa Barazani Mhe. Waziri, pamoja na Waziri wa Maendeleo ya Wanawake ina-*prove* kwamba wanawake tunaweza. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri, ambaye ameweza kutuletea Mswada huu kwa kazi nzuri pamoja na watendaji wake mpaka wakaweza kufanikisha kutuletea Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa lakini nikasema na mimi kwa suala hili nichangie japo kidogo. Nataka nianze Sehemu ya Tatu kifungu cha 5(1), naomba ninukuu.

Kifungu cha 5(1):

> "Tume itatoa elimu kwa wananchi kuhusu chanzo, sababu, njia za maambukizi, athari, na mbinu za kujikinga kudhibiti, kusimamia Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa watu na makundi yote"

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme elimu inajitahidi kutolewa kwa kweli, juu ya chanzo na sababu kwa hivi sasa wengi wanafahamu, kwa sababu hili janga limetupata muda mkubwa sasa. Lakini mimi nasema serikali bado ichukue juhudi za makusudi, kwa sababu inaonekana athari za maambukizi zinaendelea siku hadi siku, baada ya kutegemea labda zipungue lakini athari zinaonekana zinaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka niseme serikali bado iwe makini juu ya suala hili, kwa sababu kama vyanzo vipo na vinaeleweka ni kwa nini tusianze kujitahidi kuzuia vile vyanzo ambavyo ndivyo vitatufanya sisi angalau labda tuna kinga fulani. Lakini tukiachia wakati vyanzo tunajua kwamba vipo na bado tunaendelea kuvifumbia macho niseme bado tatizo hili litaendelea kutuathiri kwa muda mkubwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, vyanzo tunavielewa vingi vipo. Kuna zinaa ipo kwa wingi sana, kuna ambao wanafanya kwa kujificha lakini wapo wanaonekana wazi wazi, lakini bado serikali inaachia. Wapo watu wanaojiuza na wanaonekana lakini haionekani hatua yoyote inayochukuliwa. Ulevi umekuwa mwingi sasa hivi Zanzibar unaweza soda ukaikosa lakini pombe isikosekane ipo kwa wingi sana.

Na hivyo ndivyo vyanzo vyenyewe ambavyo tunavijua, watu wanasema kwamba "*pombe ni mama wa maasi*". Sasa hivi mabaa yapo kwa wingi, mikesha ya magoma iliyokuwa haina sababu zozote ipo kwa wingi na humu ndimo inamokuwa mikutaniko ya watu kwa wingi. Serikali ingeangalia jambo hili na ikaweza kuchukua hatua na taratibu basi nadhani tungeweza kupunguza chanzo hicho cha maambukizi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika kifungu cha 5(2)(a) kifungu hicho kinasema zitatolewa kampeni za elimu ambazo zinataka kutolewa, zitatolewa kisayansi na kwa kutumia utaratibu wa ushahidi ulio wazi. Elimu ya ukimwi itolewe kisayansi, itolewe kijiografia, itolewe kihistoria, kama sisi wenyewe hatubadiliki basi bado maambukizi yataendelea. Kwa sababu hapa baada ukishalijua lile jambo basi tayari wewe uchukue hatua za kujirekebisha.

Mhe. Naibu Spika, nikienda tena katika kifungu cha 5(2) (d), Mwakilishi mwenzangu hapa mchangiaji wa mwanzo kabisa alikisema kifungu hichi na mimi nataka nikitilie mkazo. Kifungu hiki naomba nikinukuu.

Kifungu cha 5(2) (d):

> "zitaelekezwa kwa makundi ya kijamii mitazamo ya kitamaduni, imani na mazoea ambayo yanapelekea madhara na mahusiano ya kijinsia yasio sawa, kuhusu kujikinga na Virusi vya UKIMWI, udhalilisha kijinsia na usawa wa kijinsia na kupinga dhana iliyopitwa na wakati kuwa mwanamume ndio mtawala"

Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kwa kweli mimi ni mwanamke nami naungana na wenzangu wanaopinga udhalilishaji wa kijinsia, ukandamizwaji wa mwanamke na mimi sipendelei itokezee hivyo, lakini bado nasema mwanamme bado ni kiongozi. Hili halikataliki, kwa sababu asilimia 99 wananchi wa nchi hii ni waislamu, kwa hivyo bado katika muongozo wetu wa dini hapa unaelezwa "*Arrijaalu Qawwaamuna*".

Kwa hivyo, hii haipingiki. Mwanamke awe na madaraka mpaka ya uraisi, na mumewe awe mchunga punda lakini akirudi nyumbani bado yupo chini ya amri ya mumewe, ukubwa wake na uraisi wake utakaa pembeni na atakuwa bado yupo katika uongozi wa mwanamme. (*Makofi*)

Kwa hivyo, sisi tupiganie yale yetu lakini tusije tukavuka mipaka ya kuona labda umemzidi. Mwanamme bado ni kiongozi kwa sababu ametambulika kidini. Kwa hiyo, mimi nasema bado tuichunge na sisi tudai haki zetu, kwa sababu haki zetu zipo na ziko wazi. Bado tutaendelea kuzidai na tupewe zinapostahiki kupewa lakini bado kiongozi mwanamme ataendelea kuwa kiongozi. Kwa sababu hata katika nyumba tu wewe na mama watoto nyumbani na unajua kwamba baba ndiyo kiongozi halafu wewe unakuwa kiongozi wa pili, hilo halipingiki.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mchango wangu huu nije katika kifungu cha 18(1) hapa mimi bado nahitaji ufafanuzi zaidi sijapafahamu vizuri, Mhe. Waziri utakapokuja hapa naona hiki mimi unifafanulie, naomba nikinukuu.

Kifungu cha 18(1):

> "Mtu haruhusiwi kumpima mtu virusi vya ukimwi mpaka mtu huyo awe ameruhusiwa kufanya hivyo na Waziri anayehusika na Afya"

Sasa hapa mimi huwa najiuliza Waziri wa Afya tuliyonaye hivi sasa babu Juma Duni hapa yupo, sasa kama kasafiri ina maana hatoruhusiwa mtu kupimwa mpaka aje apate amri yake au kutakuwa kuna utaratibu gani. Nilikuwa hilo nataka nilijue. Kwa sababu Waziri anakuwa hafi, kwa sababu Waziri ni cheo hata akiondoka atakuwa mwengine, lakini Waziri kama mtu anaweza akasafiri, anaweza akapata dharura nyengine akawa hayupo. Kwa hivyo, ule muda ambao hayupo ni utaratibu gani ambao utatumika au huduma hizi ndio zitasita.

Kifungu cha 18 (2):

> "Mtu hatoruhusiwa kutoa ushauri kabla na baada ya kupima chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii, mpaka awe ameidhinishwa na Waziri"

Naona hakuna tofauti kubwa hapa mimi nilikuwa nataka ufafanuzi uje unifafanulie vizuri ili niweze kuelewa. Lakini hapa kifungu hichi kinaeleza hivi, lakini na hivi sasa kuna utaratibu au siku hizi tuseme kuna elimu watu wanajipima sukari wenyewe, wana mashine zao wanajipima. Hapa kifungu mtu tu haruhusiwi kumpima mtu mwengine lakini je, ukimwi anaweza kuwa na mashine akajipima yeye mwenyewe. Hapa pia nilikuwa nataka nijue, kwa sababu siku hizi elimu inakuwa siku hadi siku.

Halafu Mhe. Naibu Spika, tuna ndoa hizi za ughaibu, ambazo mtu anaweza akaposa mtu yupo Ulaya mke yupo hapa lakini akasema aolewe mke yule halafu apelekewe mkewe. Mtu kama huyu utaratibu unakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee kutoa pongezi kwa wenzetu hawa niseme kwa elimu wanajitahidi sana, tangu lipatikane jambo hili elimu inatolewa kwa wingi. Lakini mimi nataka tujiulize je sisi ambao tunaletewa elimu hiyo tunaizingatia kwa kiasi gani.

Kwa sababu kama mwalimu atasomesha tu ukisha ukamuachia yale aliyokwisha kusomesha akaondoka nayo mwenyewe na wewe ukaondoka na sifuri maana yake elimu hiyo bado haijatusaidia. Elimu ni kitu muhimu sana, lakini na kuzingatia ile elimu pia ina umuhimu mkubwa sana. Elimu hii baada ya kuipata kama ilikuwa hatujaipata basi mimi naomba elimu hiyo tuifanyie kazi kwa kubadilisha mwenendo wa tabia zetu, kwa kuacha kabisa mambo ya zinaa au mambo yale yote yanayosababisha vyanzo hivi vya kupatikana ukimwi ikiwemo hiyo zinaa, ulevi, madawa ya kulevya, haya yote mimi naomba tungeepukana nayo ili hii elimu ikaweza kufanya kazi na yale maambukizi mapya tukaweza kunusurika nayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema mchango wangu utakuwa mdogo lakini nilisema nataka nichangie machache tu katika Mswada huu. Kwa hivyo, kwa upande wangu naunga mkono Mswada huu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba na wenzangu wauchangie Mswada huu kwa sababu una malengo mazuri ya kuweza kutukinga na kutushauri wananchi wa nchi hii. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi angalau kusema chochote katika hoja iliyo mbele yangu.

Mhe. Naibu Spika, na-*declare interest* kwamba mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu ambao tuliupitia huu Mswada kwa kina. Kwa mnasaba huo sina sababu ya kusema niukatae Mswada huo, lakini kwa niaba yangu na kwa niaba ya watu wa jimbo la Wawi nitatumia fursa hii kutia nyalio tu baadhi ya mwahala ili chungu kisije kikaungua.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuangalia jina la huu Mswada unaosema kwamba Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Kuathirika na Virusi vya Ukimwi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kwa bahati mbaya siku ya mwanzo sikuwepo kwenye Kamati nikatoa mawazo yangu katika hapa.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana kwamba Mswada huu umezungumzia zaidi ya wale watu ambao walioathirika au wamo katika hatari ya kuathirika jinsi ya kuwalinda na kutowanyanyapaa, lakini Mswada huu haukuweka nguvu katika hawa watu ambao hawajapata maambukizi.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni lazima tuwe makini sana serikali inapoletwa Mswada wake katika vyombo kama hivi. Mimi ni mzoefu sana katika masuala haya ya Mabunge haya ya *Commonwealth* nimefanya kazi katika Mabunge mawili, hili Bunge la Zanzibar na lile Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hivyo ni mzoefu sana katika masuala ya kutunga sheria katika Mabunge haya.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana serikali haipo *serious* katika ku- *excavate* zile *main causative agents* ya tatizo, kuling'oa tatizo na mizizi yake, wanaleta mambo juu juu. Mimi nilipokuwa nafanya kazi katika lile Bunge la Jamuhuri ya Muungano nilikuwa napitisha sheria ya ubakaji pale ili kuondosha ubakaji katika nchi.

Tuliletewa sheria ya Ubakaji na tukatunga sheria kwamba ukimkonyeza tu hivi, kumkonyeza mwanamke bila ya ridhaa yake ni *temptation to rape* na ni kosa. Sasa mimi nilidhani hapa Mheshimiwa katika sheria hii tungeweza kukazania zaidi wale ambao hawajaathirika wasiathirike na kutia nguvu kwa kuondosha yale mambo ambayo yangeweza kuleta Ukimwi katika nchi, lakini la kusikitisha ni kwamba sheria imepita sana juu ya kuwanyanyapaa.

Mimi naunga mkono kwamba tusiwanyanyapae hawa ni walipa kodi wenzetu, hawa ni walipa kodi wenzetu, hawa ni wananchi wenzetu, hawa ni watoto wetu, hawa ni miongoni mwetu, kama si leo ni kesho, Mwenyezi Mungu tunusuru, unaweza ukawa na wewe ni muathirika na hili, unyanyapaa ni ubaguzi na ni dhambi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini nimelazimika kusema kwamba mswada huu umeangalia upande mmoja tu kuwalinda walioathirika na wale walio mahali hatarishi ya kupata ukimwi. Lakini ukiangalia kwa mfano kipengele cha 33(1) ulinzi wa wanawake na wasichana yaani sheria imetilia nguvu kwamba hawa tuwalinde ili hata kujamiiana lazima ipatikane ridhaa yao, kitu kama hiki. Lakini haikueleza sheria hii jinsi ya kuwalinda wavulana na wanaume, iko *bias*.

Mheshimiwa tukiangalia kwamba siku moja nilibishana na Mheshimiwa Waziri wa Sheria hapa kwamba chanzo kikuu cha ukimwi ni *sexual intercourse*, kujamiiana. Na huwezi kufanya *sexual intercourse* bila ya kuona mambo haya ambayo yanapelekea *sexual intercourse*. Nilimwambia kwamba *sexual intercourse* ni *hormonal process* akapinga.

Lakini huu ukimwi utaendelea, hatutofika 03 sisi hapa, kwa sababu hatujataka kung'oa mizizi ya ukimwi. Ile sheria aliyonambia Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba ipo ya mwaka 1973 mimi siijui, lakini kama ipo naomba atuletee hapa ili tuisome sheria namba 1 ya *garment act* ya 1973 naomba utuletee Mheshimiwa hapa tuione na tuifanyie marekebisho iwapo imepitwa na wakati.

Mheshimiwa vimini vinavyovaliwa sasa hivi humu ni tatizo, kinamama wanavaa viguo vifupi. Na Mheshimiwa ukishaona kwa jicho, jicho linapeleka hisia katika kichwa na kichwa kikishapeleka hisia katika kiungo cha uzazi kichwa hiki kikishaharibika basi tena inakuwa ni tatizo nakupelekea tatizo la UKIMWI.

Mimi ninafikiria Mheshimiwa ujitahidi sana katika hili, sheria hii ilikuwa kiwemo kipengele cha kuwalinda wavulana na wanaume katika masuala ya ukimwi kwa kuzuia vimini na nguo zisizokuwa na stara. Lakini kwa hivi

tunavyoendelea, ukimwi utaendelea kuwepo kwa sababu jicho likiona moyo unatamani na nafsi inataka kukidhi haja, hapo sasa!

Sasa sheria yetu Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu tusaidie ili tufikie 03, lakini ukija kufanya mchezo tutarudi kwenye 01 na tutabakia hapo hapo kwenye 01 na 03 hatufiki hata siku moja kabisa kabisa, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, musiwe na huruma. Yaani nyinyi mnasema kuvaa nguo fupi ni haki ya binaadam, je kupoteza maisha, wakati sheria mama Katiba ya nchi inasema haki ya kuishi ni haki ya msingi. Leo wewe unavaa kimini akutamani uje umpe ukimwi unamuondoshea haki yake ya msingi.

Mheshimiwa ukienda huko Darajani kunatisha, wanavaa nguo nyembamba zinawabana mpaka nini halafu na vifulana vimefika hapa wanakupitia hapo, kwa nini sasa tusiung'oe mzizi wa maambukizi mapya kwa kuwazuia wanawake wasivae vimini katika nchi hii. Sasa nadhani tutunge sheria ya mavazi kusudi sambamba na hii sheria tunayoitunga hivi sasa. Nakuomba sana Mwanasheria Mkuu na hao *draft men* wako mtuletee sheria ya *garment act*.

Sasa Mheshimiwa kuhusu kipengele nambari 32 jinsi ya kuwalinda watoto waliomo katika mazingira hatarishi, watoto wanawake, wasichana na walemavu. Lakini kuna vijana ambao wanaishi katika mazingira ya shule *boarding school*. Kwa mfano mimi katika jimbo langu ipo *Fedel Castro Secondary School* imekusanya vijana wabichi kabisa, wachanga kuanzia tangu *Form I* mpaka *Form VI* lakini ile skuli Mhe. Naibu Spika, kuna *club* ya pombe inaitwa *mortuary* kakisema Mwenyekiti wangu pale Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mimi nilifikiri sheria ingeweka kwamba katika maeneo ya serikali kama vile shule na taasisi nyengine muhimu vilabu vya pombe ni marufuku kabisa. Pale vijana wetu Mheshimiwa unajua ni wanafunzi, ninafikiri walimu wenzangu wanajua tabia za wanafunzi, *students are curious in nature that means they want to know more than that they know.* Kwa *khulka* zao wanafunzi ni wanafunzi, ni watundu wanataka kujua kuliko kile wanachokijua ndio tafsiri yake hiyo maneno niliyosema.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba tu Mhe. Spika, katika hoja yangu hii kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atuongezee neno, vilabu vya pombe na sehemu za starehe visiwepo katika maeneo nyeti.

Mheshimiwa mimi katika hili nilikuwa ninatia nyalio kwa sababu huu mswada ni wangu lakini ninawaombeni sana Waheshimiwa tuisaidie serikali na tuwasaidie waathirika wa mambo haya ya ukimwi kutowabagua, hawa ni

watoto wetu, ubaguzi ni dhambi kubwa. Mwalim Julius Nyerere alisema naomba nimnukuu Mhe. Naibu Spika."Hakuna dhambi mbaya kabisa kama ubaguzi", leo ukishaanza kumbagua mgonjwa wa ukimwi au anaeishi na virusi vya ukimwi, kesho utambagua mwenye *typhoid*, keshokutwa utaanza kumbagua mwenye malaria na hatimae kuja kumbagua hata aliye na *flue*, hili ni tatizo Mheshimiwa.

Kwa hivyo, ninawaombeni sana Waheshimiwa katika hili tuyafuate maneno ya mwana falsafa wetu bwana Julius Nyerere kwa kutowabagua hawa tuishi nao ni sehemu yetu na katika hili Mheshimiwa kwa sababu kamati yangu ndio iliyopitisha hili, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache kuchangia mswada huu wa sheria ya kuweka masharti ya kukinga na kusimamia masuala ya ukimwi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Waziri na nimpongeze kwa kuwasilisha mswada huu, mswada ambao utawalinda na utalinda haki za binaadamu kwa watu wanaoishi na walioathirika na *VVU* na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sie mjumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu, lakini hata hivyo naunga mkono mia kwa mia mswada huu na naomba wajumbe wengine ambao watafuatia waunge mkono mswada huu, wauchangie na baadae waupitishe ili tuone kwamba hawa wenzetu ambao wameathirika ingawa tunaambiwa sote tumeathirika, ili tuone kwamba sisi sote tunalindwa na mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu tunaamini kwamba utabadilisha dhana potofu ambayo jamii wanayo juu ya watu ambao wameathirika kwa namna moja au nyengine. Lakini kwa sababu sio wote walioathirika ni wahasherati kama Mhe. Hamza Hassan Juma, alivyosema, wapo ambao ni *innocent*, wameathirika pengine kwa njia nyengine japo Mhe. Saleh amesema 85% wanaathirika kwa ile njia ya kujamiiana. Wako wanaozaliwa nao, lakini pia wapo wale ambao wanaathirika kwa njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika,mimi *concern* yangu ya kwanza ilikuwa katika sehemu ya Kwanza  sehemu ya tafsiri kifungu cha (2). Kwanza kulikuwa na neno ulemavu niliona lime-*appear* mara mbili lakini nimeangalia marekebisho ya kamati na naipongeza kamati kwa kuliona hilo kwamba ile tafsiri ya mwanzo imefuntwa.

Lakini nilikuwa nina *concern* ndogo katika hii tafsiri ya pili, tafsiri inasema kwamba kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya watu wenye ulemavu, katika mabano kuna neno hatuna fursa nambari 9 ya 2006. Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba hili neno hatuna fursa pia ni jina la hii sheria.

Lakini nikimaliza hapo Mhe. Naibu Spika, naomba niingie sehemu ya Tatu ambayo wajumbe wenzangu wamechangia kifungu cha 2(d), Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Salma wameonesha *concern* yao juu ya dhana ya mwanamme ndio mtawala. Mhe. Naibu Spika, kama Mhe. Panya Ali Abdalla, alivyosema kwamba mimi ni mwanamke kama yeye na naunga mkono kampeni hii ya elimu kwa makundi ya jamii, kiutamaduni na imani na mazoea ambayo yanapelekea madhara.

Mhe. Naibu Spika, labda wajumbe wenzangu wanawake ambao kila siku tuko nao pamoja katika kupinga mambo ya kutawaliwa pamoja na kwamba tunajua mwanamme ndio mtawala, lakini mimi nitoe wasiwasi kwamba labda yale maneno yaliyotumika pale ndio ambayo yanaleta utata katika dhana nzima ya hii elimu ambayo itaenda kutolewa huko katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa ninapendekeza labda kifungu hiki kisomeke, ninaanzia pale penye udhalilishaji kijinsia na usawa wa jinsia na kupinga dhana ya mfumo dume, naona hiyo iko sawa zaidi na itawatoa wasiwasi wanawake ambao wamezoea kutawaliwa na waume zao. Mwanamme atabaki kuwa mtawala, ndio, lakini pia tupige vita ile dhana ya mfumo dume.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia kifungu cha 2(e) ambacho kinasema kwamba taarifa ya elimu ifanyike mashuleni na katika taasisi nyengine za elimu, chuo cha mafunzo na kizuizini. Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nilikuwa nataka kuomba hizi taasisi za elimu tusisahau madarasa. Kwa sababu hivi sasa kumekuwa na baadhi ya walimu wa madarasa ambao wanafanya mambo ambayo pia hupelekea kuwepo kwa huu UKIMWI. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hii elimu itakapotolewa kusisahauliwe hizo taasisi za elimu.

Pia ninaomba hiyo elimu ambayo itakwenda kutolewa Mhe. Naibu Spika, basi itolewe kwa uwazi waambiwe kabisa madhara ya UKIMWI. UKIMWI ni nini na ukifanya nini unatapata UKIMWI bila ya kuficha, tuondoe ule muhali wa kuficha maneno, waambiwe kabisa waziwazi. Mhe. Naibu Spika, nitolee mfano wa nchi ya Uganda kwenye miaka ya 1990 na 2000 kuliwa kuna *rate* kubwa sana ya maambukizi ya UKIMWI, lakini wametumia huu mfumo wa kutoa elimu mashuleni na *alhamdulillahi* iliwasaidia kwa kiasi kikubwa sana, UKIMWI ulishuka katika nchi ya Uganda.

Kwa hivyo, naomba hii elimu izidi kutolewa japo kwamba wajumbe wenzangu wengine wamesema kwamba hata elimu ikitolewa kama sisi hatujabadilika huu UKIMWI bado utaendelea kuwepo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niingie katika sehemu ya Tano ya mswada huu kifungu cha 20, kijifungu kidogo cha 2 ambacho kinataka ridhaa kwa wale watu ambao watatakiwa kupima UKIMWI. Mhe. Naibu Spika, mjumbe mmoja amesema hapa kwamba siku hizi katika jamii yetu kuna hili suala la kupima kabla ya ndoa limezoeleka sana, na tunavyojua kwamba utaratibu ukizoeleka huwa sheria.

Na sasa kwa vile huu utaratibu umeshazoeleka, nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri, sana alifikirie hili ili tuone kwamba wale wote wanaotaka kufunga ndoa wanapitia utaratibu huu na kwa kuwa imeshakuwa utaratibu, sasa bora ikawa sheria moja kwa moja. Ninafikiri itasaidia, ninamuomba Mhe. Waziri, alizingatie hilo.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ya Tano kifungu cha 21 *subsection* (4) tumeelezwa kwamba naomba kunukuu, 'mtoto anaweza kupimwa ikiwa ridhaa imepatikana kutoka kwa daktari, mahkama, mzazi, mlezi au waziri anayehusikana, watoto au mtoto mwenyewe akiwa na umri wa miaka 16 au zaidi na awe na uwezo wa kufahamu athari za kupima'. Sasa Mhe. Spika, hapa mimi naona kumekuwa na dhana mbali mbali ya hii *age* ambayo mtoto ana-*refer* kama mtoto au anachukuliwa kama kijana.

Kwa sababu katika sheria namba 6 ya mtoto, mtoto ametafsiriwa ni kama chini ya miaka 15. Lakini katika sheria ya Baraza la Vijana ambayo tumeipitisha juzi tu kijana amechukuliwa kama mtu ambaye anaanzia miaka 15 hadi 35 pamoja na kwamba ilisema hivyo sheria, wapo waliopinga.

Lakini pia, kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, labda niombe muongozo kwamba inaonesha kuna mkanganyiko kwamba wale watoto wa kuanzia miaka 15 mpaka 17 pale hawajulikani kama ni watoto au vijana. Sasa nilikuwa naomba ufafanuzi kodogo, maana sheria hii imesema miaka 15 na kushuka chini ni mtoto.

Kifungu kinasema na watoto au mtoto mwenyewe akiwa na umri wa miaka 16. Sasa hawa kuanzia miaka 15 mpaka 17 ni mtoto, ni kijana, ni mabaleghe, sielewi, nilikuwa ninaomba labda muongozo. Na pia nilikuwa ninaomba muongozo kwamba sheria inapingana na sheria nyengine, zinapo-*contradict* ni sheria ipi ambayo ina *prevail,* kwa sababu tunajua sheria ikipingana na katiba, katiba ina-*prevail.*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kama nilivyosema mwanzo na ninashukuru kwa niaba ya vijana na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja, naunga mkono hoja. *(Makofi).*

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi na Walioathirika naVirusi vya UKIMWI na mambo yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kuchangia ningeliomba kupata ufafanuzi kuwa baadhi ya mambo kidogo ambayo yananikanganya katika mswada huu ili niweze kufahamu vizuri.

La kwanza ni ukurasa wa 312 sehemu ya Kwanza utangulizi kifungu cha (2). Kifungu hiki kinasema kuwa katika sheria hii isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo, mtu aliyeathirika kuhusiana na virusi vya ukimwi yaani *VVU* na UKIMWI vinajumuisha mtu ambaye anahusiana au anashirikiana na mtu mwenye au anaeaminika kuwa anaishi na virusi vya UKIMWI na kuendelea.

Sasa nataka nielezwe ikiwa huyu mtu umehusiana naye tu au unashirikiana nae kwa nini na wewe uwe muathirika wa UKIMWI kwa mujibu wa sheria hii. Halafu jengine ni kuwa imeshazungumzwa na Mheshimiwa aliyetangulia. Juzi tulikuwa na mswada hapa tukaambiwa, kijana ni mtu yoyote mwenye umri baina ya miaka 15 mpaka 35, lakini leo mtoto tunaambiwa ni mtu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 kwa sheria hii kama ilivyotajwa katika mswada huu. Hapa nataka maelezo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea ukurasa wa 317 sehemu ya Pili, kifungu cha 3 kinazungumzia kuwa pamoja na uwezo kazi za Tume zinazoainishwa katika sheria ya kuanzisha Tume ya Ukimwi, sheria nambari 3 ya mwaka 2002 Tume itachukua hatua zifuatazo:-

Kutoa taarifa na kuyaelimisha makundi yote katika jamii ikijumuisha watu wenye ulemavu kuhusu virusi vya UKIMWI, ukijumuisha na njia za maambukizi na namna ya kujikinga na kujisimamia. Hili neno 'kujisimamia' sijalijua maana yake naomba nipewe maelezo.

Halafu Mheshimiwa katika kifungu hiki tunajua kuwa UKIMWI haukuanza leo umeanza zamani na katika hatua za mwanzo watu walipofanya utafiti, wataalamu walitueleza kuwa wazanzibari ni asilimia 0.6 ndio walioathirika na ukimwi kwa wakati huo. Na serikali ilichukua juhudi kubwa sana ya kuelimisha pamoja na mambo mengine. Na tukishuhudia hivi sasa katika

Zanzibar nzima kila kwenye shehia kuna bango la ukimwi yaani, kuna kamati ya ukimwi na serikali ilikishirikiana na masheikh pia katika kutoa taarifa au kuelimisha watu kujikinga na UKIMWI.

Kwa wakati ule ilikuwa ni asilimia 0.6 ningeliomba kujua baada ya juhudi yote ile iliyochukuliwa kwa wakati ule mpaka hii leo, takwimu hasa watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI ni asilimia ngapi, imeongezeka au imepungua. Na kama imeongezeka ni sababu zipi serikali hapa haikutaja na serikali inachukua hatua gani ya kuona kuwa hizo sababu za kuongezeka inapambana nazo ili maradhi haya mazito yaweze kutuondokea.

Halafu pia katika kifungu cha 3(b) ukurasa huu wa 317 una maelezo yanasomeka kuchukua na kutekeleza kinga ya kitaifa ya
virusi vya UKIMWI, matibabu na mikakati ya uongozi. Lugha hii mimi siifahamu sijui imetafsiriwa vipi, naomba nipate maelezo.

Kifungu cha (d) Kifungu hicho hicho cha 3 kinasomeka, kuhakikisha kuwa taarifa na huduma zinazohusiana na virusi vya UKIMWI na ukosefu wa kinga mwilini pamoja na dawa muhimu zinapatikana kwa usawa tena bila ya ubaguzi. Mhe. Naibu Spika, kwa fikra zangu mwenyewe wakati huu tena si wakati wa kutumia neno bila ya ubaguzi, naona umeshapitwa na wakati na badala yake useme bila ya pingamizi yoyote, naona ingelikuwa ni neno zuri na ambalo linatia nguvu hii sentensi kuhusu mambo yaliyokusudiwa.

Na pia, kifungu (e) katika sehemu hiyo hiyo kinasoma kuhakikisha utoaji wa kinga dhidi ya virusi vya UKIMWI, matibabu, ushauri na msaada unaotolewa ningeliomba liongezwe neno mwisho, unaotolewa ipasavyo ili ionekane kuwa inafanyakazi kwa mujibu wa ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa ukimwi ni maradhi mabaya sana lakini ukiangalia humu inaonekana kuwa hawa watu wanaambukizwa virusi vya UKIMWI au wenye UKIMWI wanapokwenda kupima tunaambiwa taarifa zao ziwe za siri kabisa. Wakati tunajua mtu mmoja akiwa ana matatizo ya UKIMWI na mambo yake yawe ya siri tuseme akihama kwenda sehemu nyengine anaweza akaambukiza watu huko kupita kiasi, ikiwa kakusudia kufanya hivyo na wako watu walitokea kufanya hivyo.

Mimi nikitaka kujua pamoja na haki za binaadamu hii kuficha maradhi mtu kuekewa siri maana yake nini. Badala ya kutambuliwa na ikawa kinga kwa wengine ili maradhi haya ambayo mpaka leo hayana kinga yasiambukizwe. Na ikiwa ni siri kwa nini hii Tume katika kufanya kazi zake kama kushajiisha watu kutokana na mambo hayo ya ukimwi itakuwa ni pamoja na watu walioathirika.

Sasa wale watu wameshaathirika wamepimwa kwa siri lakini wanaingia katika Tume mbali mbali ili kutoa maelekezo kwa watu wengine ambao si waathirika. Kwa nini kule iwe siri, lakini huku wajitokeze. Hilo naomba vile vile nipewe maelezo.

Jambo jengine ukurasa wa 327 kifungu cha 5 (2) (d) kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, nikisome. Ni kuwa hapa kampeni za elimu na taarifa zinazoelezwa katika kijifungu cha (1) cha kijifungu hiki zitaelekezwa kwa makundi ya jamii, mitazamo ya kiutamaduni, imani na mazoea ambayo yanapelekea madhara na mahusiano ya kijinsia yasiyo sawa kuhusu kujikinga na virusi vya ukimwi, udhalilishaji kijinsia na usawa wa kijinsia na kupinga dhana iliyopitwa na wakati kuwa mwanamume ndio mtawala.

Mhe. Naibu Spika, tunajua wazi kuwa serikali haijiingizi katika dini ya mtu yeyote na kila mtu ana uhuru wa kuabudu dini anayoitaka, haijaingilia itikadi za watu katika dini zao, wala haijaruhusu kutungwe sheria yoyote ambayo itakwenda kinyume na maelekezo ya dini.

Mhe. Naibu Spika, leo umeniita *ustadh* naomba nitumie kidogo jina hilo kwa hiki kifungu, nimekiangalia na nimeambiwa na *Sheikh* wangu hapa Mhe., Rufai Said Rufai kuwa *Suratul Nissai* kuna sehemu imeeleza kuwa, *"Arrijallu Qawamuuna alannisai"*. Hii ni *Qur-ani* na *Qur-an* haina makosa na *Qur-an* itakwisha dunia hii haibadiliki, ni maneno ya Mwenyezi Mungu na mwenye kwenda kinyume na maneno ya Mwenyezi Mungu amekufuru.

Sasa siasa na haki za binadamu zisipelekee kutupeleka kukufuru sote. Mwenyezi Mungu kaumba wanawake na wanaume toka hapo asili na kuna waumini wa dini hii tangu asili kuliko hivi sasa, hakuna mwanamke aliyekuwa imamu, kwa nini? Tuangalie Mwenyezi Mungu alivyotuumba wanawake na wanaume halafu tuji-*assess* sisi wenyewe, leo useme mwanamme asimtawale mwanamke hivi Mwenyezi Mungu kakosea.

Kwa hivyo, neno hili ambalo wanasema kuwa ni dhana iliyopitwa na wakati kuwa mwanamme ndio mtawala ifutwe mara moja, ni kufuru. Tukitaka tusitake alivyoagiza Mwenyezi Mungu aliyetuumba yatosha zaidi na lazima tufuate maelekezo yake, au kama kuna aya nyengine inayofuta hii tuambiwe nifute maneno yangu.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu cha 11(d), Sehemu ya Nne, ukurasa wa 322 ambacho kinaeleza kwamba, kuhakikisha kuwepo kwa mipango madhubuti ya kupunguza madhara kwa watumiaji wa dawa za kulevya ili kupunguza ueneaji wa Virusi vya UKIMWI. Waheshimiwa mtu anapolewa huwa amelewa na baba wa maasi ni ulevi. Ulevi ni moja kati ya

mambo yanayosababisha ufuska na ni moja katika mambo yanayoeneza UKIMWI.

Hakuna sababu hata moja wala uwezo wa sheria hii ya kuweza kuhakikisha kuwa kutakuwa na mpango madhubuti wa kupunguza madhara ya watumiaji ulevi. Huyu mtu anayetumia ulevi akili yake ndio inayoharibika na kufanya mambo ambayo hayatakiwi, hivyo kuna mpango gani wa kuyapunguza haya. Hebu atupe maelezo hasa ni sayansi gani itakayotumika mpaka mlevi huyu aweze kuwekwa katika mazingira hayo yaliyoelezwa kwenye mswada huu.

Halafu Mhe. Naibu Spika, katika kuendelea na kupata maelezo ni kuwa kuna kifungu cha 27 na kifungu hiki kiko katika ukurasa wa 331 na kwa ruhusa yako naoma kukinukuu.

Kifungu 27(1) kinasema kwamba:

> "Uhuru wa mtu wa kuingia, kutembea au kusafiri ndani au nje ya Zanzibar hautazuiliwa au kuwekewa mipaka kwa kigezo kuwa mtu huyo anaishi, anaonekana au anadhaniwa kuwa na virusi vya UKIMWI"

Hivyo Mheshimiwa uhuru kama huu halafu Mwenyezi Mungu atupitishie mbali kama itatokea jambo ambalo sipendi liendelee kuwepo kutakuwa na nyumba ambayo wanaishi watu wenye virusi vya UKIMWI na wanajulikana kuwa wana virusi vya UKIMWI, kwa sababu ya haki ya binadamu na sheria hii na tunajua kuwa wanaharibu watu na haya ni mambo Mwenyezi Mungu kayaweka lazima yatokee yaani kujamiiana, hivyo tutawaachia tu wakae waharibu, watembee ovyo wenyewe wanakotaka. Mimi nahisi kama kweli tuna nia ya kutaka kupunguza madhara haya ya UKIMWI basi mambo yote ambayo yanaashiria mambo ya *sexual intercourse*, nitumie neno hilo, hapana budi kuyapiga vita.

Serikali yenyewe kwa kutumia jamii, mashekhe na kadhalika ili mtu ajione hasa mimi hivi ninavyotakiwa niwe iwe ni hivi na hivi isiwe kutokana na kujikinga na UKIMWI, lakini haki za binadamu ambazo zinatuletea madhara ni lazima tupambane nazo. Kwa nini iwe Zanzibar tu, kwa nini katika nchi za watu wengine hatuoni watu wanakwenda kama tunavyokwenda sisi na kuachiwa huru na kufanya wanavyotaka. Kwa hivyo, kifungu hiki cha 27 mimi sina imani nacho wala sikiungi mkono.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuna kifungu hiki cha 33(2)(c) ukurasa wa 334 ambacho kwa ruhusa yako naomba nikinukuu.
Kifungu 33(2)(c) kinasema kwamba:

> "Wajibu wa wanaume wa kutambua kwamba wana haki sawa katika kujamiiana na afya ya uzazi na madhara yake na kuepuka ubakaji, udhalilishaji wa kingono na udhalilishaji wa majumbani ikiwa ndani au nje ya ndoa"

Kazi hiyo Mhe. Naibu Spika, leo mswada huu unawapa wanawake nguvu na unawadhalilisha wanaume hata katika ndoa zao kiuwezo, hii ni hatari. Mhe. Naibu Spika, katika hali ya kawaida, naomba radhi Mheshimiwa umeniita *ustadh*, hata tuseme katika hali ya kawaida hata ikiwa mwanamke amechoka vipi na mashekhe wamo humu lakini mume ikiwa ndio hivyo na akikataa analaaniwa na malaika mpaka asubuhi.

Leo mtu huyu anasema hata ndani ya ndoa na kifungu cha juu kinampa mwanamke uwezo hata wa kukataa au wa kuamua analotaka kwa mumewe, jamani tunakwenda wapi, au tunaingia katika njia ambayo siyo. Tunajua Uislamu unapigwa vita dunia nzima sisi tumetumiwa kisaikolojia hapa kwa sababu ya UKIMWI.

Kwa nini Mhe. Naibu Spika, hatufuati maneno ya Mwenyezi Mungu aliyosema *'Walaatakrabu zinaa Innahukana Faahishatan Wasaa Sabiylaa'*, tukaingia katika mambo ambayo hayamo. Kwa sababu wizara hii ina mufti na mashekhe naomba watu wanapoingia katika vipengele vya dini kabla hawajatunga sheria zao waonane nao kwa maslahi yetu, tupo hapa, kesho tutakufa tukipuuza amri ya Mwenyezi Mungu tutakwenda pabaya au waniite mimi nije niwaelekeze.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kuchangia mswada, sasa naomba dakika tano tu za kuzungumza yangu mwenyewe. Mheshimiwa tunapambana na UKIMWI na mimi nampa pole sana Mhe. Waziri kwa sababu mambo ya UKIMWI ni mambo ya afya, kwa nini yasibakie katika Wizara ya Afya na mambo haya yakawekwa katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa uhuru huu tunaotoa katika nchi hii ya watu kuingia wanavyotaka, wakavaa wanavyotaka, wakafanya wanavyotaka tena vijana na ikawa sisi tunanyamaza kimya kwa sababu Zanzibar ni njema atakaye aje, hatuna njia hata moja ya kufanya UKIMWI uondoke hapa na badala yake utaongezeka.

Kwa hivyo, naishauri serikali pamoja na uhuru waliotoa wakae kitako kama kweli wanataka kuuondoa UKIMWI basi wahakikishe wanapambana na viashiria vile vinavyoleta UKIMWI kwa njia zote.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba kukaa kitako, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu wa tangu asubuhi hadi jioni. Lakini la pili nimeambiwa niwakumbushe kwamba kesho tuna semina ya kujengewa uwezo pamoja na keshokutwa, itafanyika hapa hapa kwenye ukumbi wetu asubuhi, muda mnaujua.

Kwa upande wa wachangiaji waliobakia ni watano tukijaaliwa roho zikifika, Jumatatu ataanza Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Abdalla Mohamed Ali, Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa na Mhe. Hassan Hamad Omar, lakini anayetaka zaidi ataleta jina lake.

Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao chetu hadi siku ya Jumatatu tarehe 16 saa tatu za asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 16/12/2013 saa 3:00 asubuhi)*